

**KATIKA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU
OMBI LA MAONI YA USHAURI NA. 001 YA 2024**

**KATIKA SUALA LA OMBI LA UMOJA WA WANASHERIA WA AFRIKA (PALU)
LA MAONI YA USHAURI KUHUSU KUTOAFIKIANA KATI YA ADHABU YA KIFO
NA MKATABA WA AFRIKA WA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**(Limetolewa chini ya Kifungu cha 4 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za
Binadamu na Watu wa Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za
Binadamu na Watu na Kanuni ya 82(1) ya Kanuni za Mahakama ya Afrika ya
Haki za Binadamu na Watu)**

YALIYOMO

YALIYOMO	2
1. Taarifa za Waandishi:.....	3
2. Wawakilishi wa Waandishi:	3
3. Muhtasari wa kweli muhimu	3
4. Masuala ya Kisheria	8
A. Adhabu ya kifo kwa asili inakiuka Kifungu cha 4.	13
B. Utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa uhalisia ni kumwondolea mtu uhai kikatili kwa kukiuka Kifungu cha 4.....	23
i. Ukosefu wa Mchakato Unaostahili Katika Utekelezaji wa Adhabu ya Kifo katika Uhalisia .	26
2. Kushindwa Kutoa Uwakilishi wa Kisheria wa Kutosha kwa Washtakiwa wa Adhabu ya Kifo	32
ii. Utoaji wa Adhabu ya Kifo Kibaguzi katika Uhalisia.....	36
1. Ubaguzi wa Kijinsia.....	37
2. Watoto.....	39
3. Ulemavu wa Akili.....	41
4. Umaskini	44
5. Lugha	50
6. Makundi ya Kisiasa.....	53
C. Utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo unakiuka marufuku ya Kifungu cha 5 kuhusu adhabu ya kikatili, isiyo ya kibinadamu au ya kudhalilisha.	56
i. "Mateso ya Kisaikolojia kwa Mtu Aliyehukumiwa Kifo" na Matokeo Mengine Yasiyoepukika ya Utekelezaji wa Adhabu ya Kifo Yanajumuisha Vitendo au Adhabu au Mateso ya Kikatili, ya Kinyama na Kudhalilisha	58
1. Mateso ya Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa.....	58
2. Wanawake na Watoto Wanaosubiri Kunyongwa.....	68
3. Athari kwa Wanafamilia	70
ii. Adhabu ya Kifo ni Ukiukaji Kabisa wa Kifungu cha 5	72
iii. Njia zote za Unyongaji ni Zinakiuka Kifungu cha 5	75
1. Kunyonga kwa kamba	79
2. Kupigwa mawe.....	80
3. Kupigwa risasi.....	81
4. Sindano ya Sumu	82
D. Athari ya jumla ya matatizo yote ya adhabu ya kifo yanaunga mkono uamuzi kwamba adhabu ya kifo haiafikiani na Mkataba wa Afrika na kanuni zingine za msingi za haki za binadamu.	83
E. Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu zote zinazoruhusu utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo.....	85
5. Je, kuna kesi zinazosubiri mbele ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu?	85
6. Muhtasari wa Ombi	88
7. Fahirisi ya Viambatisho	89

1. Taarifa za Waandishi:

Shirika:

Jina lililosajiliwa: PAN AFRICAN LAWYERS UNION

Nchi liliposajiliwa: TANZANIA

Anwani ya Posta na ya Mahali:

S.L.P 6069 Arusha, Nyumba namba 3, Barabara ya Jandu, Corridor Area, Arusha, Tanzania.

Simu: +255685078794

Barua pepe: legal@lawyersofafrica.org

2. Wawakilishi wa Waandishi:

Pan African Lawyers Union (PALU)

Nyumba namba 3, Barabara ya Jandu, Corridor Area

S.L.P 6065, Arusha, Tanzania

Simu: +255 27 250 3192/4

Barua pepe: legal@lawyersofafrica.org

3. Muhtasari wa kweli muhimu

1. Adhabu ya kifo, mauaji ya kukusudia ya mwanadamu yanayofanywa na Serikali, inajitofuatisha na hatua nyingine zote za adhabu. Kufungwa gerezeni kunahusisha kumwadhibu mtu kwa kumnyima uhuru na fursa, kumtenganisha na jamii, na hatimaye, mara nyingi, kumrekebisha ili aweze kuungana tena na familia yake, aingie tena katika jamii, na kutoa mchango kwa wengine. Adhabu ya kifo, kwa upande mwingine, inajumuisha kuodnoa uhai wa mtu. Ukatili wa adhabu ya kifo unaanzia wakati hukumu inatolewa hadi wakati inatekelezwa. Taarifa ya hukumu ya kifo inamfikia mtu kwa hofu kubwa kwamba, ikiwa na endapo Serikali itaamua, itamchukua na kumuua. Na utekelezaji wa hukumu ya kifo unahusisha mateso, ukatili na kudhalilishwa. Hakuna njia ya kibinadamu ya kumuua mtu.
2. Adhabu ya kifo ni ya kikatili, ya mwisho na isiyoweza kurekebishwa, na ni zaidi ya aina nyingine zote za adhabu. Ni jambo lililopitwa na wakati

ambalo haliendani na haki zilizowekwa katika Kifungu cha 4 na Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ("Mkataba wa Afrika" au "Mkataba"). Adhabu ya kifo ni dhihaka kwa kanuni ya msingi ya Kifungu cha 4: "Maisha ya binadamu hayapaswi kuharibiwa." Na kwa sababu adhabu ya kifo inakabiliwa na mapungufu katika mchakato wake na inatolewa kwa njia ya kibaguzi na kikatili, inakiuka agizo la Kifungu cha 4 kwamba "kila mwanadamu atakuwa na haki ya uhai wake kuheshimiwa na uadilifu wa utu wake. Hakuna mtu anayeweza kunyimwa haki hii kiholela." Aidha, adhabu ya kifo haiwezi kutolewa au kutekelezwa bila kusababisha adhabu na vitendo vya kikatili, vya kinyama na udhalilishaji, kinyume cha Kifungu cha 5 cha Mkataba.

3. Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Tume ya Afrika" au "Tume") imetambua kwa muda mrefu kutoafikiana kwa adhabu ya kifo na haki hizi na sheria za kimataifa za haki za binadamu, na imeendelea kutoa wito wa kukomesha adhabu ya kifo katika kipindi cha miaka 25 iliyopita.¹
4. Wanachama wengi wa Umoja wa Afrika wanatambua hili pia, kama ilivyoonyeshwa na mwenendo wa kuacha kutoa na kutekeleza adhabu ya kifo na kuelekea kuikomesha kabisa. Katika bara zima la Afrika, nchi nyingi sasa zimepiga marufuku adhabu ya kifo kwa makosa mengi ya uhalifu, kupitia marekebisho ya katiba, uamuzi wa mahakama au utungaji wa sheria.² Leo, zaidi ya asilimia 80 ya nchi za Kiafrika zimeondoa adhabu

¹Angalia infra ¶¶ 27-32.

²Angalia Kiambatisho C (Jedwali la hali ya sasa ya adhabu ya kifo katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika). Kwa kuangalia mifano kadhaa ya hivi karibuni, mnamo mwaka 2023, bunge la Ghana lilirekebisha sheria ya jinai ("Sheria ya Makosa ya Jinai") ili kuondoa adhabu ya kifo kama adhabu inayotambulika kisheria, isipokuwa kwa makosa ya uhaini wa kiwango cha juu. Angalia Ghana Abolishes the Death Penalty, EQUAL JUSTICE INITIATIVE (Julai 27, 2023), <https://eji.org/news/ghana-abolishes-the-death-penalty>. Zambia ilikomesha adhabu ya kifo kwa njia ya marekebisho ya sheria yake ya adhabu na ulinzi mwaka 2022 na 2023. Angalia Penal Code Amendment of 2022, GOVERNMENT OF ZAMBIA, Act No.

23 (Des. 23, 2022),

<https://www.parliament.gov.zm/sites/default/files/documents/acts/Act%20No.%2023%20Penal%20Code%20%28Amendment%29%2C%202022.pdf>; Defence (Amendment) of 2023, GOVERNMENT OF ZAMBIA, Act No. 12 (Dec. 26, 2023), <https://zambialii.org/akn/zm/act/2023/12>. Na mnamo Aprili 2020, Bunge la Chad liliazimia kukomesha adhabu ya kifo kwa kila aina ya uhalifu. Marion Chahuneau na Melissa Verpile, Chad's National Assembly abolishes the death penalty for all crimes, PARLIAMENTARIANS FOR GLOBAL ACTION, (Apr. 28, 2020), <https://www.pgaction.org/news/chad-abolishes-death-penalty-all-crimes.html>. Nchi kadhaa za Umoja wa Afrika pia zinafikiria kuwa na sheria inayolenga kukomesha adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria, ikiwa ni pamoja na Zimbabwe,

ya kifo kwa sheria au hawatekelezi tena adhabu ya kifo kwa wale waliohukumiwa kifo. Kwa mujibu wa takwimu kutoka Amnesty International na Shirika la Cornell Center on the Death Penalty Worldwide, kati ya Nchi 55 Wanachama wa Umoja wa Afrika ("Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika"), nchi 24 zimeondoa adhabu ya kifo kisheria kwa mujibu wa sheria za nchi yao;³ nchi 23 zinakomesha adhabu ya kifo kivitendo, baada ya kuchagua kutotekeleza adhabu yoyote ya kifo kwa angalau miaka 10 (na katika hali nyingi kubadilisha hukumu ya kifo kuwa vifungo vya kawaida);⁴ moja, Nigeria, imebaki miaka miwili tu kabla ya kuchukuliwa kuwa nchi inayokomesha adhabu ya kifo *kivitendo*, baada ya kutekeleza adhabu yake ya kifo mara ya mwisho mnamo mwaka 2016;⁵ na mbili zimeondoa adhabu ya kifo kwa makosa ya kawaida ya uhalifu wa sheria.⁶ Nchi nne tu Wanachama wa Umoja wa Afrika: Misri, Somalia, Sudan Kusini na Botswana ndizo zimetekeleza hukumu ya kifo tangu 2021;⁷ nchi mbili tu,

Liberia, Malawi, na Kenya. Angalia Ben Farmer na Peta Thornycroft, Will Africa Be The Next Continent to Abolish the Death Penalty?, TELEGRAPH (Apr. 16, 2024), <https://www.telegraph.co.uk/global-health/terror-and-security/death-penalty-abolishment-africa-capital-punishment/>. Hata hivyo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, iliondoa amri yake ya kusitisha adhabu ya kifo, iliyokuwa imedumu kwa zaidi ya miongo miwili, Machi mwaka huu, ingawa haionekani kuwa ilitekeleza adhabu yoyote ya kifo tangu wakati huo, kwa hivyo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inabaki kuainishwa kuwa ni nchi inayokomesha adhabu ya kifo kivitendo. Angalia Yassin Kombi na Sonia Rolley, Congo lifts moratorium on death penalty, justice ministry circular shows, REUTERS (Machi. 15, 2024), <https://www.reuters.com/world/africa/congo-lifts-moratorium-death-penalty-justice-ministry-circular-shows-2024-03-15/>.

³ Angalia Kiambatisho C. Angalia pia Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 41 (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024). Amnesty International inataja Nchi 23 Wanachama wa Umoja wa Afrika kuwa zimekomesha adhabu ya kifo kisheria, lakini orodha hiyo haijumuishi Zambia, ambayo ilikomesha adhabu ya kifo mwaka 2022 na 2023 kama ilivyoelezwa hapo juu (angalia supra n.2), zilikomesha adhabu ya kifo mwaka 2022 na 2023.

⁴Angalia Kiambatisho C. Angalia pia tovuti ya Cornell Center on the Death Penalty Worldwide, SHULE YA SHERIA YA CORNELL, <https://deathpenaltyworldwide.org/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024). Shirika la Cornell Center on the Death Penalty Worldwide linachukulia Nchi 22 Wanachama wa Umoja wa Afrika kuwa zinakomesha adhabu ya kifo kivitendo, taarifa hii inaweza kupatikana ama kwa kuvinjari ramani iliyo kwenye tovuti ya shirika hilo au kwa kutafuta za nchi husika katika kanzidata ya shirika hilo. Jumla ya Nchi 23 Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zinakomesha adhabu ya kifo kivitendo inafikiwa kwa kuchukuliwa Moroko na Sahara Magharibi kuwa nchi tofua.

⁵Angalia Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (Nigeria), CORNELL CENTER ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=53> (last visited Aug. 1, 2024) (ikitaja mara ya mwisho Nigeria kutekeleza adhabu ya kifo ilikuwa mwaka 2016).

⁶Angalia Kiambatisho C.

⁷Angalia Death Sentences and Executions in 2021, AMNESTY INT'L, 40, 51–52, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (imefunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024) (ikibainisha Misri, Somalia, Sudani Kusini, na Botswana kuwa nchi pekee Wanachama wa Umoja wa Afrika zilizotekeleza adhabu ya kifo mwaka 2021); Death Sentences and Executions in 2022, AMNESTY INT'L, 28, 33–34, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/6548/2023/en/> (imefunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024) (ikibainisha Misri, Somalia, na Sudani Kusini kuwa nchi pekee Wanachama wa Umoja wa Afrika zilizotekeleza adhabu ya kifo mwaka 2022).

Misri na Somalia, ndizo zilitekeleza dhabu ya kifo mwaka 2023;⁸ na, kulingana na taarifa zinazopatikana kwa sasa, ni Somalia pekee ndiyo ilitekeleza adhabu ya kifo mwaka 2024.⁹

5. Nje ya Afrika, nchi nyingi pia zimekataa adhabu ya kifo. Nchi 166 zimekomesha adhabu ya kifo kisheria, kivitendo, au kwa mkosa mengi ya uhalifu.¹⁰ Kati ya hizi, nchi 113 zimeondoa adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria,¹¹ 45 zinachukuliwa kuwa zinazokomesha adhabu ya kifo kivitendo,¹² na 8 zimekomesha adhabu ya kifo kwa makosa ya uhalifu wa kawaida.¹³ Ni idadi ndogo tu ya nchi zinazoendelea kutoa adhabu ya kifo; na kati ya hizo, nchi kadhaa bado zinaendelea kutekeleza adhabu ya kifo.¹⁴ Kwa mfano, mwaka 2022, mbali na China (ambayo haitoi takwimu

⁸Angalia Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 29, 35–36 (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024).

⁹Angalia Somalia: Somali Military Court Executes Three Men for Murder of Two Brothers, SHABELLE MEDIA NETWORK (MOGADISHU) (Juni 6, 2024), <https://allafrica.com/stories/202406070063.html#:~:text=Somalia%3A%20Somali%20Military%20Court%20Execut>.

¹⁰Jumla ya nchi 166 inapatikana kwa kujumlisha jumla ya idadi ya nchi ambazo zimekomesha adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria, jumla ya nchi ambazo zinachukuliwa kuwa zinazokomesha adhabu ya kifo kivitendo, na jumla ya idadi ya nchi ambazo zimekomesha adhabu ya kifo kwenye makosa ya uhalifu wa kawaida, kama ilivyoainishwa katika hukumu ifuatayo.

¹¹Angalia Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, 41 <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/7952/2024/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024). Amnesty International inataja nchi 112 kuwa zimekomesha adhabu ya kifo kisheria, lakini orodha hiyo haijumuishi Zambia, ambayo ilikomesha adhabu ya kifo mwaka 2022 na 2023 kama ilivyoielezwa hapo juu (angalia supra n.2).

¹²Angalia Kanzidata: 2.1. Abolitionist de facto, CORNELL CENTER ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, <https://deathpenaltyworldwide.org/database> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 2, 2024). Shirika la Cornell Center on the Death Penalty Worldwide linachukulia Nchi 44 ulimwenguni kote kuwa zinakomesha adhabu ya kifo kivitendo, taarifa hii inaweza kupatikana ama kwa kuvinjari ramani iliyo kwenye tovuti ya shirika hilo au kwa kuchuja kanzidata ya shirika hilo ili kuona nchi zinazokomesha adhabu ya kifo kivitendo. Hata hivyo, shirika la Cornell Center on the Death Penalty Worldwide linajumuisha Moroko na Sahara Magharibi kwa nchi moja, na idadi ya jumla ya nchi 45 zinazokomesha adhabu ya kifo kivitendo inapatikana kwa kuichukulia Moroko na Sahara Magharibi kuwa nchi mbili tofauti.

¹³ Angalia Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, at 41–42, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/7952/2024/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Julai 14, 2024). Amnesty International inataja nchi 9 kuwa zimekomesha adhabu ya kifo kwa makosa ya uhalifu wa kawaida, lakini inaonekana imeiainisha Zambia kimakosa katika kundi hili, kama ilivyoielezwa hapo juu (angalia supra n.2), Zambia ilikomesha adhabu ya kifo mwaka 2022 na 2023, na kubaki nchi 8 tu ambazo zimekomesha adhabu ya kifo kwa makosa ya uhalifu wa kawaida tu.

¹⁴Angalia Matthew Robinson & Lauren Moody, Capital Punishment, International Law, and Human Rights, 14 INT'L J. CRIM. JUST. SCIS., 298, 301 (2019). Angalia pia John D. Bessler, The Death Penalty, From Draconian Legal Codes to the Enlightenment, in THE DEATH PENALTY'S DENIAL OF FUNDAMENTAL HUMAN RIGHTS: INTERNATIONAL LAW, STATE PRACTICE, AND THE EMERGING ABOLITIONIST NORM, 1 (Cambridge Univ. Press 2022) (inazungumzia mitazamo inayobadilika kuhusu adhabu ya kifo na kupungua kwa idadi ya matukio ya unyongaji baada ya muda).

lakini inachukuliwa kuwa nchi inayotekeleza adhabu ya kifo kwa kiwango kikubwa duniani), nchi tatu zilitekeleza zaidi ya asilimia 90 ya unyongaji wote unaojulikana: Irani, Saudi Arabia na Misri.¹⁵ Kwa kuzingatia ukweli huu na mienendo hii, kama wasomi walivyoona, "ukomeshaji ni . . . hali ya kawaida ulimwenguni."¹⁶

6. Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Mahakama ya Afrika" au "Mahakama") imetambua mwelekeo wa kiulimwengu wa kukomesha adhabu ya kifo. Katika uamuzi wake wa mwaka 2022 katika kesi ya Ghati Mwita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mfano, Mahakama "ilitambua mwenendo wa kiulimwengu wa kukomesha adhabu ya kifo," hasa barani Afrika.¹⁷ Hasa kuhusiana na Afrika, Mahakama "ilitambua maendeleo ya bara zima kuhusiana na adhabu ya kifo."¹⁸ Mahakama iliona "Mwaka 1990, nchi moja tu, Cape Verde, ndiyo ilikuwa imeondoa adhabu ya kifo. Leo, kati ya nchi hamsini na tano (55) wanachama wa Umoja wa Afrika, ishirini na tano (25) zimekomesha adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria, kumi na tano (15) zimesitisha utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa muda mrefu huku kumi na tano (15) zikidumisha adhabu ya kifo. Hivi karibuni zaidi mwaka 2020, Chad ilikomesha adhabu ya kifo, ikifuatiwa na Sierra Leone mwaka 2021 na Jamhuri ya Afrika ya Kati na Guinea ya Ikweta [kwa makosa ya uhalifu wa kawaida] mwaka 2022."¹⁹ Kama ilivyoielezwa, ukweli kuhusu adhabu za kunyongwa huimarisha mwenendo huu, huku nchi nne tu Wanachama wa Afrika zikitekeleza adhabu za kunyonga tangu mwaka 2021; ni nchi mbili tu Wanachama wa Umoja wa Afrika zilizotekeleza adhabu ya kunyinga

¹⁵Angalia Death Penalty 2022: Recorded Executions Skyrocket to Highest Figure in Five Years, AMNESTY INT'L (Mei 16, 2023), <https://www.amnesty.org/en/latest/news/2023/05/death-penalty-2022-executions-skyrocket/> (ikisema kwamba, ukiondoa China, zaidi ya asilimia 90 ya mauaji yote yaliyoripotiwa yalifanywa na Iran, Saudi Arabia, na Misri). Ingawa haiwezekani kupata idadi thabiti ya unyongaji unaofanywa nchini China kwa sababu China inachukulia habari kama hiyo kuwa siri ya serikali, China ilikadiriwa kunyonga zaidi ya watu 1,000 mwaka 2022, kuliko nchi nyingine yoyote. Executions Around the World (2023), DEATH PENALTY INFORMATION CENTER, <https://deathpenaltyinfo.org/policy-issues/international/executions-around-the-world/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024).

¹⁶Robinson na Moody, supra n.14 ukurasa wa 300.

¹⁷Angalia Ghati Mwita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 012/2019, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 64 (Des. 1, 2022).

¹⁸Id. ¶ 65.

¹⁹19 Id. ¶ 65.

mwaka jana; na ni moja tu inayoendelea kutekeleza adhabu ya kunyonga hadi sasa mwaka huu..

7. Mnamo mwaka 2019, Jaji Tchikaya alitoa maoni tofauti katika kesi ya Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo aliona kwamba misingi ya sheria za Kiafrika na kimataifa imebadilika na kuunga mkono ukomeshaji kabisa na, kwa kuzingatia idadi inayoongezeka ya mataifa ya Kiafrika yenye ukomeshaji kamili au yanayokomesha adhabu ya kifo kivitendo, pia vyanzo mbalimbali vya kimataifa, alitoa wito kwa Mahakama hii kuona kwamba Kifungu cha 4 cha Mkataba wa Afrika kinakataza adhabu ya kifo katika aina zote.²⁰
8. Pamoja na mwenendo unaoongezeka wa kukomesha adhabu ya kifo, kama ilivyojadiliwa kwa undani zaidi katika sehemu iliyosalia ya wasilisho hili, utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo bila shaka husababisha ukiukaji wa ulinzi wa msingi unaotolewa na Mkataba; na kwa uhalisia barani Afrika (kama ilivyo katika maeneo mengine), utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo unakabiliwa na matatizo mengi, yakionyesha kwamba hukumu ya kifo haiwezi kutolewa na kutekelezwa bila kukiuka haki zilizowekwa katika Kifungu cha 4 na Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika.²¹ Sababu hizi zote, moja moja na kwa jumla, zinaunga mkono uamuzi kwamba adhabu ya kifo haiafikiani kabisa na Mkataba wa Afrika na kanuni za msingi za haki za binadamu.

4. Masuala ya Kisheria

9. 9. PALU kwa heshima inaona kwamba utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo unakiuka Kifungu cha 4 na Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika na

²⁰Angalia kwa ujumla Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.] (Novemba 28, 2019) (maoni tofauti yaliyotolewa na Jaji Blaise Tchikaya).

²¹Tunatambua ukweli kwamba Mahakama haisuluhishi migogoro masuala ya hoja za ukweli wakati wa kesi za ushauri. Ombi la Maoni ya Ushauri linalotolewa na Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU) kuhusu Kuafikiana kwa Sheria za Uzururaji na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Vyombo vingine vya Haki za Binadamu vinavyotumika barani Afrika, Na. 001/2018, Hukumu, Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 36 (Des. 4, 2020). Mifano yoyote ya mambo ya kweli iliyojadiliwa hapa imekusudiwa tu kuionyesha Mahakama viwango halisi vya utoaji wa adhabu ya kifo barani Afrika na kuonyesha jinsi ambavyo haiwezi kutolewa kwa njia ambayo haikiuki Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba wa Afrika.

kwa hivyo, Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na taratibu zote zinazoruhusu adhabu ya kifo.

10. Kwa hivyo PALU inawasilisha kwa heshima kwenye Mahakama hii Tukufu masuala yafuatayo kwa njia ya maoni ya ushauri ili yafanyiwe uamuzi:

a. Endapo sheria na/au taratibu za nchi za Afrika zinazoruhusu utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo zinakiuka:

i. Kifungu cha 4 cha Mkataba wa Afrika, ikiwa ni pamoja na agizo lake "haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa" na marufuku yake dhidi ya kuondoa uhai kiholela; na

ii. Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika, ikiwa ni pamoja na ulinzi wake wa "haki ya utu ambayo ni ya asili kwa mwanadamu na [] kutambua hadhi yake ya kisheria" na marufuku yake ya "aina za unyonyaji na udhalilishaji kwa mwanadamu, hasa utumwa, biashara ya utumwa, mateso, ukatili, adhabu na kutendewa kinyama au kwa kudhalilishwa."

b. Endapo, sheria na/au taratibu hizo zinakiuka Mkataba wa Afrika, Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu hizo.

11. Kama ilivyojadiliwa katika sehemu iliyosalia ya wasilisho hili, Mahakama hii inapaswa kujibu kila moja ya maswali haya kwa kuunga mkono kwa sababu zifuatazo.

12. Kwanza, Kifungu cha 4 kinaonyesha utambuzi wa msingi wa thamani ya kipekee ya wanadamu: "Haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa. Kila mwanadamu atakuwa na haki ya kuheshimiwa uhai wake na uadilifu wa utu wake. Hakuna mtu anayeweza kunyimwa haki hii kiholela." Tangazo na hakikisho la Mkataba kwamba "haki ya binadamu ya kuishi

haiwezi kuvunjwa" haliwezi kuafikiana na mauaji ya makusudi ya mwanadamu yanayofanywa na Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika.

13. Kutumia Kifungu cha 4 kuzuia adhabu ya kifo kwa masharti yake ya wazi kunaungwa mkono zaidi na mwenendo uliopo, miongoni mwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na mataifa mengine ulimwenguni, wa kuachana na adhabu ya kifo kama njia halali ya adhabu ya jinai, matamko na maazimio ya Tume ya Afrika, mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu, na vifungu husika vya mikataba na itifaki za kimataifa (ikiwa ni pamoja na zile zilizoridhiwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika), ambazo zote zinaunga mkono kukomesha kabisa adhabu ya kifo.²²
14. *Pili*, hata kama Kifungu cha 4 kingefasiriwa kulinda tu uondoaji wa uhai wa binadamu kiholela, utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa kwa uhalisia ungekiuka haki hiyo. Kiwango cha ulinzi dhidi ya utoaji wa adhabu ya kifo kiholela lazima kiendane na kiwango cha adhabu inayotolewa. Kwa sababu kuondoa maisha ya mwanadamu ni adhabu ya kiwango cha juu kabisa, zaidi ya aina nyingine yoyote inayoruhusiwa ya adhabu ya jinai, mfumo wa haki ya jinai haupaswi kuruhusiwa kutoa adhabu hiyo isipokuwa iwe inaweza kutoa kiwango cha usawa, uthabiti na isiwe ya kikatili.²³ Lakini mifumo ya haki ya jinai barani Afrika (na ulimwenguni kote) haifikii na haiwezi kufikia kiwango hicho; badala yake, ina alama ya mapungufu ya ndani na yanayoonekana kila mahali.

²²Angalia infra Sehemu ya 4(A).

²³Angalia, kwa mfano, Hilaire, Angalia, kwa mfano, Hilaire, Constantine na Benyamini na Wengine dhidi ya Trinidad na Tobago, Uzingatiaji wa Sheria, Fidia, na Gharama, Hukumu, Inter-Am. Ct. H.R. (ser. C) Na. 94, ¶ 148 (Juni 21, 2002) ("Kwa kuzingatia hali mbaya sana na isiyoweza kurekebisha ya adhabu ya kifo, uzingatiaji wa mchakato unaostahili, pamoja na kifungu chake cha haki na dhamana, unakuwa muhimu zaidi wakati maisha ya binadamu yako hatarini."); Medellín, Ramírez Cardenas na Leal García dhidi ya Marekani, Kukubalika na kuhakikisha kwamba kuondolewa uhai ambako kunaweza kutokea kupitia matumizi ya adhabu ya kifo kunafuata kikamilifu matakwa ya vyombo vya haki za binadamu vya Bara la Amerika."); Chad Roger Goodman dhidi ya Bahamas, Uzingatiaji wa Sheria (Chapisho), Inter-Am. Comm'n H.R., Na. 78/07, Kesi na. 12.265, ¶ 34 (Oktoba 15, 2007) ("[Jarijio la uchunguzi wa hali ya juu] linahitaji hasa kuzingatia kikamilifu sheria na kanuni za mchakato unaofaa na uendeshaji kesi wa haki katika muktadha wa kesi za hukumu ya kifo. Tume hapo awali imesisitiza kwamba, kwa sababu ya asili yake isiyoweza kubatilishwa na isiyoweza kubadilishwa, adhabu ya kifo... inalazimisha kuwe na mchakato wa kuaminika katika kuamua ikiwa mtu anawajibika kwa uhalifu ambao adhabu yake ni kifo.").

15. Kwa mfano, kama ilivyoonyeshwa hapa chini, Nchi zote nne Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zilitekeleza adhabu ya kifo kwa vifo vilivyorekodiwa kuanzia mwaka 2021 hadi sasa, Misri, Somalia, Sudan Kusini, na Botswana²⁴, zimeonesha dosari za mchakato zinazoonekana katika mifumo yao ya haki ya jinai.²⁵ Vivyo hivyo kwa nchi nyingine Wanachama wa Afrika ambazo zinaendelea kutoa adhabu ya kifo huku zikiepuka kutekeleza adhabu ya kifo. Moja wapo ya matatizo yaliyoenea na yanayosumbua sana ya mchakato stahiki, kwa mfano, ni kushindwa kutoa uwakilishi wa kutosha wa kisheria kwa wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo.
16. Aidha, adhabu ya kifo hutolewa kwa njia isiyo ya haki na ya kibaguzi kwa sababu ya mambo kama vile jinsia, umri, ulemavu wa akili, umaskini, vikwazo vya lugha na mtazamo wa kisiasa. Kwa kuzingatia athari za kasoro na mapungufu haya, adhabu ya kifo haiwezi kutolewa bila kukiuka ulinzi dhidi ukatili ambao Kifungu cha 4 kinaamuru.²⁶
17. *Tatu*, adhabu ya kifo inakiuka ulinzi uliohakikishwa na Kifungu cha 5 cha Mkataba. Kifungu cha 5 kinasema: "Kila mtu atakuwa na haki ya kuheshimiwa utu wake ambao ni kiini cha mwanadamu na kutambuliwa kwa hadhi yake ya kisheria. Aina zote za unyonyaji na udhalilishaji wa mwanadamu, hasa utumwa, biashara ya watumwa, mateso, ukatili, adhabu au kutendewa kinyama au kwa kudhalilisha ni marufuku." Utoaji na utekelezaji wa hukumu ya kifo kimsingi kunajumuisha athari na mwenendo unaokiuka Kifungu cha 5 kwa sababu ni (i) adhabu ya kikatili,

²⁴Misri ilinyonga watu 83 mwaka 2021, watu 24 mwaka 2022, na watu 8 mwaka 2023; Somalia ilinyonga watu 21 mwaka 2021, watu 6 mwaka 2022, na watu 38 mwaka 2023; Sudan Kusini ilinyonga watu 9 mwaka 2021, watu 5 mwaka 2022, na watu 0 mwaka 2023; na Botswana ilinyonga watu 3 mwaka 2021 na watu 0 mwaka 2022 na 2023. Angalia Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 29, 35–36

<https://www.amnesty.org/en/documents/act50/7952/2024/en/#:~:text=Amnesty%20International's%20monitoring%20of%20the,2022%20to%2016%20in%202023> (ilifunguliwa mara ya mwisho Juni 6, 2024); Death Sentences and Executions in 2022, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 28, 33–34, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/6548/2023/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Juni 6, 2024); Death Sentences and Executions in 2021, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 40, 51–52, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Juni 6, 2024). Angalia pia supra n.9 (ikibainisha Somalia kuwa nchi pekee ya Afrika ambayo inaonekana kutekeleza adhabu ya kifo hadi sasa mwaka huu).

²⁵Angalia infra Sehemu ya 4(B)(i).

²⁶Angalia infra Sehemu ya 4(B)(ii).

isiyo ya kibinadamu au ya kudhalilisha na kutendewa ("CIDPT") na/au (ii) mateso.

18. 18. Ukiukaji wa Kifungu cha 5 huanza wakati mtu anakabiliwa na mashtaka ambapo hukumu ya kifo inatolewa; na hakika hutokea mara tu mtu anapohukumiwa kifo kisha anafungwa gerezani akisubiri kunyongwa. Katika mazingira haya, mwanadamu anakabiliwa na mateso ya kisaikolojia ya kujua kwamba ipo siku Serikali itamuua. Mahakama hii, pamoja na mahakama nyingine na wasomi ulimwenguni kote, imekiri kwamba mateso haya ya kisaikolojia, yanayojulikana kama "Mateso ya Kisaikolojia ya Mtu anayesubiri Kunyongwa", yanaongezeka hadi kiwango cha CIDPT au mateso.²⁷
19. Kwa umahususi, Mahakama hii imekiri kwamba mahakama ya kimataifa imebaini kwamba "ucheleweshaji wa zaidi ya miaka mitatu (3) kati ya uthibitisho wa hukumu ya kifo ya mfungwa wakati wa rufaa na kutekeleza ukumu ya kifo ni adhabu au kitendo cha kikatili, kinyama au udhalilishaji" na kwa hivyo imeona ni ukiukaji wa Kifungu cha 5 wakati mshtakiwa amewekwa gerezani akisubiri kifo kwa miaka minane baada ya kuthibitishwa hukumu ya kifo wakati wa rufaa.²⁸ Kwa sababu watu walio chini ya hukumu ya kifo katika nchi za Afrika kwa kawaida wanakaa gerezani wakisubiri adhabu ya kifo kwa angalau miaka mitatu, na mara nyingi kwa muda mrefu zaidi, ukiukaji wa Kifungu cha 5 unaweza kuonekana kwa msingi huo. Lakini ukiukaji wa Kifungu cha 5 haupaswi kuwa tu kwa mazingira wakati mtu anafungwa gerezani kwa miaka mitatu au zaidi kufuatia uthibitisho wa hukumu kwenye rufaa. Mateso ya Kisaikolojia kwa Mtu anayesubiri Kunyingwa, mateso ya kisaikolojia ambayo mwanadamu anapitia anapokabiliwa na matarajio ya kuuawa na Serikali kwa kukusudia, ynaanza tangu wakati mtu anakabiliwa na matarajio ya hukumu ya kifo na yanadhihirika zaidi hukumu ya kifo inapotolewa. Kwa hivyo, Mahakama hii inapaswa kutambua ukiukaji wa Kifungu cha 5 kwa msingi huu kama kipengele kisichoepukika cha adhabu

²⁷Angalia infra Sehemu ya 4(C)(i)(1).

²⁸Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 157–158 (Juni 4, 2024).

ya kifo, bila kujali ni muda gani mtu anakuwa gerezani akisubiri kunyongwa. Aidha, hali mbaya zinazowakabili wanawake walio katika hukumu ya kifo na, wakati mwingine, watoto wao, pamoja na athari mbaya za kisaikolojia na kihisia wanazopata wanafamilia wa wale waliohukumiwa kifo, pia husababisha ukiukaji wa Kifungu cha 5.²⁹

20. Kitendo cha Serikali kutekeleza hukumu ya kifo, kimsingi kumwua mwanadamu, pia ni ukiukaji wa Kifungu cha 5. Tathmini yoyote ya kweli ingeonesha kwamba hakuna njia ya kumwua mwanadamu bila, kwa maneno ya Kifungu cha 5, kukiuka "heshima ya utu ya asili kwa mwanadamu" na bila kumweka adhabu au vitendo vya "mateso, ukatili, unyama au kudhalilisha."³⁰ Na kila moja ya njia za utekelezaji zinazotumiwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zinazoendelea na adhabu ya kifo zimeonekana kujumuisha CIDPT au mateso.³¹
21. Kwa ujumla, adhabu ya kifo haiwezi kutolewa au kutekelezwa bila kukiuka Kifungu cha 4 au 5 cha Mkataba wa Afrika. Wakati kila moja ya sababu zilizoainishwa hapo juu na kujadiliwa hapa chini inatoa msingi huru wa kubaini kwamba adhabu ya kifo ipo kinyume na Mkataba wa Afrika, athari ya jumla ya sababu hizi zote katika ujumla wake pia inaongoza kuwa na hitimisho kwamba adhabu ya kifo inakiuka Mkataba wa Afrika na kanuni za msingi za haki za binadamu.
22. Kwa hivyo, kwa kuwa adhabu ya kifo inakiuka Mkataba, kila Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika lazima ifute sheria na/au kanuni zozote ambazo zitaruhusu kuendelea kutolewa na kutekeleza adhabu ya kifo.

A. Adhabu ya kifo kwa asili inakiuka Kifungu cha 4.

23. Adhabu ya kifo ni ukiukaji kabisa wa Kifungu cha 4. Kifungu cha 4 kinasema kuwa, "Haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa. Kila

²⁹ Angalia infra Sehemu ya 4(C)(i)(2-3).

³⁰ Kifungu cha 5, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu. Angalia infra Sehemu ya 4(C)(ii).

³¹ Angalia infra Sehemu ya 4(C)(iii).

mwanadamu atakuwa na haki ya kuheshimiwa uhai wake na uadilifu wa utu wake. Hakuna mtu anayeweza kunyimwa haki hii kiholela." "Haipaswi kuvunjwa" inamaanisha "Haipaswi kukiukwa; hawajibiki au hatakiwi kufanyiwa vurugu; awekwe kwa uadilifu bila kuchafuliwa, ukiukaji au unyanyasaji." ³²Tangazo na hakikisho la Mkataba kwamba "haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa" haliwezi kuafikiana na mauaji ya makusudi ya mwanadamu yanayofanywa na Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika.³³

24. Matumizi haya ya Kifungu cha 4 kuzuia kuondoa uhai wa mwanadamu kupitia adhabu ya kifo yanaimarishwa na harakati za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na mataifa mengine ulimwenguni kuondokana na adhabu ya kifo kama njia halali ya adhabu kwa makosa ya jinai, pamoja na matamko na maazimio ya Tume ya Afrika, mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu, na vifungu husika vya mikataba na itifaki za kimataifa (ikiwa ni pamoja na zile zilizoridhiwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika), ambazo zote zinaunga mkono kukomesha kabisa adhabu ya kifo.
25. Sentensi ya pili na ya tatu ya Kifungu cha 4 zinahusu kuheshimu uhai na uadilifu wa mtu na kupiga marufuku ukiukaji wa haki hii kiholela. Kuhusu sehemu hii ya Kifungu cha 4, Mahakama hii imetoa maoni ya ziada katika kesi ya Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ghati Mwita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kesi zingine ambazo sentensi hizi katika Kifungu cha 4 hazikatazi adhabu ya kifo katika hali zote lakini badala yake zinakataza tu kuondoa uhai kiholela.³⁴ Kwa mfano, katika kesi ya Rajabu, Mahakama hii ilisema kuwa

³² Inviolable, OXFORD ENGLISH DICTIONARY (Juni 2024), <https://doi.org/10.1093/OED/5825033183>.

³³Angalia Al-Saadoon na Mufdhi dhidi ya Uingereza, Na. 61498/08, Hukumu, Eur. Ct. H.R., ¶ 115 (Aprili 10, 2010) ("Utekelezaji wa adhabu ya kifo ulioamuliwa na mahakama unahusisha kuondoa kwa makusudi uhai wa mwanadamu unaofanywa na mamlaka ya Serikali."); Kifungu cha 4, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

³⁴Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 98 (Novemba 28, 2019). Angalia Ghati Mwita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 012/2019, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 66 (Desemba 1, 2022) ("Hata hivyo, kwa kuwa mazingira ambayo adhabu ya kifo inaweza kufaa hayawezi kuainishwa kwa usahihi, uamuzi wa matukio ya uhalifu unaoruhusu kutolewa kwa adhabu ya kifo lazima uachwe kwa mahakama za ndani

kuonekana kwa neno "kiholela" katika sentensi ya tatu ya Kifungu cha 4, "kunarejelea kuondoa [uhai] ilimradi kitendo hicho kinanywa kiholela. Kwa maana dokezi, hukumu ya kifo inaruhusiwa kama kighairi cha haki ya kuishi chini ya Kifungu cha 4 maadamu haitolewi kiholela."³⁵ Lakini suala la endpo Kifungu cha 4, pamoja na amri yake kwamba "Haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa", kinazuia kabisa adhabu ya kifo halikuwasilishwa mbele ya Mahakama katika kesi hizo: suala hili halijawasilishwa na Waleta Maombi, halikushughulikiwa na wahusika, wala halikuwa muhimu wala kipengele cha kuathiri uamuzi katika uamuzi wa Mahakama. Badala yake, kesi hizo zilishughulikiwa tu iwapo Tanzania kutoa adhabu ya kifo kwa lazima katika kesi zote za mauaji kulikuwa kinyume cha Kifungu cha 4, kwa msingi kwamba inatolewa kiholela, na Mahakama ilijibu swali hilo kwa uthibitisho.³⁶ Kwa hivyo, maoni ya Mahakama kuhusu tafsiri ya Kifungu cha 4, ambayo hayaendani na busara ya kisheria na maendeleo yaliyopo katika sheria ya kimataifa, hayapaswi kuzingatiwa kuwa uamuzi wa kisheria au wa kimamlaka na yanapaswa kupuuzwa. Kimsingi, kwa uelewa wetu, Mahakama hii haijawahi kukabiliwa na swali la moja kwa moja la iwapo adhabu ya kifo haiafikiani kwa asili na Kifungu cha 4.

26. PALU kwa heshima anawasilisha kwamba Mahakama inapaswa kushughulikia swala hili sasa na inapaswa kutoa busara faafu ya kisheria kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba wa Afrika kuhusu suala hili. Kwa kufanya hivyo, Mahakama inapaswa kuthibitisha kwamba Kifungu cha 4, ikiwa ni pamoja na agizo lake muhimu kwamba "Haki ya binadamu kuishi

kuamua kwa msingi wa kesi moja moja."). Angalia pia, kwa mfano, Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 202–203 (Septemba 3, 2024).

³⁵Angalia Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 98 (Novemba 28, 2019).

³⁶Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 14(vii-viii) (Novemba 28, 2019) (ikitoa ombi la mleta maombi kwamba Mahakama ione kwamba adhabu ya lazima ya kifo inakiuka Kifungu cha 4); id. ¶ 111–114 (ikiona kwamba adhabu ya lazima ya kifo inakiuka Kifungu cha 4); Ghati Mwita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 012/2019, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 80 (Desemba 1, 2022) (ileile); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 195, 207–208 (Septemba 3, 2024).

haiwezi kuvunjwa", hakiruhusu Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika kumuua mwanadamu kwa makusudi.

27. Usaidizi wa ziada kwa hitimisho kwamba kumuua mwanadamu kunakofanywa na Serikali kunakiuka Kifungu cha 4 unaweza kupatikana katika matamko ya Tume ya Afrika, maoni tofauti ya waheshimiwa majaji wa Mahakama hii, na katika harakati za kuondokana na adhabu ya kifo barani Afrika na ulimwenguni kote.
28. Tume imeshutumu adhabu ya kifo mara kwa mara na kutoa wito wa kuikomesha kwa kusihi sana katika kipindi cha miaka 25 iliyopita. Mnamo mwaka 1999, Tume ilipitisha Azimio la 42, ambalo lilitoa wito kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika "kupunguza utoaji wa adhabu ya kifo kwa makosa ya uhalifu makubwa zaidi pekee," "kufikiria kuweka marufuku ya kunyonga," na "kuangalia uwezekano wa kukomesha adhabu ya kifo."³⁷
29. Mnamo mwaka 2008, Tume ilipitisha Azimio la 136, ambalo lilitoa wito kwa Nchi Wanachama kuweka marufuku ya kunyonga "kwa lengo la kukomesha adhabu ya kifo" na kuridhia Itifaki ya Pili ya Hiari ("OP2") ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ("ICCPR"),³⁸ ambao unasema kwamba "hakuna mtu aliye ndani ya mamlaka ya Nchi Mwanachama wa Itifaki hii atakayenyongwa" na kwamba "kila Nchi Mwanachama itachukua hatua zote muhimu ili kukomesha adhabu ya kifo ndani ya mamlaka yake." ³⁹ Mwaka 2014, Tume iliandaa Mkutano wa Bara zima kuhusu Kukomesha Adhabu ya Kifo barani Afrika ("Mkutano wa Bara zima"), ambao ulipitisha Azimio la Bara zima Kukomesha Adhabu ya Kifo barani Afrika ("Azimio la Cotonou"). Azimio la Cotonou "linatoa wito kwa watunga sheria barani Afrika wapitie sheria zao za kitaifa na watunge

³⁷Kuhimiza Serikali Kutekeleza Marufuku ya Adhabu ya Kifo, ACHPR/Res.42 (XXVI)99, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.] (Nov. 15, 1999).

³⁸Azimio la Kutoa Wito kwa Nchi Wanachama kuzingatia Marufuku ya Adhabu ya Kifo, ACHPR/Res.136 (XXXIV)08, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.] (Nov. 24, 2008).

³⁹G.A. Res. 44/128, Itifaki ya Pili ya Hiari ya Makubaliano ya Kimataifa ya Haki za Kiraia na Kisiasa, kwa lengo la kukomesha adhabu ya kifo, MMKUSANYO WA MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA, kifungu cha 1(1) (Desemba 15, 1989), [https://treaties.un.org/doc/source/docs/A RES 44 128-E.pdf](https://treaties.un.org/doc/source/docs/A%20RES%2044%20128-E.pdf).

sheria ya kukomesha adhabu ya kifo" na kuzisihi Nchi Wanachama wa Umoja kuridhia OP2 ya ICCPR.⁴⁰

30. Mnamo mwaka 2015, Tume ilipitisha Maoni ya Jumla Na. 3 kuhusu Mkataba wa Afrika kuhusu haki ya kuishi kulingana na Kifungu cha 4. Katika sehemu husika, Maoni ya Jumla Na. 3 yanasema kwamba:

"Tume mara kadhaa imepitisha maazimio yanayotoa wito kwa Mataifa kukomesha adhabu ya kifo, au kuweka marufuku kulingana na mwenendo unaoendelea barani na ulimwenguni. Idadi kubwa ya Nchi za Afrika sasa zimefuta adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria au kivitendo. **Sheria ya kimataifa inahitaji Mataifa ambayo bado hayajafuta adhabu ya kifo yachukue hatua za kuikomesha ili kutovunja haki za kuishi na utu**, pamoja na haki nyingine kama vile haki ya kuwa huru dhidi ya vitendo vya mateso, ukatili, unyama au udhalilishaji."⁴¹

31. Tume imesisitiza kanuni na misimamo hii katika busara yake ya kisheria. Katika Mawasiliano ya mwaka 2015 *Interights na Ditshwanelo dhidi ya Jamhuri ya Botswana*, Tume ya Afrika ilipendekeza kwa msisitizo kwamba adhabu ya kifo haiwezi tena kuendelea kuafikiana na Mkataba wa Afrika:

"Kutokana na 'mageuzi ya sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na busara za kisheria na desturi ya Serikali na kwa kutambua kazi inayoendelea kufanywa na Kikundi Kazi cha Tume ya Adhabu ya Kifo, Mauaji Nje ya Mfumo wa Sheria, Mauaji ya Kiholela, Tume inaona kuwa inazidi kuwa vigumu kufikiria kesi ambayo adhabu ya kifo inaweza kuonekana kuwa imetumika kwa njia isiyo ya kiholela. Kwa sababu hiyo ni vigumu kufikiria kwamba, ikiwa itaitwa katika siku

⁴⁰Azimio la Mkutano wa Bara zima kuhusu Kukomesha Adhabu ya Kifo [hapa linarejelewa kama "Azimio la Cotonou"], Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.] (Julai 4, 2014), <https://achpr.au.int/index.php/en/news/statements/2014-07-08/declaration-continental-conference-abolition-death-penalty>.

⁴¹Maoni ya Jumla Na. 3 Kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu: Haki ya Kuishi (Kifungu cha 4), Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], § D.22 (Desemba 12, 2015), <https://www.refworld.org/legal/general/achpr/2015/en/70896> (msisitizo umeongezwa).

zijazo kufanya hivyo, kwamba Tume itaona kuwa adhabu ya kifo, ikitekelezwa kwa jinsi yoyote, haitakuwa inaafikiana tena na Mkataba wa Afrika.”⁴²

32. 32. Kwa mantiki hiyo hiyo, Kamishna Zainabou Sylvie Kayitesi katika ripoti yake kwenye kikao cha 499 cha Tume ya Afrika, alisema kama ifuatavyo: "Adhabu ya kifo ni ya kikatili na kwa hivyo si ya kimaadili, isiyo ya lazima, isiyoweza kurekebisha, isiyo ya kimantiki; na inawakilisha ukiukaji mkubwa zaidi wa haki za msingi za binadamu hasa haki ya kuishi chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba wa Afrika.”⁴³
33. Aidha, waheshimiwa majaji wa Mahakama hii wametoa wito kwa Mahakama kuona kwamba adhabu ya kifo katika hali zote ni kinyume cha Kifungu cha 4. Jaji Tchikaya, kwenye maoni yake tofauti katika kesi ya Ally Rajabu na wengine dhidi ya Tanzania, aliona kwamba kusoma Kifungu cha 4 kuhitaji Nchi Wanachama waondoe kabisa adhabu ya kifo kutaonesha mwenendo wa nchi za Afrika kuweka "marufuku ya utekelezaji wa adhabu ya kifo.”⁴⁴ Zaidi ya hayo, Jaji Tchikaya aliihimiza Mahakama hii isione haya kutumia mamlaka yake ya kutafsiri ili kuhitimisha kwamba rejea ya Kifungu cha 4 kuhusu haki ya kuishi ni kamili, na kinapaswa kutafsiriwa kuwa kinakataza adhabu ya kifo.⁴⁵ Alielezea zaidi kwamba njia hii imetumiwa na mahakama na Mataifa mengine wakati wa kutafsiri Kifungu cha 4 na wakati wa kushughulikia vifungu kama hivyo vilivyomo katika vyombo vingine. ⁴⁶ Jaji Tchikaya alihitimisha kwamba, kulingana na mwenendo wa kimataifa (na wa Kiafrika) wa kukomesha adhabu ya kifo, Kifungu cha 4 kinapaswa kutafsiriwa kuwa kinakataza adhabu ya kifo.⁴⁷

⁴²Interights na Ditshwanelo dhidi ya Jamhuri ya Botswana, Mawasiliano 319/06, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], ¶ 66 (Novemba 18, 2015) (msisitizo umeongezwa).

⁴³Kikundi Kazi cha Adhabu ya Kifo, Mauaji nje ya Mifumo ya Sheria, Mauaji ya Kiholela na Utekeji Unaofanywa na Serikali barani Afrika-49OS, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.] (Apr. 28, 2011), <https://achpr.au.int/index.php/sw/node/1553>.

⁴⁴Angalia Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], ¶¶ 18–19 (Novemba 18, 2019) (maoni tofauti yaliyotolewa na Jaji Blaise Tchikaya).

⁴⁵ Angalia id. ¶ 21.

⁴⁶ Angalia id. ¶¶ 22–25.

⁴⁷ Angalia id. ¶ 28.

34. Katika maoni yake ya kupinga katika kesi ya Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jaji Tchikaya alisisitiza kwamba Kifungu cha 4 "kinafanya maisha ya binadamu yasiweze kuharibiwa katika muundo na taratibu zake zote" na kwamba "Mahakama inapaswa kubatilisha kwa udhahiri dhabu ya kifo ili kulinda haki ya kuishi" kama inavyotakiwa na matumizi ya sheria ya kimataifa na " maandishi ya kimataifa yanayokomesha adhabu ya kifo."⁴⁸ Jaji Tchikaya alionyesha maendeleo yanayofanyika Ulaya, ambapo, kwa sababu ya "chombo cha sheria ya kimataifa ya haki za binadamu", Ulaya "imekuwa eneo lisilo na adhabu ya kifo".⁴⁹ Kanuni majumui za sheria ya haki za binadamu zinapaswa kuhitaji kwamba adhabu ya kifo ipigwe marufuku barani Afrika pia. Aidha, katika tamko lake kwenye kesi ya Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jaji Tchikaya alisisitiza kwamba "hukumu yoyote ya kifo ni hukumu ya kifo, iwe ni ya lazima au la. Ni adhabu hii isiyofaa ambayo lazima ikataliwe na kuondolewa kwenye kwa utaratibu wa kijamii. Mahakama inaweza kusaidia Mataifa ambayo yapo taratibu kufanikisha hili."⁵⁰ Aliendelea kusema kwamba "Mahakama ilipaswa kuhitimisha zamani kwamba hakuna tena nafasi yoyote ya kuipa uhalali adhabu ya kifo kwa njia yoyote ile."⁵¹
35. Vivyo hivyo, Jaji Ntsebeza alitoa tamko katika kesi ya Zabron na Augustino, akisema kwamba "adhabu ya kifo ina uwezekano wa kuwa na makosa, huku matokeo yake hayawezi kubadilishwa. Aidha, haina athari ya kuzuia inayoonekana, na matumizi yake ya kibaguzi yanadhoofisha kanuni za msingi za utu wa binadamu, haki, na usawa."⁵² Wakati maoni

⁴⁸Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 35, 38, 39 (Juni 4, 2024) (maoni ya kupinga ya Jaji Blaise Tchikaya).

⁴⁹ Id. ¶ 38.

⁵⁰Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 8 (Septemba 3, 2024) (azimio la Jaji Blaise Tchikaya).

⁵¹ Id. ¶ 11.

⁵²Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 2 (Juni 4, 2024) (tamko la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa

ya Jaji Ntsebeza yalitolewa kuunga mkono tamko kwamba adhabu ya kifo “yenyewe, inakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba,” maoni hayo hayo pia yanaunga mkono ugunduzi kwamba adhabu ya kifo yenyewe inakiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba.⁵³

36. Wasomi na wataalamu wa kimataifa pia wanatafsiri ulinzi wa Kifungu cha 4 kuhusu haki ya mtu ya kuishi kuwa kamili.⁵⁴ Kulingana na wasomi na wataalamu hawa, haki kamili ya kuishi inamaanisha kuwa marufuku kamili ya adhabu ya kifo.⁵⁵
37. Tena zaidi, hitimisho kwamba adhabu ya kifo ni kinyume na ulinzi wa maisha kama kanuni ya msingi ya haki za binadamu, kama ilivyo katika Kifungu cha 4, inaimarishwa na mwenendo unaoendelea, kimataifa na barani Afrika, katika kuelekea kukomesha adhabu ya kifo. Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, idadi kubwa ya nchi kote ulimwenguni, na barani Afrika, zimefuta adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria au kivitendo.⁵⁶ Zaidi ya hayo, vyombo vingi vya kimataifa vinaunga mkono marufuku ya adhabu ya kifo, na vyombo hivi vimeridhiwa rasmi na kutumiwa kwa upana ndani ya Afrika na ulimwenguni kote. Kwa mfano, kati ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zimekomesha rasmi adhabu ya kifo, nchi 15 zimeidhinisha OP2 ya ICCPR.⁵⁷

Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 2 (Septemba 3, 2024) (azimio la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza).

⁵³Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 1 (Juni 4, 2024) (tamko la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 1 (Septemba 3, 2024) (azimio la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza).

⁵⁴Angalia, kwa mfano, Mwongozo wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, Amnesty Int'l, <https://www.amnesty.org/en/wp-content/uploads/2021/08/ior630052006en.pdf> (ulifunguliwa mara ya mwisho Aprili 24, 2024) (“hakuna mtu anayepaswa kuhukumiwa kifo au kunyongwa, hata wafungwa ambao wamekutwa na hatia baada ya kusikilizwa kwa haki na kukuta wamefanya uhalifu wa kutisha.”).

⁵⁵Angalia, kwa mfano, Andrew Novak, Hanging and the Mandatory Death Penalty in Africa: the Significance of Rajabu dhidi ya Tanzania, 5 AFR. HUM. RTS. Y.B., 401, 409 (2021).

⁵⁶Angalia supra ¶¶ 4–5.

⁵⁷ Ratification Status for the Second Optional Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights, aiming at the abolition of the death penalty, U.N. TREATY COLLECTION, 414 (Julai 11, 1991), https://treaties.un.org/Pages/ViewDetails.aspx?src=TREATY&mtdsg_no=IV-12&chapter=4&clang=_en (inaorodhesha nchi ambazo zimeidhinisha OP2).

38. Hata Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo hazijatia saini OP2, au mikataba mingine ya kimataifa iliyojadiliwa hapa, zinaweza kuwa chini ya kanuni za msingi zilizojumuishwa katika vyombo hivi, kwani Mahakama hii imetamka kuwa "Nchi Wanachama[] wote wa Umoja wa Afrika zimejitolea 'kuimarisha na kulinda haki za binadamu na watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na vyombo vingine muhimu vya haki za binadamu'" na kwamba "kwa kijizatiti kwa njia hii, Nchi Wanachama zimechukua jukumu la kudumisha haki za binadamu kwa kuwaheshimu watu wote walio ndani ya mamlaka yao."⁵⁸ Ulimwenguni kote, nchi 91 zimeidhinisha OP2.⁵⁹
39. Aidha, mashirika ya haki za binadamu ya kikanda ya Ulaya na Amerika ya Kusini pia yamepitisha itifaki kadhaa zinazolenga kuzuia adhabu ya kifo. Kwa kuanza, itifaki za mkataba wa Ulaya zinazokomesha adhabu ya kifo zinaungwa mkono karibu na wanachama wote wa Baraza la Ulaya. Kwa mfano, barani Ulaya, Itifaki Na. 6 ya Mkataba wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi, uliopitishwa mwaka 1982, unaeleza kwamba "adhabu ya kifo itakomeshwa. Hakuna mtu atakayehukumiwa adhabu ya namna hiyo au kunyongwa."⁶⁰ Maelezo haya yalithibitishwa tena mwaka 2002 kupitia Itifaki Na. 13 ya Mkataba huo huo.⁶¹ Itifaki Na. 6 imeridhiwa na wanachama wote 46 wa Baraza la Ulaya, na Itifaki Na. 13 imeridhiwa na wanachama 45 (na imesainiwa na mwanachama mmoja aliyesalia).⁶² Na barani Amerika ya Kusini, nchi 13 zimeridhia Itifaki ya

⁵⁸

Ombi la Maoni ya Ushauri linalotolewa na Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU) kuhusu Kuafikiana kwa Sheria za Uzururaji na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Vyombo vingine vya Haki za Binadamu vinavyotumika barani Afrika, Na. 001/2018, Hukumu, Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 35 (Des. 4, 2020).

⁵⁹ Ratification Status for the Second Optional Protocol to the International Covenant on Civil and Political Rights, aiming at the abolition of the death penalty, U.N. TREATY COLLECTION, (Julai 11, 1991), https://treaties.un.org/Pages/ViewDetails.aspx?src=TREATY&mtdsg_no=IV-12&chapter=4&clang=en.

⁶⁰ Itifaki Na. 6 ya Mkataba wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi Kuhusu Kukomesha Adhabu ya Kifo, W.K.S.Na. 114, kifungu cha 1 (1983).

⁶¹ Angalia Itifaki Na. 13 ya Mkataba wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi Kuhusu Kukomesha Adhabu ya Kifo katika Hali zote, W.K.S. Na. 187, kifungu cha 1 (2002).

⁶² Watia saini wa Itifaki Na. 6 ya Mkataba wa Ulaya wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi, DANISH INST. FOR HUM. RTS.,

Mkataba wa Amerika wa Haki za Binadamu wa Kukomesha Adhabu ya Kifo, uliopitishwa mwaka 1990, ambao unaeleza katika Kifungu cha 1 kwamba "Nchi Wanachama wa Itifaki hii hawatatumia adhabu ya kifo katika nchi yao kwa mtu yeyote aliye chini ya mamlaka yao."⁶³

40. Katika ngazi ya kimataifa, mwenendo wa kukomesha unaendelea kuimarika kila mwaka unapopita. Hata kama bado hakuna marufuku ya dhahiri ya adhabu ya kifo chini ya sheria ya kimataifa, jumuiya ya kimataifa imezidi kutoa matamko yanayopinga matumizi ya adhabu ya kifo yanayoendelea, ikipendekeza kuimarisha kanuni za kitamaduni. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka kumi na tano iliyopita, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa limepitisha mfululizo wa maazimio mwaka 2007, 2008, 2010, 2012, 2014, 2016, 2018, 2020, na 2022, likihimiza Mataifa kuheshimu viwango vya kimataifa vinavyolinda haki za watu wanaokabiliwa na adhabu ya kifo, na kuzuia hatua kwa hatua matumizi ya adhabu ya kifo na kupunguza idadi ya makosa ambayo yanaweza kuadhibiwa kwa adhabu ya kifo.⁶⁴ Mwaka 2022, nchi 126 za zilipiga kura kuunga mkono kupitisha azimio la kusitisha matumizi ya adhabu ya kifo, wakati nchi 37 tu ndizo zilizopiga kura kupinga azimio hilo.⁶⁵ Idadi ya nchi ambazo zimepiga kura kuunga mkono marufuku ya kimataifa kuhusu adhabu ya kifo imeongezeka kwa kasi tangu mwaka 2007. Ingawa

<https://sdg.humanrights.dk/instrument/signatories?i=44908> (imefunguliwa mara ya mwisho Juni 11, 2024); Chati ya saina na uridhaji wa Mkataba 187, BARAZA LA ULAYA, <https://www.coe.int/en/web/conventions/full-list?module=signatures-by-treaty&treatynum=187> (imefunguliwa mara ya mwisho Mei 7, 2024).

⁶³Nchi hizi ni Argentina, Brazili, Chile, Costa Rica, Jamhuri ya Dominika, Ecuador, Honduras, Mexico, Nicaragua, Panama, Paraguay, Uruguay na Venezuela. Signatories and Ratifications, A-53: Protocol to the American Convention on Human Rights to Abolish the Death Penalty, DEPARTMENT OF INTERNATIONAL LAW, <http://www.oas.org/juridico/english/sigs/a-53.html> (imefunguliwa mara ya mwisho Mei 7, 2024).

⁶⁴G.A. Res. 62/149, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/62/149 (Des. 18, 2007); G.A. Res. 63/168, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/63/168 (Des. 18, 2008); G.A. Res. 65/206, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/65/206 (Des. 21, 2010); G.A. Res. 67/176, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/67/176 (Des. 20, 2012); G.A. Res. 69/186, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/69/186 (Des. 18, 2014); G.A. Res. 71/187, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/71/187 (Des. 19, 2016); G.A. Res. 73/175, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/73/175 (Des. 17, 2018); G.A. Res. 75/183, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/75/183 (Des. 16, 2020); G.A. Res. 77/222, Marufuku ya matumizi ya adhabu ya kifo, A/RES/77/222 (Des. 15, 2022).

⁶⁵Kumbukumbu za Uoigaji Kura za Kamati ya Tatu, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (Nov. 11, 2022), https://www.un.org/en/ga/third/77/docs/voting_sheets/L.44.Rev.1.pdf. Zingatia kwamba nchi 24 hazikupiga kura. Id.

maazimio haya hayana mamlaka ya kisheria ya mkataba, yanaakisi na kuunga mkono mwenendo mkubwa wa kimataifa wa kuacha kutumia na kukomesha adhabu ya kifo kwa misingi ya haki za msingi za binadamu.

41. Kwa sababu zote zilizoainishwa hapa, PALU kwa heshima inawasilisha kwamba Mahakama inapaswa kuona kwamba adhabu ya kifo kwa asili inakiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba wa Afrika.

B. Utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa uhalisia ni kumwondolea mtu uhai kikatili kwa kukiuka Kifungu cha 4.

42. Vinginevyo, Mahakama inaweza na inapaswa kuona kwamba, hata kama Kifungu cha 4 kinatafsiriwa kuwa kinakataza tu kuondoa uhai wa binadamu kiholela, utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa uhalisia kwa kweli ni ukatili na kwa hivyo ni kinyume cha Kifungu cha 4 kwa msingi huu.
43. Kama Tume ya Afrika ilivyoelezea, "hali hii ya kiholela inapaswa kutafsiriwa kwa kuzingatia mambo kama vile kufaa, haki, kutabirika, ufaafu, ulazima na uwiano."⁶⁶ Tume ya Afrika imeona zaidi kwamba "inazidi kuwa vigumu kupata kesi ambayo adhabu ya kifo inaweza kuonekana kuwa imetumika kwa njia isiyo ya kiholela [na kwa sababu] ni vigumu kufikiria kwamba, ikiwa itaitwa katika siku zijazo kufanya hivyo, kwamba Tume itaona kuwa adhabu ya kifo, ikitekelezwa kwa jinsi yoyote, haitakuwa inaaifikiana tena na Mkataba wa Afrika."⁶⁷
44. Aidha, kama ambavyo pia Tume ya Afrika imeona, utoaji wa adhabu ya kifo kwa kukiuka viwango vya mchakato unaostahili vya Kifungu cha 7 cha

⁶⁶Angalia Maoni ya Jumla Na. 3 Kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu: Haki ya Kuishi (Kifungu cha 4), Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], ¶ 12 (Desemba 12, 2015), <https://www.refworld.org/legal/general/achpr/2015/en/70896>.

⁶⁷Interights na Ditshwanelo dhidi ya Jamhuri ya Botswana, Mawasiliano 319/06, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], ¶ 66 (Novemba 18, 2015).

Mkataba wa Afrika au kwa kukiuka ulinzi wa msingi wa Mkataba kama vile marufuku ya Kifungu cha 2 kuhusu ubaguzi, ni wa kiholela kabisa.⁶⁸

45. Mahakama hii pia inaona "uholela" kupitia kioo cha "mchakato unaostahili," ikigundua katika kesi kadhaa kwamba adhabu ya lazima ya kifo, ambayo hairuhusu kuzingatia sababu na mazingira ya kupunguza hatari na haiafikiani na mchakato unaostahili na kwa hivyo ni ya kiholela.⁶⁹ Katika kesi ya Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mfano, Mahakama hii iligundua kuwa "endapo kuondolewa uhai jambo la kiholela kwa maana ya Kifungu cha 4 cha Mkataba kunapaswa kutathminiwa kulingana na vigezo vitatu: kwanza, ni lazima iwe imetolewa na sheria; pili, ni lazima iwe imetolewa na mahakama yenye uwezo; na, tatu, ni lazima ifuate mchakato unaostahili."⁷⁰ Na katika kesi ya Marthine Christian Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama hii ilibaini kwamba ukiukaji wa "mchakato unaostahili" ni pamoja na ucheleweshaji wa muda mrefu kabla ya kesi kusikilizwa na uwakilishi hafifu.⁷¹ Kwa sababu hukumu ya kifo ni adhabu kali kupita zote, ulinzi huu dhidi ya uholela na uhakikisho wa mchakato unaostahili lazima uwe thabiti. Hata hivyo kama ilivyojadiliwa hapa, kasoro kubwa za mchakato na kasoro za kinfumo katika utoaji wa adhabu ya kifo kwa vitendo barani Afrika hufanya utekelezaji wake unaoendelea kuwa ukiukaji wa Kifungu cha 4.

⁶⁸Maoni ya Jumla Na. 3 Kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu: Haki ya Kuishi (Kifungu cha 4), Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], ¶¶ 11–12, 24 (Des. 12, 2015), <https://www.refworld.org/legal/general/achpr/2015/en/70896>.

⁶⁹Angalia, kwa mfano, Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 143–145, 152 (Juni 4, 2024); Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 107–111 (Novemba 28, 2019); Ghati Mwita dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 012/2019, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 78 (Desemba 1, 2022); Forum of Conscience dhidi ya Sierra Leone, Na. 223/98, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 19 (Novemba 6, 2000); Gozbert Henerico dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 056/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 149–50 (Januari 10, 2022); Amini Juma dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 024/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 130 (Septemba 30, 2021).

⁷⁰Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 104 (Novemba 28, 2019).

⁷¹Marthine Christian Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 052/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 86–87, 107–110 (ucheleweshaji wa muda mrefu), ¶¶ 88–101 (uwakilishi hafifu) (Desemba 1, 2022).

46. 46. Mbali na matatizo haya ya mchakato, adhabu ya kifo inakiuka Kifungu cha 4 kwa sababu ya ziada kwamba inatolewa kwa njia ya kibaguzi, ikionyesha zaidi ukatili wake kwa asili. Mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu yenye utaalamu katika adhabu ya kifo, kama vile Amnesty International, yamerekodi tatizo hili kuhusiana na utoaji wa adhabu ya kifo kwa vitendo, yakibaini kwamba adhabu ya kifo "mara nyingi hutumiwa kwa njia isiyo ya uwiano dhidi ya walio maskini, wachache na watu walio katika makundi ya rangi, kabila na dini fulani. Inatolewa na kutekelezwa kiholela...[na] kutumika kama chombo cha ukandamizaji – njia ya haraka na ya kikatili ya kunyamazisha upinzani wa kisiasa."⁷²
47. Mahakama barani Afrika zimetambua tatizo hili pia. Kwa mfano, Mahakama ya Katiba ya Afrika Kusini, ilibaini hapo awali kwamba, kwa uhalisia, adhabu ya kifo mara nyingi hutolewa kiholela na bila usawa kama matokeo ya masuala ya rangi, umaskini, fursa, ushauri usiofaa, vikwazo vya lugha, na upendeleo wa mahakama.⁷³ Kuna mifano mingi inayoonyesha kwamba, barani Afrika (kama kwingineko), adhabu ya kifo hutolewa kwa njia ya kibaguzi kwa wanawake, watoto, watu wa makabila tofauti, wale wanaoishi katika hali ngumu ya kiuchumi, na watu wa makundi fulani ya kisiasa.
48. 48. Sheria ya kimataifa inahitaji kwamba nchi zizingatie viwango vikali zaidi vya mchakato unaostahili wakati wa kutafuta kutoa adhabu ya kifo kwa kuzingatia uzito na ukali wa adhabu inayoondoa uhai wa binadamu.⁷⁴

⁷² Campaigning Toolkit, Death Penalty the Ultimate Punishment (Juni 2021), AMNESTY INT'L, 2, <https://www.amnesty.org/en/wp-content/uploads/2021/06/act500152008eng.pdf>; angalia pia What We Do: Death Penalty, AMNESTY INT'L, [hereinafter "Death Penalty, AMNESTY INT'L"] <https://www.amnesty.org/en/what-we-do/death-penalty/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 7, 2024) (ikijenga hoja kwamba "uzito wa adhabu ya kifo unachukuliwa kwa njia isiyolingana kwa wale walio na ushawishi mdogo wa kijamii na kiuchumi au walio wa mbari, kabila au dini ya watu wachache. Kwa mfano, hii ni pamoja na kuwa na ufikiaji mdogo wa uwakilishi wa kisheria, au kuathiriwa sana katika uzoefu wao wa mfumo wa haki ya jinai.").

⁷³ Angalia kwa ujumla Serikali dhidi ya T. Makwanyane na M. Mchunu, (16) HRLJ 154 (CC) (S. Afr.) (Juni 6, 1995).

⁷⁴ Angalia, kwa mfano, Hilaire, Angalia, kwa mfano, Hilaire, Constantine na Benyamini na Wengine dhidi ya Trinidad na Tobago, Uzingatiaji wa Sheria, Fidia, na Gharama, Hukumu, Inter-Am. Ct. H.R. (ser. C) Na. 94, ¶ 148 (Juni 21, 2002) ("Kwa kuzingatia hali mbaya sana na isiyoweza kurekebisha ya adhabu ya kifo, uzingatiaji wa mchakato unaostahili, pamoja na kifungu chake cha haki na

Kama ilivyojadiliwa zaidi hapa chini, ushahidi kuhusu hali ya sasa ya mambo katika nchi za Afrika zinazotoa adhabu ya kifo unaonyesha kwamba hazifikii kiwango cha uhuru dhidi ya uholela ambao unapaswa kuhitajika kabla ya adhabu ya kifo kutolewa. Badala yake, ukweli ni kwamba utoaji wa adhabu ya kifo kwa uhalisia unakabiliwa na uholela na, kwa hivyo, unakiuka Kifungu cha 4.⁷⁵

i. Ukosefu wa Mchakato Unaostahili Katika Utekelezaji wa Adhabu ya Kifo katika Uhalisia

49. Kukosekana kwa mfumo wowote wa haki, yaani, uwezekano wa mtu kuhukumiwa kimakosa au kuadhibiwa kwa adhabu ambayo ni kali sana wakati wa kuzingatia hali zote, ni wasiwasi mkubwa katika kesi yoyote ya jinai. Lakini katika kesi ambayo mshtakiwa anakabiliwa na kupoteza maisha yake, kasoro zinazoharibu ubora wa haki na mchakato unaostahili anaopokea mshtakiwa haziwezi kuvumilika kama suala la kanuni za msingi za haki za binadamu. Barani Afrika, licha ya matakwa thabiti ya sheria ya kimataifa ya mchakato stahiki kwa kesi za adhabu ya kifo, matatizo ya mchakato stahiki, na hasa ukosefu wa uwakilishi wa kutosha, husababisha utoaji wa adhabu ya kifo, kama ilivyoonyeshwa na mifano ifuatayo.

dhamana, unakuwa muhimu zaidi wakati maisha ya binadamu yako hatarini."); Medellín, Ramírez Cardenas na Leal García dhidi ya Marekani, Ukubalifu na Uzingatiaji wa Sheria (Chapisho), Inter-Am. Comm'n H.R., Repoti Na. 90/09, Kesi na. 12.644, ¶¶ 122–123 (Agosti 7, 2009) ("Tume ... inaona kwamba ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba kuondoa uhai ambako kunaweza kutokea kupitia matumizi ya adhabu ya kifo kunafuata kikamilifu mtakwa ya vyombo vya haki za binadamu bara la Amerika. ... 'Jaribio hili la uchunguzi wa hali ya juu' linaambatana na mbinu ya kuzuia iliyochukuliwa na mamlaka nyingine za kimataifa za haki za binadamu kuhusu utoaji wa adhabu ya kifo na limeelezwa na kutumiwa na Tume katika kesi za awali kabla yake. Kwa hivyo Tume itapitia madai ya mleta maombi katika kesi ya sasa kwa kiwango cha juu cha uchunguzi, ili kuhakikisha hasa kwamba haki ya kuishi, haki ya mchakato unaostahili, na haki ya kusikilizwa kwa haki...zinaheshimiwa ipasavyo na Serikali.") ; Chad Roger Goodman dhidi ya Bahamas, Uzingatiaji wa Sheria (Chapisho), Inter-Am. Comm'n H.R., Na. 78/07, Kesi na. 12.265, ¶ 34 (Oktoba 15, 2007) ("['Jaribio la uchunguzi wa hali ya juu'] linahitaji hasa kuzingatia kikamilifu sheria na kanuni za mchakato unaofaa na uendeshaji kesi wa haki katika muktadha wa kesi za hukumu ya kifo. Tume hapo awali imesisitiza kwamba, kwa sababu ya asili yake isiyoweza kubatilishwa na isiyoweza kubadilishwa, adhabu ya kifo... inalazimisha kuwe na mchakato wa kuaminika katika kuamua ikiwa mtu anawajibika kwa uhalifu ambao adhabu yake ni kifo.").

⁷⁵ Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, angalia supra n.21, mifano iliyowekwa hapa imekusudiwa kuionyesha Mahakama viwango halisi vya utoaji wa adhabu ya kifo barani Afrika na kuonyesha jinsi ambavyo haiwezi kutolewa kwa njia ambayo sio ya kiholela.

1. Masuala ya Mchakato Stahiki katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na Visa vya Unyongaji vya Hivi Karibuni

50. Kama ilivyoielezwa, nchi nne tu Wanachama wa Umoja wa Afrika: Misri, Somalia, Sudan Kusini na Botswana ndizo zimetekeleza hukumu ya kifo tangu 2021.⁷⁶ Kila moja ya hizi ina kasoro zinazoonekana katika mifumo yake ambayo husababisha kushindwa kutoa kiwango kinachohitajika cha mchakato unaofaa na kusababisha kutolewa kwa adhabu ya kifo kiholela na isivyofaa.
51. **Misri:** Misri ilinyonga angalau watu 230 kati ya Januari 2020 na Machi 2022⁷⁷ na imeripotiwa kuwa imenyoga watu wanane mwaka 2023.⁷⁸ Misri inatoa hukumu za kifo kwa idadi kubwa zaidi. Kulingana na wachunguzi huru, mwaka 2023, mahakama za Misri zilitoa hukumu za kifo kwa angalau watu 348 na Mahakama ya Kadhi ilithibitisha hukumu za kifo kwa angalau watu 27.⁷⁹ Makundi ya haki yamebaini ukiukaji wa utaratibu unaostahili katika kesi za adhabu ya kifo nchini Misri. Hizi ni pamoja na kesi zilizo mbele ya mahakama za kijeshi na Mahakama za Dharura za Usalama wa Taifa ambapo washtakiwa kesi zao zilisikilizwa ili mradi kutimiza taratibu ambapo mamlaka hazikutoa mashtaka rasmi au

⁷⁶Angalia Death Sentences and Executions in 2021, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 40, 51–52, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (imefunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024) (ikibainisha Misri, Somalia, Sudani Kusini, na Botswana kuwa nchi pekee Wanachama wa Umoja wa Afrika zilizotekeleza adhabu ya kifo mwaka 2021); Death Sentences and Executions in 2022, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 28, 33–34, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/6548/2023/en/> (imefunguliwa mara ya mwisho Agosti 1, 2024) (ikibainisha Misri, Somalia, na Sudani Kusini kuwa nchi pekee Wanachama wa Umoja wa Afrika zilizotekeleza adhabu ya kifo mwaka 2022).

⁷⁷ Egypt's Compliance with the Convention against Torture and Other Cruel Inhuman or Degrading Treatment or Punishment: the death penalty, THE ADVOCATES FOR HUMAN RIGHTS, REPRIEVE, AND WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY, (Okt. 2, 2023), <https://www.theadvocatesforhumanrights.org/Res/AHR%20WCADP%20Reprieve%20Egypt%20CAT%20Final%20.pdf>.

⁷⁸ Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 9, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/7952/2024/en/#:~:text=Amnesty%20International's%20monitoring%20of%20the,2022%20to%2016%20in%202023> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024).

⁷⁹ Decrease in the Implementation of the Death Penalty or Increase in Restrictions on Access to Information?: Monitoring Report on the Status of the Death Penalty in Egypt during the Year 2023, EGYPTIAN FRONT FOR HUMAN RIGHTS (Feb. 26, 2024), <https://egyptianfront.org/2024/02/decrease-in-the-implementation-of-the-death-penalty-or-increase-in-restrictions-on-access-to-information-monitoring-report-on-the-status-of-the-death-penalty-in-egypt-during-the-year-2023/>.

kuwasilisha ushahidi na wafungwa hawakuruhusiwa kujitetea.⁸⁰ Baada ya kueleza ukweli huu, Amnesty International ilibaini kwamba mahakama za nchi hiyo zilitoa hukumu za kifo baada ya kesi ambazo hazikukidhi viwango vya kimataifa vya kusikilizwa kwa haki.⁸¹

52. Kwa mfano, mnamo Juni 2022, kitengo cha ugaidi cha Mahakama ya Makosa ya Jinai ya jijini Cairo iliwahukumu wanaume 10 adhabu ya kifo kwa kosa la "ugaidi" na mauaji baada ya kesi ambayo haikuendeshwa kwa haki kabisa, ambapo wengi walikuwa wametekwa na kuteswa, kunyimwa haki ya kuwakilishwa na mawakili wao, na kushikiliwa katika hali za kikatili na za kinyama ambazo ni sawa na kuteswa.⁸² Mfano huu si tukio la nadra; kulingana na taarifa kutoka katika makundi ya kutetea haki ya eneo husika, ukamatati wa mamia ya watu waliohusishwa na ugaidi haukuzingatia mchakato unaofaa, watuhumiwa hawakushtakiwa kwa makosa ya uhalifu, hawakupelekwa kwa waendesha mashtaka, na/au walinyimwa fursa ya kukutana na wakili na familia zao.⁸³
53. Aidha, makundi ya kutetea haki za binadamu yamebaini ushahidi wa ukiukaji wa mara kwa mara wa mchakato katika mfumo wa mahakama ya kiraia wa Misri kuhusiana na kesi za adhabu ya kifo, ikiwa ni pamoja na lakini si tu kutesa ili mtu akiri kosa, fursa ndogo ya kumpata wakili, kutokuwa na uwazi, uchunguzi hafifu wa madai ya mateso, na kutumia njia

⁸⁰ Yee na wenzake, Egypt's Revolving Jailhouse Door: One Pretrial Detention After Another, NEW YORK TIMES, (Julai 16, 2022), <https://www.nytimes.com/interactive/2022/07/16/world/middleeast/egypt-prisoners.html>. Angalia pia infra ¶ 101.

⁸¹ Egypt Report 2023, AMNESTY INT 'LINT' L, <https://www.amnesty.org/en/location/middle-east-and-north-africa/north-africa/egypt/report-egypt/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 7, 2024).

⁸²

⁸² Wasilisho kwa Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa. Kikao cha 137, 27 Februari – 24 Machi 2023, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 7, <https://www.amnesty.org/en/wp-content/uploads/2023/01/MDE1263762023ENGLISH.pdf> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 7, 2024).

⁸³ Yee na wenzake, Egypt's Revolving Jailhouse Door: One Pretrial Detention After Another, NEW YORK TIMES, (Julai 16, 2022), <https://www.nytimes.com/interactive/2022/07/16/world/middleeast/egypt-prisoners.html>. Angalia pia Amr Ahmed Ibrahim, The Façade of Dialogue and Political Openness: Egypt's Increasing Repression and Arbitrary Detention, TAHRIR INSTITUTE FOR MIDDLE EAST POLICY (Juni 21, 2023), <https://timep.org/2023/06/21/the-facade-of-dialogue-and-political-openness-egypts-increasing-repression-and-arbitrary-detention/> (ikinukuu Arrest and Detention on Political Background Report 2018–2023, SHAFAFIA TRANSPARENCY CENTER FOR RESEARCH, ARCHIVING, AND DATA MANAGEMENT, <https://drive.google.com/file/d/1nJSwb9BLQ4ZSEQmeUUGfNuwwqK5ATkxb8/view>).

ya kusikiliza kesi za pamoja ili kuwahukumu kifo.⁸⁴ Aidha, mwaka 2017 Misri ilipunguza uwezo wa Mahakama ya Kadhi, mahakama ya juu kabisa ya Misri, kubadilisha hukumu na kupeleka kesi isikilizwe mara ya pili, na hivyo kuwaondolea washtakiwa wa adhabu ya ukaguzi muhimu kwenye hukumu zenye kasoro, jambo ambalo Amnesty International imeelezea kuwa "msumari katika jeneza la viwango vya kusikiliza kesi kwa haki."⁸⁵

54. **Somalia:** Somalia, ambayo imekuwa ikitekeleza adhabu ya kifo mara kwa mara katika miaka kadhaa iliyopita, pia inaonyeshwa kuwa na makosa ya msingi kwenye mchakato stahili na kutoa hukumu za kiholela. Kulingana na Amnesty International, kulikuwa na zaidi ya watu 38 waliouawa kwa kunyongwa nchini Somalia mwaka 2023,⁸⁶ na ripoti zinaonyesha kuwa Somalia tayari imetekeleza unyongaji wa watu watatu waliouawa mwaka 2024.⁸⁷ Kuhusiana na kunyongwa nchini Somalia, shirika la Human Rights Watch limeripoti kwamba mamlaka nchini Somalia mara nyingi zilitekeleza hukumu ya kifo kwa kunyonga, ikiwa ni pamoja na raia kunyongwa, kufuatia taratibu za mahakama za kijeshi ambazo zilikiuka viwango vya kimataifa vya kusikiliza kesi kwa haki.⁸⁸ Msingi wa mashtaka katika

⁸⁴Egypt's Compliance with the Convention against Torture and Other Cruel Inhuman or Degrading Treatment or Punishment: the death penalty, THE ADVOCATES FOR HUMAN RIGHTS, REPRIEVE, AND WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY, (Okt. 2, 2023), <https://www.theadvocatesforhumanrights.org/Res/AHR%20WCADP%20Reprieve%20Egypt%20CAT%20Final%20.pdf>; Jeed Basyouni, The Death Penalty in Egypt – Ten Years After the Uprising, REPRIEVE, ukurasa wa 10, 13–14 (Mei 24, 2021), <https://reprieve.org/uk/2021/05/24/the-death-penalty-in-egypt-ten-year-after-the-uprising/>.

⁸⁵ Jeed Basyouni, The Death Penalty in Egypt – Ten Years After the Rerising, ukurasa wa 14 (Mei 24, 2021), <https://reprieve.org/uk/2021/05/24/the-death-penalty-in-egypt-ten-year-after-the-uprising/> (nukuu za ndani zimeachwa).

⁸⁶ Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 9, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/7952/2024/en/#:~:text=Amnesty%20International's%20monitoring%20of%20the,2022%20to%2016%20in%202023> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024); angalia pia Death Sentences and Executions in 2022, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 34 (Somalia ilinyonga angalau watu 6 mwaka 2022), <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/6548/2023/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024); Death Sentences and Executions in 2021, AMNESTY INT'LINT'L, ukurasa wa 60 (Somalia ilinyonga angalau watu 21 mwaka 2021), <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (ilitembelewa mara ya mwisho Juni 6, 2024).

⁸⁷ Angalia Somalia: Somali Military Court Executes Three Men for Murder of Two Brothers, SHABELLE MEDIA NETWORK (MOGADISHU) (Juni 6, 2024), <https://allafrica.com/stories/202406070063.html#:~:text=Somalia%3A%20Somali%20Military%20Court%20Execut>.

⁸⁸Somalia. Events of 2023, HUMAN RIGHTS WATCH, <https://www.hrw.org/world-report/2024/country-chapters/somalia#:~:text=Authorities%20throughout%20the%20country%20carried,forces%2C%20oft en%20after%20unfair%20trials> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024).

mahakama hizo za kijeshi nchini Somalia mara nyingi hauko wazi na adhabu ya kifo hutolewa kiholela.⁸⁹

55. Aidha, Kamati ya Kupinga Mateso imeripoti kwamba mahakama hizo za kijeshi "zinaendesha kesi za kiraia, ikiwa ni pamoja na kesi zinazohusu vijana...[lakini] hazihakikishi mchakato unaostahili kwa mujibu wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuwapa washtakiwa uwakilishi wa kisheria na haki ya kukata rufaa, na uendeshaji wake wa kesi hauna uwazi."⁹⁰ Kwa sababu ya Somalia kutumia mahakama za kijeshi kuendesha kesi na kuwahukumu raia adhabu ya kifo, ni vigumu kujua ikiwa mahakama za kiraia za Somalia pia zimetoa hukumu ya kifo katika miaka ya hivi karibuni. Lakini kumbukumbu ziko dhahiri kwamba Somalia inaendelea kutumia mahakama za kijeshi kuwahukumu raia adhabu ya kifo na kutekeleza adhabu ya kifo, ikiwa ni pamoja na hivi karibuni mwezi Juni 2024, licha ya kuenea kwa matatizo makubwa ya mchakato unaostahili yaliyobainishwa katika mahakama hizo za kijeshi.⁹¹

56. Sudan Kusini: Sudan Kusini, ambayo ilitekeleza adhabu ya kifo mwaka 2022 na 2021, ina matatizo kama hayo ya mchakato unaostahili kuhusiana na adhabu ya kifo.⁹² Inafanya kazi chini ya serikali ya mpito na mfumo wake wa haki haufikii viwango vya kimataifa. ⁹³ Kwa mfano,

⁸⁹ Vanda Felbab-Brown, *The Limits of Punishment: Transitional Justice and Violent Extremism*, ukurasa wa 11 (Mei 2018), <https://i.unu.edu/media/cpr.unu.edu/attachment/2770/4-LoP-Somalia-Case-Study.pdf>.

⁹⁰ Concluding Observations on the initial report of Somalia, CAT/C/SOM/CO/1, U.N. Committee Against Torture, ¶ 13 (Des. 2, 2022). Angalia pia Corinne Noonan, *Calling for Somaliland to Release Abshir Saleban Hussein, a Child, from Death Row*, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Julai 31, 2024), <https://deathpenaltyworldwide.org/calling-for-somaliland-to-release-abshir-saleban-hussein-a-child-from-death-row/> (ikijadili kesi ya hivi karibuni ya Februari mwaka 2024 ambapo mahakama ya Somaliland ilimhukumu mtoto kifo).

⁹¹ Angalia Somalia: Somali Military Court Executes Three Men for Murder of Two Brothers, SHABELLE MEDIA NETWORK (MOGADISHU) (Juni 6, 2024), <https://allafrica.com/stories/202406070063.html#:~:text=Somalia%3A%20Somali%20Military%20Court%20Execut>.

⁹² *Death Sentences and Executions in 2022*, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 34 (Sudani Kusini ilinyonga angalau watu 5 mwaka 2022), <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/6548/2023/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024); *Death Sentences and Executions in 2021*, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 60 (Sudani Kusini ilinyonga angalau watu 9 mwaka 2021), <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024).

⁹³ Taarifa kwa Vyombo vya Habari, *Disturbing wave of extrajudicial executions on the rise in South Sudan's Warrap State – UN experts note*, U.N. Press Release (Julai 29, 2021),

mamlaka za utekelezaji wa sheria na mahakama, zimewaweka washtakiwa chini ya kizuizini cha muda mrefu bila fursa ya kutosha ya kuandaa utetezi⁹⁴ na zimeripotiwa kuwahukumu kifo watu binafsi kwa uhalifu walioufanya wakiwa watoto.⁹⁵ Cha kusikitisha zaidi, washtakiwa wengi walihukumiwa kifo bila kupata uwakilishi wowote wa kisheria.⁹⁶

57. Botswana: Botswana, ambayo iliwanyoga watu watatu mnamo mwaka 2021,⁹⁷ pia inakabiliwa na matatizo yanayofanana ya mchakato unaostahili, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa uwakilishi wa kutosha wa kisheria kwa washtakiwa wa jinai katika kesi zenye adhabu ya kifo . Wakati wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo wana haki rasmi ya uwakilishi wa kisheria, wakili huyo anayeteuliwa na serikali kwa ujumla hana ujuzi na mafunzo ya kuwatetea wateja wake waliohukumiwa kifo.⁹⁸ Kwa sababu ya vikwazo vya kifedha, ada zinazolipwa kwa mawakili walioteuliwa na serikali ni ndogo ikilinganishwa na ada za wastani zinazolipwa kwa mawakili wa kujitegemea, na kesi za adhabu ya kifo

<https://www.ohchr.org/en/press-releases/2021/07/disturbing-wave-extrajudicial-executions-rise-south-sudans-warrap-state-un>.

⁹⁴ Angalia, kwa mfano, "Prison Is Not For Me." Arbitrary Detention in South Sudan, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 4–5 (Juni 21, 2022), <https://www.hrw.org/report/2012/06/21/prison-not-me/arbitrary-detention-south-sudan>.

⁹⁵ Angalia, kwa mfano, Ripoti ya Wadau wa Sudan Kusini ya Kikao cha 40 cha Kikosi Kazi cha Tathmini Majumui cha Umoja wa Mataifa, WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU NA MUUNGANO WA KIMATAIFA DHIDI YA

ADHABU YA KIFO, ¶16 (Julai 15, 2021),

<https://www.theadvocatesforhumanrights.org/Res/South%20Sudan%20Death%20Penalty%20Report%20Final%202.pdf>.

⁹⁶ Angalia, kwa mfano, id. ukurasa wa 17; Rachel Ibreck na wengine., Negotiating Justice: Courts as local civil authority during the conflict in South Sudan, ukurasa wa 8–9 (2017), <https://research.gold.ac.uk/id/eprint/21114/1/17-0048-Sudan-Report-v9.Web.pdf>. Angalia pia, "Prison Is Not For Me." Arbitrary Detention in South Sudan, HUMAN RIGHTS WATCH, ukurasa wa 5, 11 (Juni 21, 2022), <https://www.hrw.org/report/2012/06/21/prison-not-me/arbitrary-detention-south-sudan> (ikisema takriban asilimia 95 ya wafungwa nchini Sudan Kusini wanapitia mfumo wa utaoaji haki katika makosa ya jinai bila ushauri na "wanahukumiwa kifo ingawa hawajaweza kuwaita na kuwaandaa mashahidi katika utetezi wao" na kuelezea kukosekana kwa msaada mzuri wa kisheria nchini Sudan Kusini).

⁹⁷ Death Sentences and Executions in 2021, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 60, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024) (Botswana ilinyonga watu 3 mwaka 2021).

⁹⁸ Elizabeth Macharia-Mokobi, The Death Penalty In Botswana: Time For a Re-Think?, SOUTH AFRICA MIGRATION CENTRE, ukurasa wa 70–71 (2017), <https://www.southernafricalitigationcentre.org/wp-content/uploads/2017/08/GOAL-16-Book-Mokobi.pdf>; The death penalty in Botswana: Hasty and secretive hangings: International fact finding mission, INTERNATIONAL FEDERATION FOR HUMAN RIGHTS (FIDH) AND DITSHWANELO – The Botswana Centre for Human Rights, ukurasa wa 21 (Juni 2007), <https://www.fidh.org/en/region/Africa/botswana/The-Death-Penalty-in-Botswana>.

zimekuwa zikishughulikiwa vibaya na mawakili wachanga kitaaluma ambao hawana uzoefu wowote katika kesi za adhabu ya kifo.⁹⁹ Aidha, kuna kesi za adhabu ya kifo zilizoripotiwa ambapo mzigo wa kutoa ushahidi limehamishiwa kwa mshtakiwa.¹⁰⁰ Ubadilishaji huu usiofaa wa mzigo wa kutoa ushahidi, pamoja na kushindwa kwa serikali kutoa uwakilishi wa kisheria wa kutosha, husababisha kuharibika kwa haki na utoaji wa adhabu ya kifo kwa kukiuka ulinzi wa mchakato unaostahili na kinyume cha marufuku ya uholela.

2. Kushindwa Kutoa Uwakilishi wa Kisheria wa Kutosha kwa Washtakiwa wa Adhabu ya Kifo

58. Kuhusiana na mifano iliyotajwa hapo juu, na kuhusiana na utoaji wa adhabu ya kifo barani Afrika kwa ujumla zaidi, tatizo linalosumbua la mchakato unaostahili ni ukosefu wa uwakilishi sahihi wa kisheria kwa watu wanaokabiliwa na adhabu ya kifo.¹⁰¹ Ingawa ni nchi nne tu Wanachama wa Umoja wa Afrika ndizo zilizotekeleza adhabu ya kifo katika miaka ya hivi karibuni, nchi nyingine kadhaa Wanachama wa Umoja wa Afrika zinaendelea kutoa adhabu ya kifo licha ya kushindwa kutoa uwakilishi wa kisheria wa kutosha kwa washtakiwa.¹⁰² Kwa mfano, nchini Nigeria, washtakiwa wa adhabu ya kifo ni mara chache wanapata uwakilishi wa kisheria wa kutosha, kwa upande fulani, kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali za msaada wa kisheria, ikiwa ni pamoja na uhaba wa mawakili ambao wana utaalamu katika utetezi wa makosa ya jinai na ukosefu wa

⁹⁹ Onkemetse B. Tshosa, The death penalty in Botswana in the light of international law: The case for abolition, BIICL, ukurasa wa 6–7 (2004), https://www.biicl.org/files/2216_tshosa_death_penalty_botswana.pdf.

¹⁰⁰ Andrew Novak, Guilty of Murder with Extenuating Circumstances: Transparency and the Mandatory Death Penalty in Botswana, BOSTON UNIVERSITY INTERNATIONAL LAW JOURNAL, ukurasa wa 187–88 (2009).

¹⁰¹ Angalia S. L. Babcock, An Unfair Fight for Justice: Legal Representation of Persons Facing the Death Penalty, in COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT (Ed. Carol S. Steiker na Jordan M. Steiker), ukurasa wa 97–105 (2019) (inajadili vikwazo halisi vya uwakilishi wa kisheria wa kutosha na wenye ufanisi katika kesi za adhabu ya kifo barani Afrika na ulimwenguni).

¹⁰² Angalia, kwa mfano, Death Sentences and Executions in 2023, AMNESTY INT'L, at 29, 35–36, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/7952/2024/en/#:~:text=Amnesty%20International's%20mo%20nitoring%20of%20the,2022%20to%2016%20in%202023> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 4, 2024) (ikibainisha kutolewa kwa hukumu za kifo mwaka 2023 katika Nchi nyingi Wanachama wa Afrika ambazo hazijafanya utekeleza unyongaji uliorekodiwa tangu mwaka 2021, ikiwa ni pamoja na Nigeria (hukumu za kifo 246) na Kenya (hukumu za kifo 131)).

ofisi za msaada wa kisheria katika maeneo ya vijijini.¹⁰³ Hii ni kweli hasa kwa washtakiwa maskini na fukara ambao mara kwa mara wanapata shida kupata uwakilishi, hasa katika ngazi ya rufaa, na ambao ni wengi kati ya wale ambao wanakabiliwa na kesi.¹⁰⁴ Zaidi ya hayo, maaskari mara kwa mara wanajaribu kuwfunya wafungwa wakiri makosa wanapokuwa kizuizini kabla ya kusikilizwa kesi, haki ambayo mara nyingi inaweza kudumu kwa miaka mingi, ambapo bado wanakuwa hawana uwezo wa kupata wakili.¹⁰⁵ Kushindwa huku kutoa uwakilishi wa kisheria katika kesi za jinai, pamoja na kesi za adhabu ya kifo, husababisha kukataliwa kwa mchakato unaostahili; na pia husababisha matokeo mabaya na ya kiholela, kati ya wale ambao wana uwakilishi na ambao hawajapewa.

59. Aidha, baadhi ya Mataifa hutoa msaada wa kisheria bila malipo pale tu ambapo kesi inafika kwenye hukumu, na matokeo yake ni kwamba watu masikini mara nyingi wanakabiliwa na kuhojiwa na uchunguzi bila msaada wa wakili, na kusababisha wasiwasi mkubwa wa mchakato unaostahili, ikiwa ni pamoja na kukiri makosa kwa kulazimishwa.¹⁰⁶ Katika hali hizi, haki ya mshtakiwa ya kusikilizwa kwa haki inaweza kuwa tayari imepotea wakati kesi itakapofika mahakamani.¹⁰⁷

¹⁰³ Paulina Lucio Maymon, Nigeria's Debate on Death Penalty: Sign Execution Warrants or Impose a Moratorium?, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Juni 26, 2019), <https://deathpenaltyworldwide.org/nigerias-debate-on-capital-punishment-sign-execution-warrants-or-impose-a-moratorium/>.

¹⁰⁴ 104 Id.

¹⁰⁵ 105 Id.

¹⁰⁶ Kwa mfano, zaidi ya theluthi moja ya wafungwa waliohukumiwa kifo nchini Kenya walinyimwa msaada wa kisheria wakati wakihojiwa na polisi. Carolyn Hoyle na Lucrezia Rizzelli, Living With a Death Sentence in Kenya: Prisoners' Experiences of Crime, Punishment and Death Row, ukurasa wa 49–50 (2022), <https://deathpenaltyproject.org/wp-content/uploads/2022/12/Living-with-a-Death-Sentence-in-Kenya-Prisoners-Experiences-of-Crime-Punishment-and-Death-Row.pdf>. Na katika baadhi ya nchi, kama vile Uganda, raia wa kigeni wanaweza wasipewe dhamana ya wakili aliyeteuliwa na serikali wanaposhtakiwa kwa kosa dhidi ya usalama wa Nchi (kosa ambalo adhabu yake ni kifo). Ripoti ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Adhabu ya kifo na utekelezaji kanuni zilizowekwa ili kuhakikisha ulinzi wa haki za wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo, A/HRC/36/26, ¶ 28 (Agosti 22, 2017), <https://documents.un.org/doc/undoc/gen/g17/244/09/pdf/g1724409.pdf>.

¹⁰⁷ Angalia Taarifa kwa Vyombo vya Habari, Adhabu ya Kifo Inaathiri vibaya Maskini, Wataalamu wa Haki wa Umoja wa Mataifa Wanaonya, Taarifa kwa Vyombo vya Habari kutoka Umoja wa Mataifa (Oktoba 10, 2017) [hapa inarejelewa kama "Tamko la Pamoja la Umoja wa Mataifa"], <https://www.ohchr.org/en/press-releases/2017/10/death-penalty-disproportionately-affects-poor-un-rights-experts-warn> (msisitizo umeongezwa).

60. Hata katika nchi ambazo washtakiwa wa makosa ya jinai (ikiwa ni pamoja na washtakiwa katika kesi za adhabu ya kifo) wana haki ya kikatiba au ya kisheria ya kupata uwakilishi, wengi hawapati uwakilishi unaofaa au uwakilishi wowote. Mahakama (au mamlaka ya serikali) mara nyingi hushindwa kuwapatia washtakiwa masikini wakili katika kesi za makosa ya jinai, ikiwa ni pamoja na kesi za adhabu ya kifo. Bila uwezo wa kulipia mawakili binafsi au kuomba msaada wa mashirika yasiyotengeneza faida, watu wengi wamehukumiwa kifo bila uwakilishi wa kisheria. Kwa mfano, nchini Sudan Kusini, ingawa Sheria ya Utaratibu wa Makosa ya Jinai inaonesha kuwa mawakiliwa wanatolewa kwa washtakiwa maskini, kwa kweli hakuna msaada wa kisheria unaopatikana au muundo wowote wa kisheria wa kutoa msaada huo.¹⁰⁸ Kutokuwepo kwa wakili kunamaanisha kwamba karibu wafungwa wote walionyongwa hawakupokea uwakilishi katika kesi ambayo ilisababisha wao kukutwa na hatia na hatimaye kuhukumiwa kifo.¹⁰⁹
61. Hata katika nchi ambazo zinaonekana kuwa na muundo wa kutoa msaada wa kisheria, ukosefu wa fedha serikalini mara kwa mara husababisha washtakiwa kuhukumiwa bila uwakilishi au bila kuwasiliana na watetezi wao vya kutosha, kinyume cha haki zao za mchakato unaostahili.¹¹⁰ Kwa mfano, utafiti wa mwaka 2022 nchini Kenya, uliripoti kwamba karibu robo ya wafungwa waliohukumiwa kifo hawakupata uwakilishi wa kisheria wakati wa kusikiliza kesi na karibu nusu waliripoti kutopokea msaada wa kisheria wakati wa rufaa yao.¹¹¹

¹⁰⁸ Jamhuri ya Sudan Kusini, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Aprili 25, 2013), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=69>.

¹⁰⁹ Id.

¹¹⁰ Angalia S. L. Babcock, An Unfair Fight for Justice: Legal Representation of Persons Facing the Death Penalty, in *COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT* (Ed. Carol S.

¹¹¹ Steiker na Jordan M. Steiker), 100–02 (2019) (inajadili ukosefu wa rasilimali za serikali zinazopatikana kwa ajili ya watetezi wa umma na ugumu halisi katika kuhakikisha mfungwa anapata wakili katika nchi kadhaa za Kiafrika). Carolyn Hoyle na Lucrezia Rizzelli, ukurasa wa 50; angalia pia Ripoti ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, supra n.106 ukurasa wa ¶ 17. Aidha, nchini Kenya hakuna watetezi wa umma wanaofadhiliwa na serikali, na mashirika ya ndani yasiyo ya kiserikali hayawezi kukidhi mahitaji ya wakili. Kwa sababu hiyo, washtakiwa wengi wanajiwakilisha wenyewe au wanategemea huduma za kisheria gerezani. Angalia, kwa mfano, Damaris Kemunto, Legal And Regulatory Gaps Inherent to the Implementation Of the Legal Aid Act, INTERNATIONAL COMMISSION OF JURISTS (Machi 6, 2024), <https://icj-kenya.org/news/legal-and-regulatory-gaps-inherent-to-the-implementation-of-the-legal-aid-act/>; Keith Zubrow, How COVID-19

62. Hata pale ambapo uwakilishi hutolewa, uteuzi wa wakili mara nyingi linakuwa ni jambo la kutimiza wajibu tu ambalo halisababishi kuwa na uwakilishi wenye ufanisi. Kwa mfano, nchini Botswana, mahakama zimeripoti na kusesitiza katika maoni ya hadharani uhalisia wa uwakilishi duni katika kesi za hukumu ya kifo.¹¹² Katika kesi moja ya mauaji, mawakili wa awali walioteuliwa na mahakama hawakuwahi kushauriana na washtakiwa, na walishindwa kuwajulisha washtakiwa kuhusu mambo wanayoweza kufanya chini ya sheria ya Botswana kutoa ushahidi wakati wa kusikiliza kesi.¹¹³ Aidha, kesi za hukumu ya kifo mara nyingi hushughulikiwa na mawakili wasio na uzoefu, kwa sababu, kwa sehemu fulani, katika kesi nyingi za hukumu ya kifo, ada za mawakili mara nyingi hazilipwi kabisa, au hulipwa kwa kuchelewa sana, kiasi kwamba mawakili wenye uzoefu wanakuwa hawana hamasa ya kushughulika na kesi hizo.¹¹⁴
63. Hatimaye, hata pale ambapo uwakilishi hutolewa, mara nyingi kuna kuwa na tofauti kubwa katika upatikanaji wa wakili kati ya jamii za vijijini na mijini. Katika nchi nyingi, mawakili hawawezi kuwafikia wateja wao kwa sababu ya jinsi walivyo mbali na jiji. Kwa mfano, nchini Mali, ambapo unyongaji wa mara ya mwisho unaojulikana ulifanywa miaka mingi iliyopita lakini watu wengi wanabaki kwenye hukumu ya kifo, utafiti ulibaini kuwa wengi wa wanasheria 275 katika nchi hiyo walifanyia shughuli zao katika

transformed the Kenyan court system, CBS NEWS (Agosti 15, 2021), <https://www.cbsnews.com/news/covid-19-kenya-court-system-60-minutes-2021-08-15/>.

¹¹²Angalia Gorosang v. State, Criminal Appeal No. 95 of 2012, Judgement, Ct. of Appeal of Botswana, BWCA 40, ¶ 3 (Februari 1, 2013) (ikibainisha kwamba kesi hiyo "iliharibiwa. .. na uchunguzi usiotosha, mashtaka yasiyotoshelevu, na utetezi usiotoshelevu, ambao una athari muhimu kwa matokeo."). Angalia pia Alice Mogwe, The Death Penalty in Botswana: Barriers to Equal Justice, in MOVING AWAY FROM THE DEATH PENALTY: ARGUMENTS, TRENDS AND PERSPECTIVES, 170, 174 (Ivan Simonovic ed., Sept. 21, 2015), <https://www.ohchr.org/en/documents/tools-and-resources/moving-away-death-penalty-arguments-trends-and-perspectives> (inajadili DITSHWANELO dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Botswana, MISCRA Kesi Na. 2 ya mwaka 1999).

¹¹³Angalia Alice Mogwe, The Death Penalty in Botswana: Barriers to Equal Justice, in MOVING AWAY FROM THE DEATH PENALTY: ARGUMENTS, TRENDS AND PERSPECTIVES, 170, 174 (Ivan Simonovic ed., Sept. 21, 2015), <https://www.ohchr.org/en/documents/tools-and-resources/moving-away-death-penalty-arguments-trends-and-perspectives> (inajadili DITSHWANELO dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Botswana, MISCRA Kesi Na. 2 ya mwaka 1999).

¹¹⁴Jamhuri ya Botswana, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Apr. 21, 2020), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=10>.

mji mkuu, ikifanya iwe vigumu sana kwa washtakiwa walio nje ya mji mkuu kupata mawakili.¹¹⁵

* * *

64. Yaliyotajwa hapo juu yanaonyesha kuwa ukosefu wa mchakato unaostahili katika kesi za hukumu ya kifo ni tatizo kubwa, ambalo husababisha kukataliwa kwa mchakato unaostahili na kutolewa kwa adhabu ya kifo kiholela. Hasa, kushindwa kuhakikisha kwamba washtakiwa wa makosa yenye hukumu ya kifo wanawakilishwa vya kutosha kunamaanisha kwamba washtakiwa wawili wanaofanana ambao walifanya uhalifu unaofanana wanaweza kupata hukumu tofauti kabisa, yaani, mtu anaweza kuhukumiwa kifo na kunyongwa na mwingine asipewe hukumu hiyo, kulingana na endapo ana rasilimali za kutosha kudumu kuwa na wakili wake. Dhuluma kama hizo husababisha kukataliwa kwa mchakato unaostahili na kuondoa uhai kiholela kinyume cha Kifungu cha 4.

ii. Utoaji wa Adhabu ya Kifo Kibaguzi katika Uhalisia

65. Tatizo jingine la msingi la adhabu ya kifo ni kwamba inatolewa kwa njia ya kibaguzi, au kiholela, kati ya aina tofauti za watu. Kama mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu yalivyobainisha, adhabu ya kifo "hutumiwa kwa njia isiyo ya uwiano dhidi ya walio maskini, wachache na watu walio katika makundi ya rangi, kabila na dini fulani. Inatolewa na kutekelezwa kiholela...[na] kutumika kama chombo cha ukandamizaji – njia ya haraka na ya kikatili ya kunyamazisha upinzani wa kisiasa."¹¹⁶ Hasa, kama ilivyojadiliwa hapa chini, adhabu ya kifo hutolewa barani Afrika kwa njia ya kibaguzi kwa wanawake, watoto, watu wa makabila tofauti, wale wanaoishi katika hali ngumu ya kiuchumi, wale wanaozungumza lugha tofauti na walio wengi, na watu wa makundi fulani ya kisiasa. Utoaji huu

¹¹⁵ Actualités du projet Mali: La situation du Mali, AVOCATS SANS FRONTIERES FRANCE (imefikwa mara ya mwisho tarehe 24 Julai, 2010) (nakala inapatikana kwa kuomba).

¹¹⁶ Angalia Death Penalty, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 8: "Uzito wa adhabu ya kifo unachukuliwa kwa njia isiyolingana na wale walio na ushawishi mdogo wa kijamii na kiuchumi au walio wa mbari, kabila au dini ya watu walio wachache. Kwa mfano, hii ni pamoja na kuwa na ufikiaji mdogo wa uwakilishi wa kisheria, au kuathiriwa sana katika uzoefu wao wa mfumo wa haki ya jinai."

wa adhabu ya kifo kwa ubaguzi na kiholela unaonesha zaidi ni kwa jinsi gani adhabu ya kifo inakiuka Kifungu cha 4.

1. *Ubaguzi wa Kijinsia*

66. Ubaguzi wa kijinsia mara nyingi huchangia matumizi tofauti ya adhabu ya kifo kwa wanawake na wasichana. Wanawake wanaoshtakiwa kwa uhalifu wenye hukumu ya kifo mara nyingi wanakabiliwa na ubaguzi wa kimfumo, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa elimu, rasilimali za kiuchumi, au uwakilishi wa kisheria, na kufanya iwe "vigumu kwa wanawake kupata haki sawa na wanaume."¹¹⁷ Zaidi ya hayo, wanawake wanaposhtakiwa kwa uhalifu, mahakama mara nyingi hushindwa kutambua sababu za kupunguza hatari kama vile unyanyasaji wa nyumbani au ugonjwa wa akili.¹¹⁸
67. Ubaguzi wa kijinsia pia unawanyima wanawake kupata elimu, jambo linalofanya wawe katika hatari hasa ya kunyanyaswa na vyombo vya kutekeleza sheria na mfumo wa haki ya makosa ya jinai.¹¹⁹ Kwa sababu ya kutokuwa na fursa sawa ya kupata elimu, wanawake wanaweza kuwa hawaifahamu lugha ya mfumo wa kisheria, na hivyo kuwafanya washindwe kujaribu kujitetea.¹²⁰ Wanawake kwa ujumla pia mara nyingi wanakosa rasilimali za kiuchumi ikilinganishwa na wanaume, na wanaposhtakiwa kwa adhabu ya kifo wanaweza kuwa na uwezo mdogo wa kumudu huduma ya wakili.¹²¹ Kwa mfano, kati ya wanawake wanne waliohukumiwa kifo nchini Malawi kufikia mwaka 2018, wote walikuwa maskini, watatu hawakuwahi kwenda shule, na wawili hawakujua kusoma

¹¹⁷Angalia, kwa mfano, Judged for More Than Her Crime: A Global Overview of Women Facing the Death Penalty, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, ukurasa wa 3–4, 6–8, 15 (Sept. 2023) [hapa inarejelewa kama "Judged for More Than Her Crime"], <https://deathpenaltyworldwide.org/wp-content/uploads/2019/12/Judged-More-Than-Her-Crime.pdf>.

¹¹⁸ Angalia id.

¹¹⁹ Angalia id. ukurasa wa 29.

¹²⁰ Id. ukurasa wa 3; angalia Fati: An Innocent Woman Sentenced to Death for Terrorism After Being Falsely Accused by a Rejected Suitor, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Nov. 17, 2021), <https://deathpenaltyworldwide.org/publication/fati-an-innocent-woman-sentenced-to-death-for-terrorism-after-being-falsely-accused-by-a-rejected-suitor/?version=html> (ambapo Fati, mwanamke wa Kikameruni ambaye hakuzungumza Kifaransa, hakupewa mtafsiri licha ya kushtakiwa kwa ugaidi na kufungwa).

¹²¹ Angalia Judged for More Than Her Crime ukurasa wa 8, 18 (ikionyesha kwamba wanawake mara nyingi hukosa pesa au mali zao wenyewe, na kwamba idadi kubwa ya wanawake wanaohukumiwa kifo wanatoka katika jamii maskini na zilizotengwa, na kuzuia uwezo wao wa kupata wakili anayefaa).

na kuandika.¹²² Kutokuwa na uwezo wa kuelewa mchakato na kujihusisha kwa kina, au hata kuweza kumudu huduma ya wakili mara nyingi husababisha kushindwa kujitetea vya kutosha na kuhakikisha kesi inasikilizwa kwa haki.¹²³

68. Aidha, vyombo vya kutekeleza sheria na waendesha mashtaka mara nyingi hushindwa kutambua sababu za kupunguza hatari ambazo huathiri wanawake hasa, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa nyumbani au ugonjwa wa akili.¹²⁴ Kwa mfano, kufikia mwaka 2018, wanawake wote waliohukumiwa kifo nchini Malawi "walikuwa wamepata aina mbalimbali za ukandamizaji wa kijinsia na aina fulani ya ugonjwa wa akili au kiwewe."¹²⁵ Zaidia ya hayo, mwanamke mmoja nchini Malawi alishtakiwa kwa kosa la mauaji mnamo mwaka 2003 baada ya kumpiga mumewe mnyanyasaji kwa hali ya kujilinda.¹²⁶
69. Tatizo hili linaendelea katika kuwahukumu wanawake, ambapo mahakama mara nyingi hupuuza athari za unyanyasaji wa kijinsia, ukatili, na kiwewe kama sababu za kupunguza hukumu.¹²⁷ Wanawake waliohukumiwa kifo mara nyingi walikuwa waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia, jambo ambalo mara kwa mara hupuuza au kudharauliwa wakati wa kuzingatia mazingira ambayo yalisababisha uhalifu wao.¹²⁸ Kama mfano mmoja tu, katika kesi ya hivi karibuni nchini Tanzania, mahakama ya iliyosikiliza kesi ilishindwa kuzingatia ushahidi wa kupunguza adhabu wa utetezi binafsi wa mshtakiwa wa kike kwa kumhukumu kifo kwa kumuua "mumewe mnyanyasaji," ikiwa ni pamoja na ushahidi wake usiopingwa kwamba alikuwa amemshambulia kikatili na kumpiga kwa

¹²² Angalia id. ukurasa wa 29.

¹²³ Angalia id.

¹²⁴ Angalia id. ukurasa wa 12, 15–17.

¹²⁵ Angalia id. ukurasa wa 29.

¹²⁶ Angalia id. ukurasa wa 30.

¹²⁷ Angalia, kwa mfano, Sally Parker, Center on the Death Penalty Worldwide Wins Freedom for Two Women in Tanzania, CORNELL L. SCH. (Machi 13, 2024), <https://www.lawschool.cornell.edu/news/center-on-the-death-penalty-worldwide-wins-freedom-for-two-women-in-tanzania/> (ambapo mume wa mwanamke Mtanzania alikuwa amesababisha vurugu za mara kwa mara na za kikatili kwa mkewe na watoto wake, na hali hii haikuzingatiwa katika hukumu yake ya kumuua mumewe katika kujitetea).

¹²⁸ Angalia, kwa mfano, id.; angalia pia Judged for More Than Her Crime ukurasa wa 15–16, 29–30.

nyundo alipokuwa amelewa kabla ya kumnyang'anya nyondo hiyo na kumuua.¹²⁹

70. Ubaguzi wa kimfumo uliotajwa hapo juu unaokabiliwa na wanawake wanaoshtakiwa kwa uhalifu wa adhabu ya kifo, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa elimu, rasilimali za kiuchumi, na uwakilishi wa kisheria, pamoja na kushindwa kwa watekelezaji wa sheria, waendesha mashtaka, na mahakama kushindwa kuangalia vizuri sababu za kupunguza hukumu kama vile unyanyasaji wa nyumbani na ugonjwa wa akili katika kesi za adhabu ya kifo kwa wanawake, husababisha hali ya ukatii wa kijinsia katika utoaji wa adhabu ya kifo katika uhalisia.

2. Watoto

71. Kuna marufuku dhahiri na majumui kuhusu kuwahukumu watoto kifo, kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto, vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu, na sheria za kila Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika. Hata hivyo, watoto barani Afrika wanaendelea kuhukumiwa kifo. Utoaji wa adhabu ya kifo kwa watoto unaendelea kwa sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na kwamba Nchi zinapuuza sheria zinazokataza, umri wa walio wachache ni tofauti katika sheria ya Nchi kuliko umri katika vyombo vya kisheria vya kimataifa, na ukosefu wa kumbukumbu za umri kimaandishi.
72. Kati ya mwaka 1990 na 2019, Amnesty International ilirekodi visa vya watoto waliouawa katika nchi tano za Afrika: Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Nigeria, Somalia, Sudan Kusini, na Sudan.¹³⁰ Mnamo mwaka 2015, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliripoti kwamba Nigeria iliwahukumu adhabu ya kifo watoto wenye makosa katika miaka ya hivi

¹²⁹ Chausiku Nchama Magoiga dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya Jinai Na. 297 ya 2020, Hukumu, Ct. ya Rufaa ya Tanzania, ukurasa wa 5 (Novemba 9, 2023). Angalia pia id. ukurasa wa 9–11 (ikielezea zaidi shambulio la mume kwa mshtakiwa na kubatilisha hatia yake kwa sababu ya kosa la mahakama iliyosikiliza kesi kutozingatia mazingira yanayohusiana na kosa hilo).

¹³⁰ Executions of Juveniles Since 1990 as of November 2019, AMNESTY INT'L (Nov. 2019), <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/0233/2019/en/>; Somalia: Five Children Executed, Two Others at Risk, AMNESTY INT'L (Apr. 28, 2017), <https://www.amnesty.org/en/documents/afr52/6112/2017/en/>.

karibuni.¹³¹ Katika baadhi ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, kuendelea kutolewa kwa adhabu ya kifo kwa watoto kunaweza kutokana na ukweli kwamba fasili ya nchi fulani kuhusu "watoto" haikubaliani na fasili ya neno hilo katika vyombo vya kisheria vya kimataifa. Mkataba wa Haki za Mtoto ("CRC"), ambao umetiwa saini na kuridhiwa na kila Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika,¹³² unafasili "watoto" kumaanisha watu walio chini ya umri wa miaka 18,¹³³ lakini baadhi ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zimechagua umri wa chini ya miaka 18 kama hatua ambayo mtu hachukuliwi tena kuwa mtoto na anaweza kutendewa kama mtu mzima kwa madhumuni ya hukumu ya jinai.¹³⁴

73. Zaidi ya hayo, watoto wako katika hatari ya kuhukumiwa kama watu wazima katika kesi za adhabu ya kifo wanapokosa nyaraka za tarehe yao ya kuzaliwa. Mtoto anapokuwa hawezi kuthibitisha umri wake, yuko katika hatari ya kuhukumiwa kama mtu mzima na kuhukumiwa kifo wakati kesi yake vinginevyo haistahiki adhabu ya kifo. Suala hili limeenea hasa ambapo kuna viwango vya chini vya usajili wa vyeti vya kuzaliwa.¹³⁵ Barani Afrika, Nchi nyingi Wanachama wa Umoja wa Afrika zinazoendelea kutumia adhabu ya kifo hazina rejista za tarehe za kuzaliwa zinazofanya kazi.¹³⁶
74. Sababu moja ya ziada inayosababisha kuwa na utambulisho usio sahihi, na kuhukumiwa kifo kwa wahalifu wa watoto ni muda mrefu ambao

¹³¹ Angalia Adhabu ya Kifo na Utekelezaji wa Kanuni Zilizowekwa ili Kuhakikisha Ulinzi wa Haki za Wale Wanaokabiliwa na Adhabu ya Kifo, Baraza la Uchumi na Kijamii Res. 2015/49, ¶ 79 (Aprili 13, 2015).

¹³² Angalia Ratification Status for CRC - Convention on the Rights of the Child, UNITED NATIONS TREATY BODY DATABASE, https://treaties.un.org/Pages/ViewDetails.aspx?src=TREATY&mtdsg_no=IV.11&chapter=4&clang=en.

¹³³ Mkataba wa Haki za Mtoto, UN.T.S., Na. 27531, kifungu cha 1 (Novemba 20, 1989) (ulianza kutumika Septemba 2, 1990).

¹³⁴ Angalia Minimum Ages of Criminal Responsibility in Africa, CHILD RIGHTS INTERNATIONAL NETWORK (CRIN) (Okt. 17, 2014), <https://archive.crin.org/en/home/ages/Africa.html>.

¹³⁵ Angalia S. L. Babcock, Deciding who lives and who dies: eligibility for capital punishment under national and international law, in COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT (Ed. Carol S. Steiker na Jordan M. Steiker), ukurasa 56–58 (2019).

¹³⁶ Katika nchi nyingi zinazoendelea kutumia sheria ya kifo chini ya asilimia 50 ya idadi ya watu walio chini ya umri wa miaka mitano wana cheti cha kuzaliwa. Yaani, tunarejelea Somalia (asilimia 3) na Sudan Kusini (asilimia 35). Angalia Birth Registration, UNICEF GLOBAL DATABASE, <https://data.unicef.org/topic/child-protection/birth-registration/#data> (last update: Juni 2023).

watuhumiwa wanatumia wakiwa kizuizini kabla ya kufikishwa mahakamani.¹³⁷ Katika nchi kadhaa za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wale wanaoshtakiwa kwa uhalifu wanaweza kubaki kizuizini kwa miaka kadhaa bila kuonana na wakili.¹³⁸ Wakati wanaonakana mahakamani, mara nyingi huwa wamezidi umri wa walio wengi, na mawakili wao kwa kawaida hawaoni kuwa ni muhimu wakati huo kuthibitisha umri wao wakati uhalifu ulipotendeka.¹³⁹

75. Kwa jumla, licha ya ukweli kwamba utoaji wa adhabu ya kifo kwa watoto umelaaniwa na kupigwa marufuku ulimwenguni kote kama kanuni ya msingi ya haki za binadamu, maadamu adhabu ya kifo ni chaguo la adhabu barani Afrika, kuna hatari inayoendelea na uwezekano kwamba watoto watakuwa katika hatari ya kuhukumiwa kifo na kunyongwa.

3. *Ulemavu wa Akili*

76. Wale wanaosumbuliwa na ulemavu wa kiakili au kisaikolojia na kijamii wako katika hatari kubwa ya kunyongwa kimakosa na kupitia mchakato wa makosa ya uhalifu usio wa haki kwa ujumla ikilinganishwa na watu wasio na hali kama hizo. Inatambuliwa sana kwamba kutoa adhabu ya kifo kwa watu wenye ulemavu wa akili ni kinyume cha kanuni za haki za binadamu. Hakika, Tume ya Afrika imesema waziwazi kwamba "... unyongaji wa...watu wenye ulemavu wa kisaikolojia na kijamii au kiakili, daima utachukuliwa kuwa ukiukaji wa haki ya kuishi."¹⁴⁰ Aidha, mashirika kadhaa ya Umoja wa Mataifa yamehimiza Mataifa yawaondoe kabisa watu wenye ulemavu wa akili kwenye adhabu ya kifo: Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu katika Azimio Na. 2005/59 ilitoa wito kwa Mataifa yasitoe hukumu ya kifo au kumnyonga "mtu anayesumbuliwa na

¹³⁷ Angalia S. L. Babcock, Deciding who lives and who dies: eligibility for capital punishment under national and international law, in COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT (Ed. Carol S. Steiker na Jordan M. Steiker), ukurasa wa 58, n.27. (2019).

¹³⁸ Id.

¹³⁹ Id.

¹⁴⁰Maoni ya Jumla Na. 3 Kuhusu Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu: Haki ya Kuishi (Kifungu cha 4), Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Comm'n H.P.R.], § D.25 (Des. 12, 2015), <https://www.refworld.org/legal/general/achpr/2015/en/70896>.

ulemavu wowote wa akili¹⁴¹; Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso mwaka 2014 alisema kuwa "sheria ya kimataifa inachukulia utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa watu wenye ulemavu wa akili kuwa ni ukiukaji wa marufuku ya mateso na adhabu nyingine za kikatili, za kinyama na za kudhalilisha"¹⁴²; Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu imepitisha maazimio ya kuhimiza mataifa yote yasimnyonge mtu yeyote"anayesumbuliwa na aina yoyote ya ugonjwa wa akili"¹⁴³; na hivi karibuni, azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la kuunga mkono marufuku ya adhabu ya kifo linahimiza mataifa "yaendeleo kuzuia matumizi ya adhabu ya kifo na si kutoa adhabu ya kifo...."kwa watu wenye ulemavu wa akili".¹⁴⁴ Aidha, Mahakama hii hapo awali ilitambua kwamba kushindwa kuzingatia ushahidi wa hali ya afya ya akili ya mshtakiwa kunaweza kusababisha ukiukaji wa haki ya mshtakiwa ya kusikilizwa kwa haki chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba na, katika muktadha wa adhabu ya kifo ya lazima, kwamba kushindwa huko ni ukiukaji wa haki ya kuishi kama ilivyohakikishwa na Kifungu cha 4 cha Mkataba.¹⁴⁵

77. Ulinzi dhidi ya utoaji wa adhabu ya kifo kwa watu wenye ulemavu wa akili ni tatizo hasa barani Afrika, kwa kuzingatia ukosefu wa rasilimali muhimu za kuwatambua wahalifu wenye ulemavu kama huo na kuzingatia ipasavyo hali yao kama sababu ya kupunguza uzito wa hukumu.

¹⁴¹ Angalia, kwa mfano, Maazimio ya Tume ya Haki za Binadamu 2005/59: Question of the Death Penalty, UN Commission on Human Rights (Apr. 20, 2005).

¹⁴² Taarifa kwa Vyombo vya Habari, Death row: UN experts urge US authorities to stop execution of Scott Panetti, a mentally ill prisoner, U.N. Press Release (Des. 02, 2014), <https://www.ohchr.org/en/press-releases/2014/12/death-row-un-experts-urge-us-authorities-stop-execution-scott-panetti>.

¹⁴³ The Question of the Death Penalty, E/CN.4/RES/2003/67, U.N. HUM. RTS. OFFICE HIGH COMM'R, ¶ 4(g) (Apr. 25, 2003).

¹⁴⁴ Azimio Na. 77/222 la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Kusitisha kwa muda matumizi ya adhabu ya kifo, A/Res/77/222, ¶ 7(e) (Januari 6, 2023).

¹⁴⁵ Angalia Gozbert Henerico dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 056/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 160 (Januari 10, 2022) (kutafuta ukiukaji wa Kifungu cha 7(1) kwa sababu ya mahakama ya ndani kushindwa kuzingatia ripoti ya tathmini ya matibabu ya hali ya afya ya akili ya Mleta Maombi). Angalia pia Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 214–15 (Septemba 3, 2024) (kutafuta ukiukaji wa Kifungu cha 4 "kwa sababu ya mahakama za ndani kutopewa uhuru wa kuzingatia afya ya akili ya Waleta Maombi katika kutoa hukumu ya kifo").

78. Hata katika nchi ambazo wale walio na magonjwa ya akili au ulemavu wa akili wana msamaha wa adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria, na hata wakati kipimo kinachotumika kuamua ni nani anayeugua ugonjwa huo wa akili au mwenye ulemavu wa akili kinajitosheleza na hakiondoi makundi fulani ya watu wenye ulemavu wa akili, washtakiwa ambao wanaangukia katika kundi hili bado wanaweza kuhukumiwa kifo kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu wenye mafunzo ambao wana sifa za kufanya uchunguzi unaohitajika.¹⁴⁶ Kwa mfano, utafiti nchini Malawi, uligundua kuwa wafanyakazi wachache wa afya ya akili wamefundishwa kufanya tathmini kamili ya washtakiwa wa mauaji walio katika hukumu ya kifo ili kubaini ikiwa walipata ulemavu wa akili ambao unaweza kutumika kama sababu za kupunguza hukumu.¹⁴⁷ Kwa kweli, ingawa zaidi ya watu mia mbili walihukumiwa kifo nchini Malawi kati ya mwaka 1994 na 2005, hakuna hata mmoja aliyepimwa ulemavu wa akili kabla ya kusikiliza kesi.¹⁴⁸
79. Katika hali nyingine, mahakama inapuuzia tu ushahidi wa ulemavu wa akili wa mshtakiwa kama sababu inayoweza kupunguza hukumu. Kwa mfano, kama Mahakama hii ilivyobainisha katika kesi ya Gozbert Henerico dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania¹⁴⁹, Mahakama Kuu ya Tanzania mjini Bukoba ilishindwa kuzingatia ripoti ya matibabu kuhusu hali ya afya ya akili ya Bw. Henerico na ikamhukumu kifo, jambo ambalo lilifanya kuwepo ukiukaji wa haki ya kusikilizwa kwa haki.¹⁵⁰
80. Kama ilivyoonyeshwa na yaliyotajwa hapo juu, mifumo ya haki ya makosa ya jinai barani Afrika haiwezi kuhakikisha kuwa hali ya afya ya akili ya

¹⁴⁶ Angalia S. L. Babcock, Deciding who lives and who dies: eligibility for capital punishment under national and international law, in *COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT* (Ed. Carol S. Steiker na Jordan M. Steiker), ukurasa wa 58–66 (2019); Justice Denied: A Global Study of Wrongful Death Convictions, ukurasa wa 6, 37 (Jan. 2018).

¹⁴⁷ Angalia Justice Denied: A Global Study of Wrongful Death Convictions, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, ukurasa wa 37 (Januari 2018).

¹⁴⁸ S. L. Babcock, Deciding who lives and who dies: eligibility for capital punishment under national and international law, in *COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT* (Ed. Carol S. Steiker na Jordan M. Steiker), ukurasa wa 65 (2019). Wakati unyongaji wa mara ya mwisho unaojulikana nchini Malawi ulifanyika mwaka 1992, rekodi ya hukumu za kifo kutolewa bila tathmini ya kutosha ya ulemavu wa akili inaonyesha kuenea kwa tatizo hili.

¹⁴⁹ Gozbert Henerico dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 056/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.] (Januari 10, 2022).

¹⁵⁰ Id. ¶ 160; angalia pia Mkataba wa Afrika, Kifungu cha 7(1).

mshtakiwa inatathminiwa, au hata kuzingatiwa, kabla ya kumhukumu kifo, na kusababisha hatari kubwa kwamba watu wanaosumbuliwa na ugonjwa wa akili au ulemavu wa akili wanauawa kwa njia isiyo ya haki.

4. *Umaskini*

81. Adhabu ya kifo pia mara nyingi hutolewa kwa njia isiyo ya uwiano kwa wale wanaoishi katika umaskini. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wamesema kwamba, kwa ujumla:

"ikiwa wewe ni maskini, uwezekano wa kuhukumiwa kifo ni mkubwa zaidi kuliko ikiwa wewe ni tajiri. Hakuwezi kuwa na mashtaka makubwa ya adhabu ya kifo kuliko ukweli kwamba kimsingi ni adhabu iliyowekwa kwa ajili ya watu wanaotoka katika makundi ya hadi ya chini kijamii na kiuchumi. Hali hii inafanya uwe ubaguzi wa kitabaka katika nchi nyingi, na hivyo kufanya kuwa sawa na mauaji ya kiholela."¹⁵¹

Hali kadhaa zinawafanya wale wanaoishi katika umaskini wawe na uwezekano mkubwa wa kukabiliwa na adhabu ya kifo na hatimaye kuhukumiwa kifo, ikiwa ni pamoja na: (1) vizuizi vya kinfumo, kama vile gharama za uendeshaji kesi au kukosekana kwa taasisi muhimu katika maeneo ya vijijini au yenye umasikini, mambo ambayo huwazuia watu kama hao kutumia haki zao za kusikilizwa kwa haki; (2) dhana zinazohusiana na umaskini na uhalifu; (3) ukosefu wa upatikanaji wa elimu, msaada wa kijamii au kifedha unaohitajika ili kuendesha kesi ngumu za jinai; (4) ukosefu wa uwakilishi mzuri wa kisheria, ambao unasababisha uwezekano mkubwa wa uendeshaji kesi isivyo haki; na (5) kunyimwa haki za rufaa. Kila moja imefupishwa hapa chini.

82. Kwanza, vizuizi vya kinfumo vya kufikia mfumo wa haki vinaathiri kwa kiasi kikubwa wale wanaoishi katika hali ya umaskini, na kusababisha

¹⁵¹ Taarifa ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa; angalia pia Ripoti ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, majadiliano ya jopo la ngazi ya juu kuhusu suala la adhabu ya kifo, A/HRC/42/25, ¶ 5 (Juni 21, 2019), https://ap.ohchr.org/documents/dpage_e.aspx?si=A/HRC/42/25.

matokeo mabaya katika kesi za jinai na athari kubwa ya adhabu ya kifo kwa kundi hili.¹⁵² Kushindwa kwa mshtakiwa kumudu gharama za kesi za jinai ni kikwazo kimojawapo. Kuanzia uchunguzi wa awali hadi kunyongwa, utajiri na mapato huathiri kila hatua ya mchakato wa makosa ya uhalifu, ikiwa ni pamoja na mchakato wa adhabu ya kifo, kwani washtakiwa wanakabiliwa na ada na gharama zingine katika hatua zote za kesi. Kwa mfano, wakati wa mchakato wa uchunguzi, watu masikini wanaweza kuathiriwa katika hali ambapo malipo (au rushwa) yanaweza kuathiri kina cha uchunguzi.¹⁵³ Kwa mfano, nchini Nigeria, watuhumiwa wanaweza kuhitajika kulipia mafuta ya polisi wanaposafiri kuwaona na kuwahoji mashahidi, ikiwa ni pamoja na mashahidi ambao wanaweza kuthibitisha kutokuwepo kwenye eneo la tukio kwa watuhumiwa wanaokabiliwa na adhabu ya kifo kwa makosa yao ya uhalifu.¹⁵⁴ Kuna kesi mazingira ambapo polisi hawakufanya mahojiano haya kwa sababu watuhumiwa wanaokabiliwa na adhabu ya kifo hawakuweza kulipa, pamoja na mazingira ambapo watuhumiwa walihukumiwa kifo baadaye.¹⁵⁵

83. Aidha, maeneo ya vijijini, masikini, na yaliyotengwa mara nyingi hukosa taasisi zinazohitajika au utoaji wa haki, kama vile maafisa wa polisi, mawakili, majaji, na mahakama.¹⁵⁶ Katika hali kama hizo, wale "wanaoishi katika umaskini wanapaswa kusafiri umbali mrefu kwa gharama kubwa ili kupata mfumo wa utoaji haki."¹⁵⁷ Kwa mfano, nchini Malawi, ukosefu wa rasilimali unamaanisha kuwa "uchunguzi wa historia ya mhalifu ni nadra kufanyika kwa sababu ya ukweli kwamba washtakiwa huenda wakawa wanaishi katika vijiji vya mbali ambavyo havifikiki kutokana na kukosekana kwa rasilimali. [...] Gharama za kusafiri pia ni kubwa sana kuleta mashahidi

¹⁵² Angalia Ripoti ya Mwandishi Maalumu kuhusu umaskini uliokithiri na haki za binadamu, Umaskini uliokithiri na haki za binadamu, A/67/278, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ¶¶ 35–59 (Agosti 9, 2012) [hapa inarejelewa "Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Umaskini"].

¹⁵³ Angalia Nigeria. Waiting for the Hangman, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 3 (Okt. 2008) [hapa inarejelewa kama "Ripoti ya AI kuhusu Nigeria"], <https://www.amnesty.org/en/documents/afr44/020/2008/en/>. Nigeria ni nchi inayoendelea kutumia adhabu ya kifo. Death Sentences and Executions in 2022, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 41 (Mei 16, 2023), <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/6548/2023/en/>.

¹⁵⁴ Angalia Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 3.

¹⁵⁵ Id, ukurasa wa 3, 13–14.

¹⁵⁶ Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Umaskini, ¶ 37.

¹⁵⁷ Id.

wa kesi za mauaji."¹⁵⁸ Matokeo yake, mara nyingi, shahidi pekee wa utetezi ni mshtakiwa mwenyewe.¹⁵⁹

84. *Pili*, watu wanaoishi katika umaskini mara nyingi hulengwa kama watuhumiwa wa uhalifu: "idadi kubwa kwa kiasi fulani ya [watu wanaoishi katika umaskini] wanakamatwa, wanawekwa kizuizini na kufungwa kwa sababu watekelezaji wa sheria mara kwa mara wanatumia umasikini, kutokuwa na makazi au mazingira magumu kuwa kiashiria cha uhalifu."¹⁶⁰ Katika suala hili, ripoti ya Tume ya Rais ya Marekebisho ya Utawala wa Sheria ya Nigeria ilihitimisha kwamba "ulinzi mdogo wa kisheria [na] upatikanaji usio sawa wa haki huendeleza hali ambayo masikini na makundi mengine ya watu walio katika mazingira magumu wanaweza kukamatwa na baadaye kufungwa."¹⁶¹ Athari za jambo hili la "uhalifu wa umaskin" pia zilizingatiwa katika muktadha wa adhabu ya kifo. Kulingana na ripoti hiyo hiyo, wafungwa waliohukumiwa kifo nchini Nigeria "ni maskini tu na hawana uwakilishi wa kisheria."¹⁶²

85. *Tatu*, washtakiwa masikini pia mara nyingi wanakosa fursa ya kupata elimu na wananyimwa msaada unaohitajika wa kijamii, kifedha, na kisheria ili kupitia mchakato mgumu wa kesi ya adhabu ya kifo. Kwa kukosekana kwa elimu na msaada kama huo, mara nyingi hawawezi kuelewa au kushiriki kikamilifu katika kesi na kujitetea kwa ufanisi.¹⁶³ Kwa mfano, utafiti nchini Kenya uliohusisha wafungwa 671 katika magereza 12 ambao walikuwa wamehukumiwa kifo ulionyesha hali mabaya sana ya kielimu na kiuchumi: wastani wa kipato chao kabla ya kukamatwa ulikuwa chini ya kipato cha kuendesha maisha nchini Kenya na zaidi ya asilimia 10

¹⁵⁸ Ripoti ya Kikao cha 56 cha Kawaida cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kwa ajili ya Uchunguzi wa Tume kuhusu Ripoti ya Awali na Jumuishi ya Nchi ya Malawi kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu nchini Malawi, WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU, ukurasa wa 10 (Septemba 2014) [hapa inrejelewa "Ripoti kuhusu Malawi ya WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU"].

¹⁵⁹ Angalia Ripoti kuhusu Malawi ya WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU, ukurasa wa 10.

¹⁶⁰ Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Umaskini, ¶ 48 (msisitizo umeongezwa).

¹⁶¹ Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 37.

¹⁶² Id.

¹⁶³ Death Penalty and Poverty Factsheet, WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY, ukurasa wa 4, https://worldcoalition.org/wp-content/uploads/2020/09/EN_WD2017_FactSheet-1.pdf (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 8, 2024).

hawakuwahi kupata elimu rasmi.¹⁶⁴ Aidha, zaidi ya theluthi mbili walikuwa wamemaliza elimu ya msingi tu, na karibu nusu hawakuendelea zaidi ya darasa la 4.¹⁶⁵ Chini ya asilimia 2 walikuwa wamepata elimu ya chuo kikuu.¹⁶⁶ Kwa kuzingatia sababu hizi, haishangazi kwamba Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu ya Kenya ilitaja umaskini na elimu duni kati ya sababu za msingi zinazochangia ukosefu wa uendeshaji kesi kwa haki kwa wafungwa wengi wanaohukumiwa kifo.¹⁶⁷

86. *Nne*, mara tu mtu anapotambuliwa kama mtuhumiwa, umaskini unaendelea kuathiri kesi yake kwa sababu utetezi wa kisheria wenye ufanisi mara nyingi huhitaji rasilimali kubwa. Kwa hivyo, watu masikini wanakabiliwa na kutendewa isivyo haki katika mchakato wote wa kesi, pamoja na katika kesi za adhabu ya kifo, kwa sababu ya ukosefu wao wa rasilimali. Hii ni kweli hasa katika nchi ambazo haki ya kupata wakili haijahakikishiwa kwa washtakiwa wote wa hukumu ya kifo, ama chini ya sheria au kivitendo. Kwa mfano, Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Nigeria inasema (i) kwamba mahakama "zinaweza" kutoa msaada wa kisheria katika kesi mbaya za jinai lakini (ii) msaada wa kisheria hautolewi kwa wizi wa kutumia silaha, kosa lenye adhabu ya kifo ya lazima.¹⁶⁸ Na kama ilivyojadiliwa kwa undani zaidi hapo juu katika ¶ 58-61, supra, mipango ya msaada wa kisheria katika Nchi nyingi zinazoendelea kutoa adhabu ya kifo inaelemewa na kufadhiliwa pesa pungufu, na kufanya iwe changamoto sana kwa wafungwa masikini wanakabiliwa na adhabu ya kifo kupata mawakili wa kuwawakilisha kwa ufanisi au wasipate kabisa.¹⁶⁹

¹⁶⁴ Living With a Death Sentence in Kenya: Prisoners' Experiences of Crime, Punishment and Death Row, The Death Penalty Project, ukurasa wa 26, 29 (2022), <https://deathpenaltyproject.org/wp-content/uploads/2022/12/Living-with-a-Death-Sentence-in-Kenya-Prisoners-Experiences-of-Crime-Punishment-and-Death-Row.pdf>.

¹⁶⁵ *Id.* ukurasa wa 26.

¹⁶⁶ *Id.*

¹⁶⁷ Ripoti ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, supra n.106 ukurasa wa ¶ 17

¹⁶⁸ Justice Denied: A Global Study of Wrongful Death Convictions, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, ukurasa wa 44 (Jan. 2018), <https://www.deathpenaltyworldwide.org/wp-content/uploads/2019/12/Justice-Denied-A-Global-Study-of-Wrongful-Death-Row-Convictions.pdf>.

¹⁶⁹ Ripoti ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Question of the death penalty, A/HRC/51/7, U.N. HUM. RTS. OFFICE HIGH COMM'R, ¶ 37-40 (Julai 26, 2022), <https://worldcoalition.org/document/a-hrc-51-7-advance-edited-version-question-of-the-death-penalty/> (ikinukuu Azimio la Pamoja la Katibu Mkuu na Mwakilishi Mkuu wa Umoja wa Ulaya katika Siku ya Ulimwengu na Ulaya Dhidi ya Adhabu ya Kifo, [https://www.coe.int/en/web/portal/-/world-day-against-](https://www.coe.int/en/web/portal/-/world-day-against-47)

87. Zaidi ya hayo, wafungwa wengi waliowekwa kizuizini katika nchi zinazotoa adhabu ya kifo, ikiwa ni pamoja na wafungwa wengi masikini, wanalazimika kusubiri miaka mingi hadi kesi zao zihitimishwe au hata kupangiwa siku nyingine kwa sababu, pamoja na mambo mengine, mfumo wa mahakama umezidiwa kwa kutokuwa na rasilimali na idadi ndogo ya wanasheria walioteuliwa na serikali.¹⁷⁰ Ucheleweshaji huu hausababishi tu watu wasio na hatia kulazimishwa kukaa miaka mingi gerezani kabla ya kesi yao kusikilizwa, lakini pia unaweza kusababisha uharibifu wa ushahidi au kupoteza mashahidi. Mambo haya "yana athari kubwa kwa masikini, ambao kwao mchakato wa muda mrefu si tu kunawanyima haki lakini pia hawawezi kumudu gharama na kufaya hali yao kuwa mbaya zaidi."¹⁷¹ Aidha, kesi za watu masikini "hazipewi kipaumbele kwa sababu ya kutenda kwa kuwapendelea matajiri au kukosa kujali au kuelewa athari za ucheleweshaji" kwao.¹⁷²
88. Kwa mfano, wafungwa wengi nchini Nigeria, wanasubiri angalau miaka miwili, na wakati mwingine zaidi ya miaka saba ili kesi zao zihitimishwe.¹⁷³ Takriban wanaume wanne kati ya kumi waliohukumiwa kifo nchini Nigeria walisubiri kesi zao zisikilizwe kwa zaidi ya miaka mitano, wakati wengi walisubiri miaka sita, saba au nane.¹⁷⁴ Mtu mmoja nchini Nigeria alikaa gerezani kwa miaka 16 kabla ya kuhukumiwa kifo.¹⁷⁵
89. Tano, ugumu mahususi wanaoukabili washtakiwa masikini au fukara katika kesi za adhabu ya kifo haziishii katika mahakama ya kusikiliza kesi. Ingawa haki ya kukata rufaa imehakikishwa na Mkataba wa Afrika na

the-death-penalty-10-october-2020-joint-declaration-by-eu-high-representative-and-council-of-europe-secretary-general);

angalia pia Maoni ya Jumla Na. 36 kuhusu Kifungu cha 6: Right to Life, CCPR/C/GC/36, U.N. HUM. RTS. COMM., ¶ 41 (Septemba 3, 2019), <https://www.ohchr.org/en/calls-for-input/general-comment-no-36-article-6-right-life#:~:text=The%20right%20to%20life%20is,the%20life%20of%20the%20n>

¹⁷⁰Angalia Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Umaskini, ¶ 68.

¹⁷¹ Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Umaskini, ¶ 69.

¹⁷² Id.

¹⁷³ Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 15.

¹⁷⁴ Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 15.

¹⁷⁵ Id. Ucheleweshaji huo wa muda mrefu pia ni wa kawaida katika mchakato wa rufaa nchini Nigeria, kwani kipindi cha wastani cha mfungwa kukaa gerezani akisubiri kunyongwa ni kati ya miaka 10 hadi 15. Id. ukurasa wa 25.

ICCPR, washtakiwa¹⁷⁶ masikini au fukara wanaweza kuzuiwa kutumia haki zao za rufaa kwa sababu ya ukosefu wao wa rasilimali.¹⁷⁷ Kwa mfano, Ripoti ya Amnesty International Nigeria ilibaini kwamba "wafungwa wanne kati ya 10 waliohukumiwa kifo hawakuwahi kukata rufaa, ama kwa sababu walinyimwa haki yao ya kukata rufaa au kwa sababu hawakuwa na pesa za ada ya mahakama na kumlipa wakili."¹⁷⁸ Nchini Malawi, ingawa washtakiwa wote wanaoshtakiwa kwa mauaji wanaweza kupata msaada wa kisheria bila malipo katika ngazi ya mahakama ya kusikiliza kesi, "uwakilishi wa kisheria hautolewi mara kwa mara kwa wafungwa wanaotaka kukata rufaa dhidi ya hukumu zao za kifo."¹⁷⁹ Utafiti uliofanywa mwaka 2014 ulikadiria kuwa ni nusu tu ya wafungwa 200 waliohukumiwa kifo nchini Malawi kati ya mwaka 1994 na 2007 ndio waliweza kutumia haki yao kukata rufaa dhidi ya hukumu zao za kifo.¹⁸⁰ Ukosefu wa fedha za kufuatilia mchakato mrefu wa kukata rufaa unamaanisha wafungwa fukara wanashindwa kutumia haki yao ya kukata rufaa na kwa hivyo wanabaki gerezani wakisubiri kunyongwa.¹⁸¹

90. Kila moja ya sababu hizi inamaanisha wale wanaoishi katika umaskini mara nyingi wananyimwa ufikiaji kamili wa rasilimali muhimu kwa ajili ya kuhukumu kwa haki. Kwa kutozipata, watu wanaoishi katika umaskini wanakabiliwa na uwezekano mkubwa wa kuhukumiwa kimakosa.¹⁸² Wakati adhabu ya kifo ni adhabu inayoweza kutolewa katika hali kama hizo, matokeo yake ni ukiukaji wa ulinzi wa mchakato unaostahili na

¹⁷⁶ Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, Kifungu cha 7(1)(a) (kinachotoa haki ya mtu binafsi kusikilizwa kesi yake, ikiwa ni pamoja na "haki ya kukata rufaa kwa vyombo vya kitaifa vyenye uwezo dhidi ya vitendo vya kukiuka haki zao za msingi"); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, U.N.T.S 171, juzuu ya 999, kifungu cha 14(5) (Desemba 19, 1966) (ukionyesha kwamba "kila mtu aliyekutwa na hatia ya uhalifu atakuwa na haki ya kuthibitishwa hatia yake na kuhukumiwa na mahakama ya juu kwa mujibu wa sheria").

¹⁷⁷ Angalia S. L. Babcock, *An Unfair Fight for Justice: Legal Representation of Persons Facing the Death Penalty*, in *COMPARATIVE CAPITAL PUNISHMENT* (Ed. Carol S. Steiker na Jordan M. Steiker), ukurasa wa 99 (2019) (ikizingatiwa kuwa kote Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, wafungwa waliohukumiwa kifo lazima wakate rufaa vinginevyo wanapoteza haki yao ya kukata rufaa).

¹⁷⁸ Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 21.

¹⁷⁹ Ripoti kuhusu Malawi ya WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU, ukurasa wa 11.

¹⁸⁰ Id.

¹⁸¹ Angalia Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 21 (ikibainisha kwamba hofu ya mchakato wa rufaa uliocheleweshwa sana au wa muda mrefu pia huwazuia baadhi ya wafungwa wanaosubiri kunyongwa nchini Nigeria kukata rufaa).

¹⁸² Angalia Ripoti ya AI kuhusu Nigeria, ukurasa wa 15 na kuendelea.

marufuku ya kuondoa uhai kiholela ambayo imehakikishwa katika Kifungu cha 4 cha Mkataba.

5. *Lugha*

91. Vikwazo vya lugha pia vina sehemu kubwa katika matumizi holela ya adhabu ya kifo. Hasa, raia wa kigeni na makabila ya watu wachache wanaozungumza lugha tofauti na kundi kubwa katika nchi fulani hawawezi hata kuelewa lugha inayotumika katika kuendesha kesi zao za jinai, ikipunguza uwezo wao wa kujitetea kwa ufanisi. Zaidi ya athari katika uwezo wa mshtakiwa kuelewa kesi inavyoendeshwa na kuweza kujitetea, raia wa kigeni na makabila madogo pia mara nyingi watakuwa hawajui mchakato na taratibu za kisheria, wana ufahamu mdogo wa haki zao, wanakabiliwa na vikwazo vya kifedha, na hawana mtandao wa kijamii unaowaunga mkono.¹⁸³ Matatizo haya ni makubwa hasa barani Afrika, kwa sababu ni "ni mahali ambapo huzungumzwa takriban theluthi moja ya lugha za ulimwengu."¹⁸⁴ Aidha, urithi wa ukoloni wa Afrika umesababisha mipaka ya nchi kuchorwa kwa njia ambayo haiakisi sifa za kitamaduni na kijamii za watu wao, mara nyingi ikigawanya makabila katika nchi kadhaa na kusababisha makundi ya kikabila na lugha ya walio wachache kuwa walengwa wa taratibu za uhalifu katika mifumo ya kikabila ya walio wengi ambayo hufanyika kwa lugha ambayo si yao wenyewe.¹⁸⁵
92. Katika kushughulikia suala hili, Mahakama hii hapo awali imeona kwamba pale ambapo mshtakiwa hawezi kuelewa au kuzungumza lugha inayotumika katika kesi ya jinai, ana haki chini ya Kifungu cha 7(1)(c) cha

¹⁸³ Taarifa ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa, supra n.107. Aidha, watu hawa wako katika hatari kubwa ya kukabiliwa na adhabu ya kifo kwa aina fulani za makosa, kama vile makosa ya dawa za kulevya na ukiukaji wa sheria za kupambana na ugaidi. Angalia Ripoti ya Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Question of the death penalty, A/HRC/51/7, U.N. HUM. RTS. OFFICE HIGH COMM'R, ¶ 30–31 (Julai 26, 2022), <https://worldcoalition.org/document/a-hrc-51-7-advance-edited-version-question-of-the-death-penalty/>.

¹⁸⁴ Introduction to African Languages, THE AFRICAN LANGUAGE PROGRAM AT HARVARD, HARVARD L. SCH., <https://alp.fas.harvard.edu/introduction-african-languages#:~:text=With%20anywhere%20between%201000%20and,more%20than%20one%20million%20speakers> (imefunguliwa mara ya mwisho Agosti 8, 2024).

¹⁸⁵ Angalia Tasew Gashaw, Colonial Borders in Africa: Improper Design and its Impact on African Borderland Communities, WILSON CENTER (Nov. 17, 2017), <https://www.wilsoncenter.org/blog-post/colonial-borders-in-africa-improper-design-and-its-impact-on-african-borderland-communities>.

Mkataba wa Afrika ya kusaidiwa na mkalimani anayezungumza lugha anayoielewa.¹⁸⁶ Jaji Bensaoula alisisitiza zaidi hali muhimu ya haki ya mshtakiwa kuelewa uendesaji wa kesi kwenye maoni yake tofauti katika kesi ya Zabron, akisema kwamba "hakuna shaka kwamba haki ya kusikilizwa kwa haki ni pamoja na 'haki ya kushiriki katika uendesaji wa kesi', ambayo inahitaji kwamba mshtakiwa aweze kuelewa uendesaji wa kesi na kujadili na wakili wake masuala yoyote ambayo anaona yanafaa kuibuliwa kwa madhumuni ya utetezi wake. Kwa hivyo msaada wa mkalimani ni muhimu sana kiasi kwamba hauwezi kupuuzwa katika uhusiano kati ya mshtakiwa na wakili wake, lakini lazima upanuliwe hadi kwenye uhusiano kati ya mshtakiwa na majaji wanaoendesha kesi."¹⁸⁷ Vivyo hivyo, katika tamko lake huko Augustino, Jaji Rafaa Ben Achour alisema kwamba "ukosefu wa huduma za ukalimani" katika kesi hiyo ulikuwa na athari kubwa sana kiasi kwamba "ingeweza kubadilisha mwenendo wake", na kwa hivyo Mahakama ilipaswa kuzingatia kuachiliwa huru kwa watu waliohusika katika kesi hiyo au kuamuru kesi hiyo isikilizwe upya.¹⁸⁸ Lakini, kama ilivyojadiliwa zaidi hapa, ukweli ni kwamba haki ya mtuhumiwa ya kupata mkalimani mara nyingi hupuuza kabisa.

93. Vikwazo vya lugha vinavyowakabili watu wa kabila la walio wachache vinaonyeshwa na nchi kama vile Botswana, ambayo ina makabila zaidi ya 30.¹⁸⁹ Wakati makundi nane kati ya makabila haya yana lugha yao ya Taifa ya Kisetswana kama lugha yao ya kwanza¹⁹⁰, lugha rasmi

¹⁸⁶ Angalia Guehi dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 001/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 66–79 (Desemba 7, 2018); Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 102–105 (Juni 4, 2024); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 84 (Septemba 3, 2024) ("Kwa hivyo, ni dhahiri kutokana na usomaji wa pamoja wa [Kifungu cha 7(1) (c) cha Mkataba na Kifungu cha 14 (3) (a) cha ICCPR] kwamba kila mtuhumiwa ana haki ya kupewa mkalimani ikiwa hawezi kuelewa lugha inayotumika kuendesha kesi.").

¹⁸⁷ Angalia Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 20 (Juni 4, 2024) (maoni tofauti ya Jaji Chafika Bensaoula).

¹⁸⁸ Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 7–8 (Septemba 3, 2024) (azimio la Jaji Rafaa Ben Achour).

¹⁸⁹ Mogwe, supra n.112 saa 177.

¹⁹⁰ Id.

inayotumika katika kuendesha kesi nyingi mahakamani ni Kiingereza.¹⁹¹ Hii inaweka mzigo mkubwa kwa washtakiwa wa kesi za jinai, ambao lazima wategemee tafsiri na wakalimani, na washtakiwa jutoweza kuelewa lugha husika kunaweza kuathiri vibaya matokeo ya kesi yao.

94. Kwa mfano, mnamo mwaka 1999, wanaume wawili wa asili ya kabila la walio wachache la Basarwa/San walikutwa na hatia ya mauaji na kuhukumiwa kifo. Si tu washtakiwa walikuwa maskini na wasiojua kusoma na kuandika, lakini pia hawakuzungumza Kisetswana wala Kiingereza. Washtakiwa Wabasarwa walizungumza tu Kisecherechere, lahaja ya Kisesarwa.¹⁹²
95. Walipokata rufaa, washtakiwa walidai kuwa hawakuelewa nyaraka za kukiri kosa ambazo walidhani zilikuwa zimethibitishwa, na waliwasiliana na jaji kwa barua iliyoandikwa kwa niaba yao kwamba hawakuweza hata kuelewa nyaraka za korti, ambazo zilikuwa zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kisesarwa kwenda lugha ya Kisetswana kwenda Kiingereza.¹⁹³ Licha ya hayo, hakuna wakili mpya wa umma aliyeteuliwa, wala mtafsiri rasmi hakuwepo.¹⁹⁴
96. Kisa kama hicho kiliripotiwa nchini Cameroon mwaka 2021.¹⁹⁵ Kesi hiyo, ambapo wanaume 4 walihukumiwa kifo na mahakama ya kijeshi, ilikuwa na dosari kwa sababu ya vikwazo vya lugha.¹⁹⁶ Kesi iliendeshwa kwa

¹⁹¹ Fewdays Miyanda, Problems Faced by Court Interpreters in Botswana, ukurasa wa 44 (2019), <https://journals.co.za/doi/pdf/10.10520/AJA18167659>

29#:~:text=Despite%20the%20fact%20that%20the, to%20conduct%20their%20legal%20affairs

¹⁹² Mogwe, supra n.112 saa 177.

¹⁹³ Id.

¹⁹⁴ Id. Msaada wa kupewa mkalimani bila malipo unahitajika chini ya kifungu cha 14(3)(f) cha ICCPR. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, UU.N.T.S 171, juzuu ya 999, kifungu cha 14(3)(f) (Des. 19, 1966).

¹⁹⁵ Kamerun ni taifa linalokomesha adhabu ya kifo kivitendo. Jamhuri ya Kamerun (Kamerun), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Machi 26, 2012), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=13>.

¹⁹⁶ Death Sentences and Executions in 2021, AMNESTY INT'L, ukurasa wa 54, <https://www.amnesty.org/en/documents/act50/5418/2022/en/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 2, 2024).

Kifaransa na kutafsiriwa kwa Kiingereza licha ya ukweli kwamba washtakiwa wengi walielewa tu Kiingereza cha pijini.¹⁹⁷

97. Zaidi ya hayo, katika kesi ya Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyoamuliwa mwezi Septemba mwaka huu, Mahakama hii ilibaini kuwa Tanzania "ilikiuka Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba, kama kinavyosomwa pamoja na Kifungu cha 14(3)(a) cha ICCPR, kuhusu madai ya kushindwa kuwapa Waleta Maombi huduma za ukalimani wakati wa kuhojiwa, kuwekwa kizuizini na kusikiliza kesi."¹⁹⁸ Katika kesi hii, watu wawili walihojiwa na kesi iliendeshwa kwa Kiswahili, lugha ambayo hawakuielewa kikamilifu.¹⁹⁹ Kwa hivyo, Mahakama hii ilibaini kuwa watu hao "hawakuweza kushiriki kikamilifu katika uendeshaji wa kesi hizo."²⁰⁰

98. Kutoa adhabu ya kifo kwa mtu ambaye hawezi kuelewa na kushiriki katika uendeshaji wa kesi kwa sababu ya vikwazo vya lugha (au kabila) ni ukiukaji wa ulinzi wa Mkataba wa mchakato unaostahili na marufuku yake ya kuondoa uhai kiholela.

6. *Makundi ya Kisiaa*

99. Adhabu ya kifo pia hutumiwa kulenga makundi ya kisiasa na wanaharakati wasiopendwa, matumizi ya kiholela kabisa ya adhabu ya kifo kulingana na tofauti za maoni ya kisiasa kati ya watu.

100. Makundi ya wanaharakati wa kisiasa ambayo yanawakilisha walio wachache au wale wanaokosoa au kupinga kundi kubwa la kisiasa linalotawala ni watu wanaoweza kulengwa na ukandamizaji wa serikali wanapokabiliana na mfumo wa haki ya makosa ya jinai. Ukandamizaji huo unaweza kujumuisha, kwa mfano, mateso, uwakilishi wa kisheria ulio

¹⁹⁷ Id.

¹⁹⁸ Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 88 (Septemba 3, 2024).

¹⁹⁹ Id. ¶ 86.

²⁰⁰ Id. ¶ 87.

hafifu, kutopata ufikiaji wa ushahidi, na uwazi mdogo katika kesi za jinai, ambazo kila moja huchangia matokeo ya upendeleo na yasiyo ya haki, ikiwa ni pamoja na kuhusiana na hukumu za kifo.²⁰¹ Hasa, kwa sababu baadhi ya nchi zimehalalisha kuendelea kutumia adhabu ya kifo kwa sababu za ugaidi²⁰² na kwa sababu sheria za ugaidi zinaweza kuwa, na mara nyingi huzuia haki za mshatikiwa kusikilizwa kwa haki²⁰³, adhabu ya kifo inaweza kutumika kiholela chini ya kisingizio cha "kupambana na ugaidi" kulingana na imani za kisiasa za mshtakiwa.²⁰⁴

101. tatizo hili limeonyeshwa nchini Misri.²⁰⁵ Nchini Misri, raia wamekuwa wakishtakiwa kwa makosa yanayohusiana na ugaidi mbele ya mahakama za kijeshi tangu mwaka 1992, ikiwa ni pamoja na wakati wanakabiliwa na mashtaka ambayo yanaweza kusababisha adhabu ya kifo.²⁰⁶ Mahakama hizo za kijeshi zinapuuza dhamana za msingi za kusikiliza kesi kwa haki, kama vile haki ya kusikilizwa hadharani mbele ya mahakama huru na isiyo na upendeleo.²⁰⁷ Zaidi ya hayo, kuanzia mwaka 2017, mamlaka ya kisheria juu ya uhalifu fulani unaohusiana na siasa na ugaidi, ikiwa ni pamoja na ule ambao unaweza kusababisha adhabu ya kifo, yaliwekwa kwenye Mahakama za Dharura ya Usalama wa Nchi, na matumizi ya

²⁰¹ Angalia, kwa mfano, Ruth Michaelson, na Adham Youssef, Egypt Sentences 75 Muslim Brotherhood Supporters to Death, THE GUARDIAN (Sept. 8, 2018), <https://www.theguardian.com/world/2018/sep/08/egypt-sentences-75-to-death-in-rabaa-massacre-mass-trial>; Nigeria: The Ogoni Trials and Detentions, AMNESTY INT'L (Sept. 14, 1995), <https://www.amnesty.org/en/documents/afr44/020/1995/en/>.

²⁰² Nchi ambazo zinadumisha adhabu ya kifo kwa makosa yanayohusiana na ugaidi ni pamoja na: Algeria, Cameroon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Eritrea, Ethiopia, Gambia, Liberia, Libya, Mali, Mauritania, Morocco, Niger, Nigeria, Somalia, Sudan Kusini, Sudan, Tanzania, Tunisia, Uganda, na Zimbabwe. Angalia Death Penalty, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, <https://deathpenaltyworldwide.org/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 2, 2024).

²⁰³ Angalia Martin Scheinin (Mwandishi Maalumu wa Kuhamasisha na Kulinda Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi wakati wa Kupambana na Ugaidi), Rep. on the Promotion and Protection of Human Rights and Fundamental Freedoms while Countering Terrorism, U.N. Doc. A/63/223, ¶ 13 (Agosti 6, 2008).

²⁰⁴ Angalia The Death Penalty, Terrorism and International Law, PENAL REFORM INT'L (2014), <https://www.penalreform.org/resource/death-penalty-terrorism-international-law/>.

²⁰⁵ Tume ya Misri ya Haki na Uhuru imekadiria kuwa, tangu mwaka 2011, zaidi ya watu 57 wamehukumiwa kifo kwa uhalifu unaohusiana na ugaidi. Angalia Trials Data, EGYPT DEATH PENALTY INDEX, <https://egyptdeathpenaltyindex.com/index/trials/> (ilifunguliwa mara ya mwisho Mei 20, 2024).

²⁰⁶ See Justice subverted: trials of civilians before military courts, AMNESTY INT'L, at 1–2 (Agosti 2, 2007), <https://www.amnesty.org/en/documents/mde12/022/2007/en/>.

²⁰⁷ Angalia id. ukurasa wa 2–5 (ikizingatiwa kuwa dhamana za kusikilizwa kwa haki ambazo zinakiukwa ni pamoja na haki ya kusikilizwa hadharani mbele ya mahakama huru na isiyo na upendeleo, haki ya kupata wakili kwa haraka, haki ya kuandaa utetezi wa kutosha, na haki ya kukata rufaa).

mahakama hizo yaliongezeka mwaka 2021.²⁰⁸ Na mwaka 2019, bunge la Misri liliidhinisha marekebisho ya katiba ambayo yalipanua jukumu la mahakama za kijeshi katika kuwashtaki raia.²⁰⁹ Tofauti na mahakama za kawaida, maamuzi ya Mahakama za Dharura ya Usalama wa Nchi "hayawezi kukatiwa rufaa"²¹⁰ na ripoti zinaonyesha kwamba pia hayaheshimu dhamana za msingi za uendeshaji kesi kwa haki, ikiwa ni pamoja na matumizi ya maelezo ya kukiri kosa yaliyopatikana kwa kulazimishwa au kuteswa.²¹¹ Mahakama hizi pia zimeripotiwa kutumika kuwahukumu wapinzani wa kisiasa.²¹² Ingawa hali ya hatari ilifikia kikomo mnamo Oktoba 2021, kesi zilizoanzishwa kabla ya Rais al-Sisi kumaliza hali ya hatari bado ziko chini ya mamlaka ya Mahakama za Dharura ya Usalama wa Nchi, ikiwa ni pamoja na kesi dhidi ya Udugu wa Kiislamu na wafuasi wa rais wa zamani wa Misri Mohamed Morsi.²¹³

102. Kutumia adhabu ya kifo kulenga makundi ya kisiasa yasiyopendwa ni jambo lisilo na mantiki, kwa sababu hukumu ya kifo hutumiwa kama silaha ya kisiasa na si kama kipimo cha haki ya jinai. Matokeo haya yasiyokubaliwa yanachagizwa na ukweli kwamba kesi kama hizo mara nyingi zinaendeshwa bila kuwa na mchakato unaostahili.

* * *

²⁰⁸ Angalia Egypt: President Declares State of Emergency for Health and Security Conditions, LIBR. OF CONG. (Mei 6, 2021), <https://www.loc.gov/item/global-legal-monitor/2021-05-06/egypt-president-declares-state-of-emergence-for-health-and-security-conditions/>.

²⁰⁹ Angalia A Crisis By Design: The Systematic Violation of Human Rights Abuses in Egypt, CAIRO INST. FOR HUM. RTS. STUD., ¶ 33 (Januari 2023), <https://egyptianfront.org/wp-content/uploads/2023/01/Egypt-UPR-Crisis-by-Design-1.pdf>.

²¹⁰ World Report 2022: Events in 2021, HUMAN RIGHTS WATCH, ukurasa wa 215 (2022), https://www.hrw.org/sites/default/files/media_2022/01/World%20Report%202022%20web%20pdf_0.pdf.

²¹¹ Angalia "We Do Unreasonable Things Here." Torture and National Security in al-Sisi's Egypt, HUMAN RIGHTS WATCH (Sept. 5, 2017), <https://www.hrw.org/report/2017/09/06/we-do-unreasonable-things-here/torture-and-national-security-al-sisis-egypt>. Angalia pia Amir Ahmed, Egypt Using Death Sentences to 'Settle Scores,' Lawyer Says, CNN (Jan. 3, 2018), <https://www.cnn.com/2018/01/03/middleeast/egypt-military-courts-executions/index.html>.

²¹² Angalia EGYPTIAN FRONT FOR HUMAN RIGHTS, supra n.79; Ibrahim, supra n.83.

²¹³ Angalia Egypt: Stop Trials by Emergency Courts, AMNESTY INT'L (Oktoba 31, 2021), <https://www.amnesty.org/en/latest/news/2021/10/egypt-stop-trials-by-emergency-courts/>.

103. Kwa ujumla, kwa sababu nyingi, adhabu ya kifo haitaruhusiwa chini ya Kifungu cha 4 hata kama upeo na maana ya Kifungu hiki iliishia kwenye marufuku ya kuondoa uhai kiholela.

C. Utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo unakiuka marufuku ya Kifungu cha 5 kuhusu adhabu ya kikatili, isiyo ya kibinadamu au ya kudhalilisha.

104. Kifungu cha 5 kinasema: "Kila mtu atakuwa na haki ya kuheshimiwa utu wake ambao ni kiini cha mwanadamu na kutambuliwa kwa hadhi yake ya kisheria. Aina zote za unyonyaji na udhalilishaji wa mwanadamu, hasa utumwa, biashara ya watumwa, mateso, ukatili, adhabu au kutendewa kinyama au kwa kudhalilisha ni marufuku." Kwa hivyo, kifungu cha 5, kati ya mambo mengine, kinapiga marufuku adhabu ya kikatili, ya kinyama au ya kudhalilisha ("CIDPT") na mateso.

105. Mahakama hii imesisitiza kwamba "Kifungu cha 5 hakina masharti ya kikomo na kwa hivyo marufuku ya kutojali utu kulikodhihirishwa katika kutendewa kwa ukatili, unyama na udhalilishaji ni kamili" na kwamba "marufuku katika Kifungu cha 5 hutoa ulinzi mpana kadiri iwezekanavyo dhidi ya unyanyasaji wa kimwili na kiakili."²¹⁴ Kwa kuzingatia wigo mpana wa ulinzi unaotolewa na Kifungu cha 5, Mahakama hii pia imeelezea kwamba inapaswa "kuwa na mtazamo chanya katika kutathmini madai mapya ya ukiukaji wa Mkataba."²¹⁵ Mtazamo na mbini hii inaafikiana na marufuku kamili na isiyo ya kawaida kuhusu mateso na CIDPT chini ya sheria za kimataifa.²¹⁶ Kama ilivyojadiliwa hapa chini, adhabu ya kifo

²¹⁴Ombi la Maoni ya Ushauri linalotolewa na Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU) kuhusu Kuafikiana kwa Sheria za Uzururaji na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Vyombo vingine vya Haki za Binadamu vinavyotumika barani Afrika, Na. 001/2018, Hukumu, Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 77 (Des. 4, 2020). Angalia pia Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika wa Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 152 (Septemba 3, 2024) ("... marufuku ya kutendewa kwa ukatili, unyama na udhalilishaji chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba ni dhahiri.").

²¹⁵ Id. ¶ 78.

²¹⁶ Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kiasia ("ICCPR") na Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu ("UDHR") hati hizi zinasema kwamba hakuna mtu atakayepitia mateso au kutendewa kwa ukatili, unyama au udhalilishaji. Angalia International Covenant on Civil and Political Rights, U.N.T.S 171, juzuu ya 999, kifungu cha 7 (Desemba 19, 1966); G.A. Res. 217 (III) A, Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, kifungu cha 5 (Desemba 10, 1948).

inakiuka marufuku ya Kifungu cha 5 kuhusu mateso na CIDPT. Kuanzia wakati mtu anakabiliwa na tishio la Serikali kuondoa uhai wake, hadi kipindi ambacho mtu anawekwa gerezeni akisubiri kifo huku mawazo ya kusubiri kunyongwa yakimwandama, hadi wakati Serikali inatekeleza mauaji ya mwanadamu, hakuna njia ya kuondoa maisha ya mwanadamu ambayo haihusishi CIDPT au mateso. Kwa sababu hizi zote, tunawasilisha kwa heshima kwamba Mahakama hii inapaswa kuona kwamba adhabu ya kifo, adhabu ya kikatili zaidi na isiyo ya kibinadamu, haiwezi kuafikiana na Kifungu cha 5.

106. "Mateso ya Kisaikolojia kwa Mtu Aliyehukumiwa Kifo" ambayo Mahakama hii, pamoja na mashirika mengine na mamlaka ya haki za binadamu ulimwenguni kote, imetambua kuwa ukiukaji wa Kifungu cha 5 huanza wakati mtu anakabiliwa na tishio la Serikali kuondoa uhai wake na yanaendelea katika kipindi chote ambacho mtu anakabiliwa na hukumu ya kifo na mawazo yasiyoisha kwamba atanyongwa.
107. Utoaji wa adhabu ya kifo pia unasababisha mateso ya kinyama kwa wafungwa wa kike waliohukumiwa kifo na wakati mwingine, watoto wao, pamoja na wanafamilia wa wale waliohukumiwa kifo, wakati wanakabiliwa mara kwa mara na jinamizli Serikali kutafuta kuondoa uhai wa mpendwa wao, wakati adhabu ya kifo itakapotekelezwa, wanakabiliwa na hofu kubwa ya kuona serikali ikumuua mpendwa wao. Kwa sababu hizi, utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa unasababisha CIDPT na mateso kwa wanawake, watoto, na wanafamilia wa mtu aliyehukumiwa adhabu ya kifo.
108. Aidha, wakati adhabu ya kifo inatolewa, kitendo cha Serikali cha kumuua mtu kinapaswa kuchukuliwa kuwa ni CIDPT au mateso, na kwa hivyo pia ni ukiukaji wa Kifungu cha 5. Hatimaye, njia za utekelezaji zinazotumika sasa au zinazopatikana kutekeleza hukumu ya kifo kila moja inajumuisha CIDPT na mateso. Hakuna njia ya kumwua mwanadamu ambayo haihusishi CIDPT na mateso.

109. Kwa sababu hizi, tunawasilisha kwa heshima kwamba Mahakama hii inapaswa kuona kwamba sheria na/au taratibu zinazoruhusu utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo zinakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika na kwamba Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu hizo.

- i. "Mateso ya Kisaikolojia kwa Mtu Aliyehukumiwa Kifo" na Matokeo Mengine Yasiyoepukika ya Utekelezaji wa Adhabu ya Kifo Yanajumuisha Vitendo au Adhabu au Mateso ya Kikatili, ya Kinyama na Kudhalilisha

110. Ukweli kwamba adhabu ya kifo inasababisha hofu na mateso ya kisaikolojia yanayojulikana kama Mateso ya Kisaikolojia kwa Mtu Aliyehukumiwa Kifo ni ukiukaji wa wazi wa Kifungu cha 5. Sababu zingine za ukiukaji wa Kifungu cha 5 zinaundwa na matatizo fulani yanayohusiana na kuwahukumu kifo wanawake na kuwafunga gerezani wakisubiri hukumu ya kifo itekelezwe, na kwa mateso wanayopata familia za wale waliohukumiwa kifo.

1. Mateso ya Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa

111. "Mateso ya Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa" ni matokeo yasiyoepukika ya hukumu za kifo yanayotokana na mateso makali ya kiakili ya adhabu ya kifo yanayotokea katika kila hatua ya mchakato: mwanzoni, wakati Serikali inakabiliana na mtu aliye na matarajio ya kunyongwa kwa kumshtaki katika kesi ambayo Serikali inalenga kutoa hukumu ya kifo; wakati wa kesi, wakati hukumu ya kifo inatolewa; baadaye, wakati hukumu ya kifo inathibitishwa kwenye rufaa; na katika kipindi chote ambacho mtu anakabiliwa na adhabu ya kifo akijua kwamba anasubiri kuuawa na Serikali kwa kukusudia. Mahakama hii, pamoja na mahakama nyingine za Afrika na kimataifa, imehitimisha kwamba Mateso ya Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa ni CIDPT na ni kinyume cha Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika na vifungu vinavyolingana vya vyombo vingine vya haki za binadamu. Aidha, wataalamu wa haki za binadamu wameona kuwa athari za Mateso ya

Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa ni kali sana kiasi cha kuwa mateso.

112. Mateso ya Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa yanatambulika sana. Kama ilivyoelezewa na Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu mateso na vitendo vya kikatili, unyama au udhalilishaji ("Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso"), jambo hilo linajumuisha mateso makubwa, ikiwa ni pamoja na "kusubiri kwa muda mrefu na kuwa na kiwewe kuhusu mambo yanayoweza kutokea, kutengwa, kuwa na fursa ndogo kabisa ya kuonana na wanadamu na hata hali za kimwili ambazo zinawakumba baadhi ya wafungwa," hali ambayo inasababisha kiwewe kikubwa kiakili na mateso ya kimwili.²¹⁷
113. Katika kesi ya Marthine Christian Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hukumu iliyotolewa hivi karibuni ya Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama hii imebaini kwamba "hali ya mtu kusubiri kunyongwa kwa asili inaweza kusababisha athari mbaya katika hali ya kisaikolojia ya mtu kutokana na ukweli kwamba mtu anayehusika anaweza kunyongwa wakati wowote."²¹⁸ Katika kesi hizi, Mahakama hii ilibaini ukiukaji wa Kifungu cha 5 kulingana na Mateso ya Kisaikolojia kwa Wafungwa Wanaosubiri Kunyongwa, ikabaini kuwa hali hiyo ilisababisha kiwewe kikubwa na uchungu wa kisaikolojia hadi kuwa kiwango cha CIDPT.²¹⁹

²¹⁷ Ripoti ya mpito ya Mwandishi Maalumu kuhusu mateso na adhabu nyingine za kikatili, za kinyama au za kudhalilisha, A/67/279, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ¶ 42 (Agosti 9, 2012).

²¹⁸Marthine Christian Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 052/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 112 (Dec. 1, 2022); Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 156 (Juni 4, 2024); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 166 (Septemba 3, 2024).

²¹⁹Marthine Christian Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 052/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 114, 116 (Des. 1, 2022); Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 158 (Juni 4, 2024); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 168 (Septemba 3, 2024).

114. Katika kesi zake hadi sasa, Mahakama hii imejikita katika hali zinazohusisha kipindi kirefu cha kusubiri hukumu ya kifo. Kwa umahususi, Mahakama hii ilihitimisha katika kesi ya Zabron "kwamba ucheleweshaji wa zaidi ya miaka mitatu (3) kati ya uthibitisho wa hukumu ya kifo ya mfungwa wakati wa rufaa na utekelezaji ni kitendo au adhabu ya kikatili, unyama au udhalilishaji" na kwa hivyo iligundua kwamba kipindi cha Zabron cha miaka minane akisubiri kunyongwa "ambapo [Zabron] alilazimika kuvumilia hali zilizo katika mazingira ya kusubiri konyongwa na uchungu na msongo wa mawazo wa kuishi na hofu ya kwamba siku moja utanyongwa" baada ya kuhukumiwa kifo kilikuwa CIDPT na kilikiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba. Na katika kesi ya Augustino, Mahakama hii ilisisitiza kwamba ucheleweshaji wa zaidi ya miaka mitatu kati ya uthibitisho wa adhabu ya kifo ya mfungwa wakati wa rufaa na utekelezaji wa adhabu ni CIDPT kwa kuona kwamba miaka zaidi ya minane ya Augustino akisubiri kutekelzwa kwa hukumu ya kifo ni CIDPT kinyume cha Kifungu cha 5 cha Mkataba.²²⁰
115. Wakati Zabron na Augustino walikuwa kwenye kipindi kirefu wakisubiri hukumu ya kifo itekelezwe, "uchungu na msongo wa mawazo" uliosababishwa na "hofu ya kunyongwa" huanza kuanzia wakati Serikali inamtishia mtu hukumu ya kifo, inaendelea katika mchakato wote, na pia inajumuisha kipindi ambacho mtu anakuwa gerezani akisubiri kunyongwa, ikiwa ni pamoja na wakati akifuatilia rufaa na changamoto katika hukumu yake.
116. Mahakama nyingine za haki za binadamu zimetambua ukweli huu. Katika kesi ya Al-Saadoon na Mufdhi dhidi ya Uingereza, Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu iliona kwamba mateso haya, ambayo mahakama pia iliona yanajumuisha kitendo cha kinyama, huanza hata kabla ya kusikiliza

²²⁰Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 166–69 (Septemba 3, 2024).

kesi na kutoa hukumu, na huendelea hadi wakati ambapo mtu anawekwa chini ya ulinzi wa Serikali ambayo inatishia kumpa hukumu ya kifo.²²¹

117. Suala katika kesi ya Al-Saadoon na Mufdhi lilikuwa endapo Kifungu cha 3 cha Mkataba wa Ulaya wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi, ambacho kinasema kwamba "hakuna mtu atakayepewa adhabu au kutendewa kinyama kudhalilishwa," kitakiukwa ikiwa Uingereza ingewasafirisha watu kwenda chini ya ulinzi wa Iraq, ambapo wanaweza kukabiliwa na mashtaka ya jinai yenye adhabu ya kifo.²²² Kwa hivyo, kesi hiyo haikuhusisha kushikiliwa gerezani kwa muda mrefu au hata kuhukumiwa kifo, lakini matarajio tu ya kushtakiwa ambapo Serikali ingeweza kutoa adhabu ya kifo. Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu ilihitimisha kwamba hatua hii yenyewe ingekuwa ukiukaji wa marufuku ya Kifungu cha 3 kuhusu mateso na adhabu au vitendo vya kinyaman na udhalilishaji.²²³

118. Hasa, Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu ilibaini kwamba "kuelewa mapema kutakuwa na kifo mikononi mwa Serikali lazima kulete mateso makali ya kisaikolojia."²²⁴ Kisha mahakama ilibaini, kuhusiana na marufuku ya CIDPT na mateso, kwamba vitendo vya "kinyama" vinajumuisha vitendo vya "makusudi" "vilivyofanywa kwa saa kadhaa" ambavyo husababisha "mateso makali ya kimwili au kiakili" na kwamba vitendo vya "kudhalilisha" ni pamoja na vitendo "vinavyoamsha hisia za woga, uchungu na udhaifu ambavyo vinaweza kuwadhalilisha."²²⁵ Kwa hivyo, mahakama ilisisitiza kwamba "kufukuzwa na Serikali Inayotoa Mkataba kunaweza kusababisha" ukiukaji wa marufuku hii "ambapo sababu za msingi zimeonyeshwa kwa kuamini kwamba mtu anayehusika,

²²¹Angalia kwa ujumla Al-Saadoon na Mufdhi dhidi ya Uingereza, Na. 61498/08, Hukumu, Eur. Ct. H.R. (Aprili 10, 2010).

²²²Angalia Al-Saadoon na Mufdhi dhidi ya Uingereza, Na. 61498/08, Hukumu, Eur. Ct. H.R., ukurasa wa 45 (Aprili 10, 2010).

²²³Al-Saadoon na Mufdhi dhidi ya Uingereza, Na. 61498/08, Hukumu, Eur. Ct. H.R., ¶ 144 (Aprili 10, 2010).

²²⁴Id.115.

²²⁵Id.121.

ikiwa atasafirishwa, atakabiliwa na hatari halisi ya kutendewa" vitendo hivyo.²²⁶

119. Kwa hivyo, Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu iliona kwamba "mateso makali ya kisaikolojia" ya "kukabiliwa na hofu ya kweli ya konyongwa" yalianza wakati mahakama za jinai za Iraq zilikubali kuwa na mamlaka juu ya kesi za waleta maombi kusimama mahakamani kwa ajili ya uhalifu ambao adhabu ya kifo ilikuwa ni moja wapo ya adhabu inayoweza kutolewa, kwamba mateso kama hayo yaliongezeka wakati ambapo Uingereza iliwahamishia waleta maombi hao chini ya ulinzi wa mamlaka ya Iraq, na kwamba "hofu hiyo ya kweli ya kunyongwa...lazima ilikuwa imetoa kiwango kikubwa cha mateso ya kiakili" ambayo "yalijumuisha vitendo vya kinyama kwa maana ya Kifungu cha 3."²²⁷ Kwa hivyo, kwa kuwasafirisha wafungwa kwenda chini ya ulinzi wa mamlaka ya Iraq, mahakama iliona, Uingereza ilikiuka wajibu wake chini ya Kifungu cha 3 cha Mkataba wa Ulinzi wa Haki za Binadamu na Uhuru wa Msingi, kwa sababu ya "sababu kubwa za kuamini kwamba waleta maombi watakaliwa na hatari halisi ya kuhukumiwa kifo na kunyongwa."²²⁸

120. Katika uamuzi wake miaka kadhaa mapema katika kesi ya Soering dhidi ya Uingereza, Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu ilihitimisha kwamba, kwa kiwango ambacho muda ambao mtu anashikiliwa chini ya hukumu ya kifo unakuwa mrefu, hesabu inapaswa kujumuisha kipindi baada ya hukumu ya kifo kutolewa na wakati wa kufuatilia rufaa. Kwa maneno mengine, kipindi ambacho rufaa zinasubiriwa hakipaswi kuondolewa. Mahakama ilielezea kwamba ingawa muda wa kusubiri kunyongwa kati ya kutoa hukumu na kukamilisha mchakato wowote wa rufaa ni "kwa namna fulani ni matokeo ya uamuzi wa mfungwa mwenyewe", "matokeo yake ni kwamba mfungwa aliyehukumiwa anapaswa kuvumilia kwa miaka mingi hali ya kuwa gerezani akisubiri kunyongwa na uchungu na msongo wa mawazo unaoongezeka wa kuishi

²²⁶ Id.123.

²²⁷ Angalia id. ¶¶ 133–37.

²²⁸ Angalia id. ¶¶ 143–44.

huku akijua kifo kinamkabili." ²²⁹ Hapo, mahakama ilibaini kwamba kumsafirisha Soering kwenda Marekani, ambapo atakuwa katika hatari ya kufungwa jela akisubiri kunyongwa na kuteseka kutokana na Mateso ya Kisaikolojia Yanayomkabili Mtu anayesubiri Kunyongwa kama matokeo ya yaliyotajwa awali, kutakiuka Mkataba wa Ulaya wa Haki za Binadamu wa kuzuia mateso na CIDPT.²³⁰ Kwa hivyo, kwa kiwango ambacho Mahakama hii inachagua kuzingatia muda ambao mtu anakabiliwa na hukumu ya kifo, kipindi hicho kinapaswa angalau kujumuisha kipindi ambacho mhusika anatafuta kukata rufaa, kama Mahakama ya Ulaya ilivyoona katika kesi ya Soering. Lakini kwa kweli, ukiukaji wa Kifungu cha 5 haupaswi kutegemea urefu wa muda ambao mtu anakuwa chini ya tishio la hukumu ya kifo. Badala yake, kama Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu ilivyohitimisha katika kesi ya AlSaadoon na Mufdhi, ukiukaji wa marufuku dhidi ya mateso na adhabu au vitendo vya kinyama au udhalilishaji huanza tangu wakati mtu anakabiliwa na hofu kuhusu Serikali kutaka kumhukumu kifo.

121. Mahakama za ndani barani Afrika, pamoja na Mahakama hii, pia zimebaini uhalisia wa Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungu Anayesubiri Kunyongwa na kuainishwa kwake kama CIDPT.²³¹ Mahakama Kuu ya Zimbabwe iliamua katika kesi ya Kamishna wa Haki na Amani wa Kanisa Katoliki nchini Zimbabwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba "tangu wakati anaingia katika chumba jela, mfungwa anaingizwa katika mazingira ya kuondoa utu na hali ya kukaribia kukosa tumaini kabisa" na kwamba mfungwa "anaanza kupitia" Mateso ya Kisaikolojia kwa Kukaa Jela

²²⁹ 229 Soering dhidi ya Uingereza, Na. 14038/88, Hukumu, Eur. Ct. H.R., ¶ 106 (Julai 7, 1989).

²³⁰ Id. ¶ 111.

²³¹ Angalia Kamishna wa Haki na Amani wa Kanisa Katoliki nchini Zimbabwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hukumu, Mahakama Kuu ya Zimbabwe, (4) SA 239 (ZS), (Juni 24, 1993) (ikibaini kuwa kufungwa jela kati ya miaka minne hadi sita chini ya hukumu ya kifo, huku uzito ukizidishwa na hali mbaya ya gereza kwa wanaosubiri kunyongwa, ilikuwa adhabu isiyo ya kibinadamu au ya kudhalilisha, hata pale ambapo hukumu ya awali ilikuwa imewekwa kisheria). Mahakama Kuu ya Zimbabwe ilibaini kwamba "kuna mwafaka mkubwa kwa mahakama na wanataaluma kwa kile linachoitwa 'mateso ya kisaikolojia kwa mtu anayesubiri kunyongwa'. Mengi yamesemwa na kuandikwa na wanasheria, wanasaikolojia na wataalamu wa magonjwa ya akili kuhusu mateso ya akili wanayopitia wafungwa ambao wamehukumiwa kifo. Kufungwa chini ya hukumu ya kifo kumeelezwa kuwa ni mateso makubwa ya kisaikolojia, ambapo wafungwa wengi wanakabiliwa na kuzorota kwa afya kuliko dhahiri na kubadilika kwa haiba yao." Id. ukurasa wa 3.

Akisubiri Kunyongwa baada ya "kuhukumiwa kifo."²³² Ugunduzi huu kwamba wale waliohukumiwa kifo wanaanza kupata Mateso ya Kisaikolojia kwa Kukaa Jela akisubiri Kunyongwa, si tu wakati ambapo michakato ya rufaa imekamilika, ni jambo la kutumia akili ya kawaida. Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso anafasili Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa kuwa ni "kusubiri kwa kiwewe kuhusu mambo yanayoweza kutokea, kutengwa, kuwa na fursa ndogo kabisa ya kuonana na wanadamu," fasili hii inatumika kuanzia wakati wa hukumu, wakati ambapo kusubiri kwa muda mrefu hukumu ya kifo kunaanza, kukiwa na uwezekano wa kifo kukaribia kama moja ya matokeo yanayoweza kutokea.

122. Mahakama nyingine za ndani barani Afrika pia zimekubali uhalisia wa Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa na kuteseka kunakoambatana na mateso hayo. Majaji kadhaa wa Mahakama ya Katiba ya Afrika Kusini katika kesi ya S dhidi ya Makwanyane na Mwingine walibaini athari Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa kwa wale ambao wamelazimishwa kuipata.²³³ Mahakama Kuu

²³² Kamishna wa Haki na Amani wa Kanisa Katoliki nchini Zimbabwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama Kuu ya Zimbabwe, (4) SA 239 (ZS), ukurasa wa 3 (Juni 24, 1993). Mahakama Kuu ya Zimbabwe pia ilijumuisha hitimisho ambalo lilisisitiza umuhimu wa kudumisha marufuku dhidi ya mateso na CIDPT kuhusiana na adhabu ya kifo, ikisema:

"Kwa sababu adhabu haina nafasi katika mpango wa ustaarabu wa kisheria, mtu hawezi kukataa ombi lililotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa haki za kikatiba. Ubinadamu na utu wa mtu binafsi ni sifa za sheria za ustaarabu. Haki lazima itendeke bila upendeleo na kwa mujibu wa mamlaka ya kikatiba. Swali si endapo Mahakama inakubali maovu yaliyofanywa na wafungwa wanne waliohukumiwa, kwani hakika haikubaliani nayo. Ni endapo mateso makali ya kiakili na hofu ya kutisha ya kunyongwa ambayo imewasumbua wakiwa katika jela zao kwa muda mrefu tangu kupitishwa kwa hukumu ya kifo yanaendana na hakikisho dhidi ya adhabu au vitendo visivyo vya kibinadamu au vya kudhalilisha. Kwa maana, kama ambavyo kifungu cha 21 cha Katiba ya India, kifungu cha 15(1) kinasimama kama mlinzi dhidi ya taabu, udhalilishaji na ukandamizaji wa binadamu. Sauti yake ni ile ya haki na usawa Haiwezi kamwe kunyamazishwa kwa sababu wakati wa kutii maagizo yake ulimalizika kwa kupitisha adhabu ya kifo. Inaakisiwa katika hatua zote, kusikiliza kesi, hukumu, kufungwa jela ili kusubiri kunyongwa na hatimaye kunyongwa."

Id. ukurasa wa 28.

²³³ Angalia Serikali dhidi ya T. Makwanyane na M. Mchunu, (16) HRLJ 154 (CC) (S. Afr.), ¶ 55–56 (Juni 6, 1995) (Jaji Chaskalson akibainisha ugumu wa kuweka mfumo ambao unaepuka uholela na Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa na kwamba vipindi virefu mtu akisubiri kunyongwa vimeonekana kuwa ni vya kikatili na vya kudhalilisha); ¶ 196 (Jaji Kentridge akibainisha kwamba Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa, na "n mateso ya kiakili kwa mhalifu, hofu, matumaini na kukata tamaa lazima viwepo hata wakati kati ya hukumu na kunyongwa hupimwa katika miezi au wiki badala ya miaka."); ¶ 234 (Jaji Langa akibaini kwamba Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa yanazidisha ukatili, unyama na udhalilishaji wa

ya Uganda katika kesi ya Mwanasheria Mkuu dhidi ya Susan Kigula na wengine 417 pia ilibaini ukali wa Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa, na kupendekeza kwamba ucheleweshaji usiofaa unaweza kuwa adhabu maradufu. Mahakama iliona kwamba "wakati mtu anatumia haki zake chini ya sheria kutumia taratibu zote kwa mujibu wa sheria kabla hajanyongwa, wakati huo huo [haenda] asiwe katika mazingira mazuri gerezani akitumikia hukumu ambayo hakuhukumiwa kuitumikia."²³⁴ Mahakama ilihitimisha kwa "kuhimiza kwamba Bunge linapaswa kufungua tena mjadala juu ya ulazima wa adhabu ya kifo katika Katiba ya [Uganda], hasa kwa kuzingatia matokeo kwamba kwa miaka mingi hakuna hukumu ya kifo iliyotekelezwa huku watu wanaohusika na hukumu hizo bado wanaendelea kuwa gerezani wakisubiri kunyongwa bila kujua ikiwa walisamehewa, ikiwa hukumu zao ziliondolewa, au wanapaswa kunyongwa."²³⁵

123. Athari za Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa zinawapata si tu na wale waliohukumiwa kifo katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zimeteteleza adhabu ya kifo katika miaka ya hivi karibuni, bali pia wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo katika nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo kivitendo ambazo zinaendelea kutoa adhabu ya kifo kwa idadi kubwa ya watu, hata bila kutekeleza adhabu ya kifo. Kama inavyotambuliwa na Mahakama hii katika kesi ya Msuguri, Zabron, na Augustino, sehemu ya kile kinachofanya Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa kuwa ya kikatili sana, ikipanda kuwa katika kiwango cha CIDPT, ni mfungwa kutokujua atanyongwa lini.²³⁶ Hali hii ya kikatili ya kutokuwa na uhakika inaendeela bila kujali kama Nchi ambayo

adhabu ya kifo); ¶ 249–50 (Jaji Madala akizungumzia athari za tukio Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa).

²³⁴ Mwanasheria Mkuu dhidi ya Susan Kigula na Wengine 417, Rufaa ya Kikatiba Na. 3 ya mwaka 2006, Hukumu, Mahakama Kuu ya Uganda, ukurasa wa 50 (Januari 21, 2009).

²³⁵ Id. ukurasa wa 63.

²³⁶ Marthine Christian Msuguri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 052/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 112 (Dec. 1, 2022); Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 156 (Juni 4, 2024); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 166 (Septemba 3, 2024).

imemhukumu mtu adhabu ya kifo imetekeleza adhabu hiyo katika miaka ya hivi karibuni, na ni jambo kubwa katika Mataifa hayo ambayo yanaendelea kuwaweka idadi kubwa ya watu kwenye hukumu ya kifo hata bila kutekeleza adhabu ya kifo.

124. Kwa mfano, Nigeria, iliwafunga zaidi ya watu 2,000 waliokuwa wakisubiri kunyongwa kufikia mwishoni mwa mwaka 2018, lakini haijatekeleza hukumu ya kifo tangu mwaka 2016.²³⁷ Unyongaji nchini Nigeria hufanywa tu mara magavana wa majimbo watakaposaini hati za kifo, ambapo muda wa kufanya hivyo unaweza kuwa usitabirike kabisa.²³⁸ Baadhi ya wafungwa nchini Nigeria wamekuwa gerezani wakusubiri kunyongwa, wakiwa chini ya kivuli cha Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa, kwa zaidi ya miaka 30, huku wastani wa kipindi cha kukaa jela wakisubiri kunyongwa ukiwa miaka 10 na 15, na kusababisha wakutwe na "magonjwa mbalimbali, huku ugonjwa unaowapata watu wengi ukiwa ugonjwa wa akili."²³⁹ Vivyo hivyo, nchini Tanzania, ingawa unyongaji uliofanywa mara ya mwisho ulifanyika mnamo mwaka 1994 (na kwa hivyo Tanzania inachukuliwa kuwa nchi inayokomesha adhabu ya kifo kivitendo), watu wasiopungua 500 walikuwa jela wakisubiri kunyongwa kufikia mwishoni mwa 2018.²⁴⁰ Nchi nyingine zinazokomesha adhabu ya kifo kivitendo pia zinaendelea kutoa hukumu za kifo, zikiwalazimisha wafungwa wanaosubiri kunyongwa wateseke kwa muda mrefu chini ya tishio la kifo.²⁴¹ Kinachozidisha kiwewe

²³⁷ Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria (Nigeria), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Mei 23, 2019), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=53>.

²³⁸ Angalia Ayodeji Adeyemi, Waiting Endlessly on Nigeria's Death Row, AL JAZEERA (Desemba 4, 2013), <https://www.aljazeera.com/features/2013/12/4/waiting-endlessly-on-nigerias-death-row>.

²³⁹ Id.

²⁴⁰ Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tanzania), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Mei 23, 2019), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=77>.

²⁴¹ Angalia, kwa mfano, People's Democratic Republic of Algeria (Algeria), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Desemba 1, 2011), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=2> (inakadiria watu 1,000 kuwa wamehukumiwa kifo, ingawa unyongaji wa mwisho ulifanywa mwaka 1993); Jamhuri ya Cameroon (Cameroon), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Agosti 6, 2018), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=13> (inakadiria angalau watu 220 wanasubiri kunyongwa kufikia Agosti 2018, ingawa unyongaji wa mwisho ulifanywa mwaka 1997); Jamhuri ya Ghana (Ghana), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Mei 29, 2019), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#/results/country?id=27> (inakadiria angalau watu 172 wanasubiri kunyongwa mwishoni mwa mwaka 2018, ingawa unyongaji wa mwisho ulifanywa mwaka 1993); Jamhuri ya Kenya (Kenya), CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY

kinachotokana na kukaa jela kwa muda mrefu wakisubiri kunyongwa ni ukweli kwamba wafungwa wanaosubiri kunyongwa mara nyingi wanawekwa katika vyumba vya gereza huku wakiona sehemu ambapo watanyongwa. Kwa mfano, katika Gereza Kuu la Zomba nchini Malawi, nchi nyingine mwanachama wa Umoja wa Afrika inayokomesha adhabu ya kifo kivitendo, kwa kawaida uwanja uliowekwa kwa ajili ya matumizi ya wafungwa wanasubiri kifo una jukwaa la kunyongwa katika upande mmoja.²⁴²

125. Aidha, mbali na CIDPT, Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa yanapanda na kuwa kiwango cha utesaji. Kama ilivyokubaliwa na Mahakama Kuu ya Zimbabwe katika kesi ya Kamishna wa Kanisa Katoliki, "kufungwa chini ya hukumu ya kifo kumeelezwa kuwa ni mateso makubwa ya kisaikolojia...."²⁴³ Aidha, kama ilivyojadiliwa katika aya ya 140, infra, adhabu ya kifo inalazimisha matumizi ya vitendo ambavyo kwa muda mrefu vimechukuliwa kuwa ni mateso, ikiwa ni pamoja na kwa sababu mashtaka yanayosababisha adhabu ya kifo na hukumu za kifo si zaidi ya vitisho vya serikali na kwa sababu mfungwa anayenyongwa anapata madhara sawa ya kisaikolojia sawa na mfunguwa anayejua kwamba ipo siku atanyongwa. Katika ngazi ya kimataifa, wataalamu kutoka Umoja wa Mataifa pia wameona kuwa Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa ni utesaji. ²⁴⁴ Mwandishi Maalumu wa zamani wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso, Manfred Nowak, alibainisha

WORLDWIDE (Juni 5, 2019), <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#!/results/country?id=38> (inakadiria watu 650 wanasubiri kunyongwa, ingawa unyongaji wa mwisho ulifanywa mwaka 1986 au 1987).

²⁴² Death-Sentenced Prisoners: Description of Prison Conditions, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, <https://deathpenaltyworldwide.org/database/#!/Results/?search> (imesasishwa mara ya mwisho Septemba 6, 2018).

²⁴³ Kamishna wa Haki na Amani wa Kanisa Katoliki nchini Zimbabwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama Kuu ya Zimbabwe, (4) SA 239 (ZS), ukurasa wa 3 (Juni 1993).

²⁴⁴ Tume ya Haki za Binadamu ya Marekani pia imebaini kwamba mfungwa aliyefungwa gereza kwa miaka ishirini katika mazingira ya kusikitisha alipata matokeo mabaya sana ya afya ya akili kiasi kwamba muda wake akiwa gereza akisubiri kunyongwa "pamoja na kuwa hali ya kinyama, kikatili, isiyo ya kawaida, na isiyo nzuri ni aina ya mateso." Víctor Saldaño dhidi ya Marekani, Ripoti kuhusu Uzingatiaji wa Sheria (Chapisho), Inter-Am. Comm'n H.R., Ripoti Na. 24/17, Kesi ya 12.254, ¶ 251 (Machi 18, 2017).

uhusiano kati ya adhabu ya kifo na mateso na CIDPT.²⁴⁵ Mrithi wa Nowak, Juan Méndes, pia alielezea kwamba kumhukumu mtu kifo kunawasababishia uchungu mkubwa wa akili kwa sababu ya mazingira ya gerezani na kutokuwa na uhakika ni lini watanyongwa.²⁴⁶ Kwa hivyo alisema kwamba "Nchi zinapaswa kuangalia upya taratibu zao kwa mujibu wa sheria za kimataifa kwa sababu uwezo wa nchi kuweka na kutekeleza adhabu ya kifo unapungua kwani vitendo hivi vinazidi kuchukuliwa kuwa ni mateso."²⁴⁷ Na mwaka 2022, Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso na Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mauaji Nje ya Mifumo ya Kisheria wa Ziada au Mauaji ya Kiholela alitoa taarifa kwamba "haiwezekani kwa nchi kutoa adhabu ya kifo huku wakitimiza wajibu wao wa kuheshimu haki za binadamu za wale waliohukumiwa" - yaani, bila kuwatesa wafungwa wao au kuwaweka chini ya CIDPT-na kwa hivyo "kukomesha adhabu ya kifo ndiyo njia pekee inayofaa."²⁴⁸

126. Kwa muhtasari, kama Mahakama hii ilivyokiri katika kesi ya Msuguri, Zabron, na Augustino, muda uliotumika kusubiri na hali ya mtu kujua kwamba kichwa chake kitaondolewa bila shaka utasababisha mateso ya kisaikolojia kwa kiwango ambacho ni wazi kuwa ni CIDPT, na pia yatakuwa ni mateso, kinyume cha Kifungu cha 5. Kwa kuwa kiwango hiki cha mateso hakiepukiki katika mfumo ambao bado unatumia adhabu ya kifo, adhabu ya kifo haiwezi kutolewa bila kumhukumu mtu huyo apitie mateso ya CIDPT au kuteseka.

2. Wanawake na Watoto Wanaosubiri Kunyongwa

127. Mazingatio maalumu yanapaswa kuwekwa katika hali mbaya zinazowakabili wafungwa wa kike wanaohukumiwa kifo na, wakati mwingine, watoto wao. Hali hizi ni wazi zinajumuisha mateso au CIDPT.

²⁴⁵ Angalia Nicolas Chua & FIACAT, Death Penalty is Torture, Says Expert, WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY (Nov. 29, 2018), <https://worldcoalition.org/2018/11/29/death-penalty-is-torture-says-expert/>.

²⁴⁶ Angalia Taarifa kwa vyombo vya Habari, Death penalty increasingly viewed as torture, UN Special Rapporteur finds, U.N. Press Release (Okt. 23, 2012), <https://www.ohchr.org/en/press-releases/2012/10/death-penalty-increasingly-viewed-torture-un-special-rapporteur-finds>.

²⁴⁷

²⁴⁸ Id.

128. Kuwalinda wanawake gerezani kunatambuliwa katika Kanuni za Umoja wa Mataifa za Kuwatendea Wanawake Wafungwa na Hatua Zisizo za Kuwekwa Kifungano Wanawake Wahalifu ("Kanuni za Bangkok")²⁴⁹ na Kanuni za Kawaida za Umoja wa Mataifa za Kuwatendea Wafungwa ("Kanuni za Mandela"),²⁵⁰ ambazo hutoa maelekezo mahususi kuhusu ulinzi wa wanawake, ikiwa ni pamoja na sheria za kuwatenganisha wafungwa wa kike na wafungwa wa kiume na usimamizi wa moja kwa moja kutoka kwa wafanyakazi wa kike pekee. Licha ya Kanuni za Bangkok na Kanuni za Mandela, wanawake wanaohukumiwa kifo katika magereza barani Afrika mara nyingi wanakabiliwa na hali za kikatili kinyume cha sheria hizi.²⁵¹ Matatizo mahususi yanawakabili wanawake wenye watoto wanaosubiri kunyongwa, ambao ama wametengwa na watoto wao huku wakisubiri mwisho wa maisha yao au vinginevyo wanalazimika kuwalea watoto wao wakiwa gerezani wakisubiri kunyongwa, jambo ambalo katika hali zote mbili litakuwa na athari dhahiri na ya kudumu kwa afya ya akili ya mama na mtoto.²⁵²

²⁴⁹ Kanuni za Umoja wa Mataifa za Kuwatendea Wafungwa Wanawake na Hatua Zisizo za Kuwekwa Kifungoni Wanawake Wahalifu (Kanuni za Bangkok), zilizopitishwa katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa tarehe 21 Desemba 2010, <https://cdn.penalreform.org/wp-content/uploads/2016/07/BangkokRules-Updated-2016-with-renumbering-SMR.pdf>.

²⁵⁰ Kanuni za Kawaida za Umoja wa Mataifa kuhusu Kuwatendea Wafungwa (Marekebisha ya 2015) (Kanuni za Nelson Mandela), zilizopitishwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa tarehe 17 Desemba 2015, <https://cdn.penalreform.org/wp-content/uploads/1957/06/ENG.pdf>.

²⁵¹ Angalia, kwa mfano, Prison Conditions for Women Facing the Death Penalty, A Factsheet, PENAL REFORM INT'L na CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, 3 (2018), <https://deathpenaltyworldwide.org/wp-content/uploads/2020/02/Prison-conditions-for-women-facing-death-penalty.pdf> (ikizingatiwa kuwa nchini Tanzania wanawake wanaweza kuwa walengwa wa unyanysaji kutoka kwa walinzi wanaume, kama vile kuhitaji upendeleo wa ngono kwa kubadilishana na mahitaji ya msingi kama vile chakula); Judged for More Than Her Crime, ukurasa wa 21-22 (kikijadili Malawi, ambapo baadhi ya wafungwa wa kike wanaosubiri kunyongwa wanaohitaji kwenda haja ndogo au haja kubwa wakati wa usiku lazima watumie ndoo zilizo kwenye chumba chao cha gereza, na Zambia, ambapo maji yanadhibitiwa na hayatoshi, na kusababisha matatizo makubwa ya usafi, na ambapo wanawake lazima wafue nguo za hedhi kwa kutumia sabuni yasiyotosha au bila sabuni, kwani gereza halitoi sabuni).

²⁵² Angalia, kwa mfano, Prison Conditions for Women Facing the Death Penalty, A Factsheet, PENAL REFORM INT'L na CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE, ukurasa wa 4 (2018), <https://deathpenaltyworldwide.org/wp-content/uploads/2020/02/Prison-conditions-for-women-facing-death-penalty.pdf> (ikibainisha kuwa wanawake wanaohukumiwa kifo nchini Malawi wanatembelewa na familia zao kwa nadra na kwamba nchini Uganda kumekuwa na visa vya watoto wanaoishi na mama zao jela wakisubiri kunyongwa); Judged for More Than Her Crime (kinajadili mfano nchini Sudan ambapo mfungwa wa kike anayesubiri kunyongwa alifungwa kwenye minyororo mizito gerezani huku akiwa na ujauzito wa miezi minane na kumtunza mtoto mdogo).

3. Athari kwa Wanafamilia

129. Marufuku ya CIDPT kwa mujibu wa Kifungu cha 5 pia inahusishwa na athari mbaya za kisaikolojia na kihisia wanazopata wanafamilia wa wale waliohukumiwa kifo, ambazo ni sawa na CIDPT kwa wanafamilia hao.
130. Mashirika anuwai ya Umoja wa Mataifa yametafakari athari za kutolewa kwa hukumu ya kifo au kunyongwa mzazi kwa watoto wake tangu 2013.²⁵³ Athari kwa watoto walio na wazazi waliohukumiwa kifo nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ilijadiliwa mahsusi mwaka 2019 wakati wa kikao cha 65 cha Tume ya Afrika.²⁵⁴
131. Utafiti mmoja uliofanywa nchini Afrika Kusini, uliochapishwa mwaka 1994 (kabla ya kukomeshwa kwa adhabu ya kifo nchini Afrika Kusini), ulibaini kuwa wanafamilia mara nyingi waliathiriwa na kukosa uelewa kuhusu kesi za kisheria, lugha ya kiufundi au rasmi iliyotumika katika kesi hizo, na kukosa ufafanuzi wowote kutoka kwa wakili.²⁵⁵ Familia nyingi zilizochunguzwa hawakujua kwamba mwanafamilia wao alihusika katika aina yoyote ya shughuli haramu, hawakuamini kwamba adhabu ya kifo ilikuwa halali, na walikuwa walishtushwa na kuwa na hali ya kutokuamini kuhusu hukumu hiyo.²⁵⁶ Wanafamilia walielezea kwamba kushuhudia kesi ambayo mpendwa wao alikuwa anakabiliwa na adhabu ya kifo kilikuwa chanzo cha "maumivu yasiyovumilika."²⁵⁷ Athari za kisaikolojia pia zilikuwa na athari za afya kimwili kwa watu ambao walishuhudia wanafamilia wao

²⁵³ Angalia, kwa mfano, Azimio 22/11, Jopo kuhusu haki za binadamu za watoto wa wazazi waliohukumiwa adhabu ya kifo au kunyongwa, A/HRC/Res/22/11, U.N. H.R.C (Aprili 10, 2023), <https://www.refworld.org/legal/resolution/unhrc/2013/en/100464>.

²⁵⁴ Connie Numbi na Bronwyn Dudley, Children and the death penalty in Sub-Saharan Africa: NGO Forum and the 65th ACHPR Session, WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY (Des. 9, 2019), <https://worldcoalition.org/2019/12/09/children-and-the-death-penalty-in-sub-saharan-africa-ngo-forum-and-the-65th-achpr-session/> (inaelezea tukio la pembeni lililoandaliwa na FIACAT na WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY ambapo suala hili lilijadiliwa).

²⁵⁵ C.M. De La Rey, na wengine, Socio-psychological effects of the death penalty on families of prisoners on death row, ACTA CRIMINOLOGICA, Juzuu ya 7 Na.2, ukurasa wa 20, 22 (1994), <https://journals.co.za/doi/pdf/10.10520/AJA10128093> 357.

²⁵⁶ Id.

²⁵⁷ Id.

wakikabili mchakato wa kisheria, ikiwa ni pamoja na shinikizo juu la damu, kuzimia au kufanya hali ya ugonjwa iliyopo kuwa mbaya zaidi.²⁵⁸

132. Athari za hukumu ya kifo zinaendelea muda mrefu baada ya kesi, na kuwaacha wanafamilia katika hali ya kuvunjika moyo na kukata tamaa.²⁵⁹ Familia inakabiliwa na sintofahamu kuhusu lini, au endapo, mwanafamilia wao atakufa na hivyo kuishi katika "hali ya kutokuwa na uhakika" ambamo lazima watafakari kifo cha mwanafamilia wao bila uhakika wowote wa hali hiyo kufikia mwisho kwa amani.²⁶⁰ Aina hii ya huzuni, inayoitwa huzuni ya kutarajia, ni tofauti na huzuni ya kawaida kwa kuwa haipungui kadiri muda unavyokwenda.²⁶¹

133. Wanafamilia wa wale waliohukumiwa kifo pia mara nyingi wanakabiliwa na kutengwa katika jamii yao, kupoteza mawasiliano na wanafamilia wengine, na wanapambana na hisia za "hatia kwa kushirikiana" na "kujilaumu."²⁶² Watoto ambao wanafamilia wao wanahukumiwa kifo au kunyongwa pia wanapata kiwewe kutokana na "unyanyapaa, kufikiriwa vibaya, na kutengwa mbali na usadizi wa asili kama vile jumuiya za kijamii" na "kuaibika, kunyanyaswa, au kutengwa na wengine."²⁶³ Kama utafiti mmoja ulivyosema, wanafamilia "lazima wajue kwamba kifo cha mpendwa wao wengine wanakifurahia sana," ikiongeza maumivu zaidi.²⁶⁴ Uponyaji unakuwa mgumu zaidi kwa wanafamilia kwa sababu huenda wasionekane kwa jamii nzima kuwa wana haki ya kuomboleza.²⁶⁵ Hatimaye, katika hali nyingi, mwanafamilia aliyehukumiwa kifo ama ni chanzo kikuu au chanzo

²⁵⁸ Id.

²⁵⁹ Id. ukurasa wa 22–23.

²⁶⁰ Id. ukurasa wa 23–24.

²⁶¹ Id. ukurasa wa 24.

²⁶² Nobody to Talk To: Barriers to Mental Health Treatment for Family Members of Individuals Sentenced to Death or Executed, TEXAS AFTER VIOLENCE PROJECT REPORT, ukurasa wa 2 (Oktoba. 2019), https://texasafterviolence.org/wp-content/uploads/2021/02/TAVP_Report.pdf; C.M. De La Rey supra n.255 at 23.

²⁶³ Children Who Are Impacted by a Family Member's Death Sentence or Execution: Information for Mental health Professionals, THE NATIONAL CHILD TRAUMATIC STRESS NETWORK (NCTSN) (Desemba 2021), <https://www.nctsn.org/sites/default/files/resources/fact-sheet/children-who-are-impacted-by-a-family-members-death-sentence-or-execution-for-mh-professionals.pdf>.

²⁶⁴ Ripoti Ikielezea Vikwazo vya Kupaa Huduma ya Afya ya akili kwa Wanafamilia wa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa, DEATH PENALTY INFORMATION CENTER (Jan. 2, 2020), <https://deathpenaltyinfo.org/news/report-addresses-death-row-family-members-barriers-to-mental-health-care> (ikinukuu utafiti wa 1983 wa Michael Radelet).

²⁶⁵ TEXAS AFTER VIOLENCE PROJECT REPORT, supra n.262 ukurasa wa 5.

muhimu cha mapato, na kusababisha matatizo ya kifedha kwa familia zao kama matokeo yake.²⁶⁶ Mwakilishi Maalumu wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Ukatili dhidi ya Watoto, Marta Santos Pais, alibainisha kuwa watoto wanaweza kuhisi shinikizo la kuwa "mchuma kipato" wa familia.²⁶⁷ Kwa sababu hiyo, mtoto anakuwa katika hatari ya kudhulumiwa.²⁶⁸ Athari hizi zote pamoja na kiwewe ni sawa na CIDPT ya wanafamilia wa wale waliohukumiwa kifo, kinyume cha Kifungu cha 5.

ii. Adhabu ya Kifo ni Ukiukaji Kabisa wa Kifungu cha 5

134. Kwa kuzingatia mgogoro usiosuluhishwa kati ya utoaji wa adhabu ya kifo na marufuku ya mateso na CIDPT, adhabu ya kifo inapaswa kuonekana kuwa ni ukiukaji wa wazi wa Kifungu cha 5.²⁶⁹

135. Jaji Ntsebeza wa Mahakama hii ameelezea kwa nini adhabu ya kifo ni ukiukaji wa wazi wa Kifungu cha 5 cha Mkataba:

"Adhabu ya kifo si tu ni ukiukaji wa wazi wa Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ("Mkataba") kuhusiana na njia ya kunyongwa kwa kamba kama ilivyotekelezwa na Mjibu Maombi lakini pia, yenyewe inakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba, kwa sababu kwa asili ni kitendo au adhabu ya kikatili, inayodhalilisha na ya kinyama. Adhabu ya kifo ina uwezekano wa kuwa na makosa, lakini matokeo yake hayawezi kubadilishwa. Aidha, haina athari ya kuzuia

²⁶⁶ C.M. De La Rey, supra n.255 ukurasa wa 23.

²⁶⁷ The Death Penalty in the OSCE Area, Background Paper, OSCE's OFFICE FOR DEMOCRATIC TAASISI NA HAKI ZA BINADAMU (ODIHR), ukurasa wa 7 (2017), <https://www.osce.org/files/f/documents/5/5/343116.pdf>.

²⁶⁸ Oliver Robertson na Rachel Brett, Lightening the Load of the Parental Death Penalty on Children, Quaker United Nations Office, ukurasa wa 29 Juni 2013, https://www.quno.org/sites/default/files/resources/Lightening%20the%20Load.Web_.EN_.pdf.

²⁶⁹ Cf. Juan E. Mendez, The Death Penalty and the Absolute Prohibition on Torture and Cruel, Unhuman and Degrading Treatment or Punishment, <https://www.corteidh.or.cr/tablas/r27394.pdf> (ilifunguliwa mara ya mwisho Agosti 8, 2024).

inayoonekana, na matumizi yake ya kibaguzi yanadhoofisha kanuni za msingi za utu wa binadamu, haki, na usawa."²⁷⁰

136. Mahakama ya Katiba ya Jamhuri ya Afrika Kusini ("Mahakama ya Afrika Kusini") vivyo hivyo ilibaini katika kesi ya S dhidi ya Makwanyane kwamba "[adhabu ya kifo] ni . . . adhabu isiyo ya kibinadamu kwa kuwa '... inahusisha, kwa asili yake, kukataa ubinadamu wa mtu aliyenyongwa', na inadhalilisha kwa sababu inamwondolea mtu aliyehukumiwa utu wote na kumchukulia kama kitu kinachopaswa kuuawa na serikali."²⁷¹ Mahakama ya Afrika Kusini ilichunguza malengo ya serikali wakati wa kutekeleza adhabu ya kifo, kupunguza, kuzuia na kulipiza kisasi, na kuyapima dhidi ya adhabu mbadala zinazopatikana kwa ajili ya serikali na sababu zinazofanya adhabu ya kifo kuwa ya kikatili, ya kinyama na ya kudhalilisha.²⁷² Kwa kufanya hivyo, Mahakama ya Afrika Kusini ililinganisha adhabu ya kifo na njia mbadala za adhabu, ikibaini kuwa, ingawa kifungo ni adhabu kali, "kuna tofauti kati ya kukiuka haki kwa madhumuni ya adhabu na kuziharibu kabisa."²⁷³ Kwa hivyo, Mahakama ya Afrika Kusini ilibaini kwamba "adhabu ya kifo ni adhabu ya kikatili, ya kinyama na ya kudhalilisha."²⁷⁴
137. Wasomi wakuu wa haki za binadamu wenye utaalamu katika adhabu ya kifo wameona vivyo hivyo kuwa ni jambo lisilo na mantiki kuona kuuawa kwa mtu kwa mujibu wa hukumu ya kifo kunaruhusiwa, wakati adhabu zisizo za kuua lakini zenye kudhoofisha mwili zinachukuliwa kuwa haramu chini ya sheria za kidesturi za kimataifa.²⁷⁵

²⁷⁰Angalia Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 1–2 (Juni 4, 2024) (tamko la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 1–2 (Septemba 3, 2024) (azimio la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza).

²⁷¹ Serikali dhidi ya T. Makwanyane na M. Mchunu, (16) HRLJ 154 (CC) (S. Afr.), ¶ 26 (Juni 6, 1995) (akinukuu Furman dhidi ya Georgia, 408 Marekani 238, 290 (1972) (Brennan, J., akikubaliana)).

²⁷² Serikali dhidi ya T. Makwanyane na M. Mchunu, ¶ 135.

²⁷³ Id. ¶ 143.

²⁷⁴ Id. ¶ 95.

²⁷⁵Angalia, kwa mfano, John D. Bessler, Human Dignity and the Law's Evolution, in THE DEATH PENALTY'S DENIAL OF FUNDAMENTAL HUMAN RIGHTS: INTERNATIONAL LAW, STATE PRACTICE, AND THE EMERGING ABOLITIONIST NORM, ukurasa wa 227–28 (Cambridge University Press, 2022).

138. Aidha, Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso alionyesha kwamba tofauti ndogo za haki za jumla za kuishi chini ya sheria ya kimataifa, ambazo zimetumika kuhalalisha Mataifa kuendelea kutumia adhabu ya kifo, zinazidi kupungua na kwamba kanuni ya sheria ya kitamaduni inayozuia adhabu ya kifo yenyewe kama aina ya CIDPT au mateso huenda ikawepo tayari.²⁷⁶ Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso aliripoti kwamba kulikuwa na "kiwango kinachobadilika ndani ya vyombo vya kimataifa na utendaji thabiti wa Serikali wa kuanzisha mjadala kuhusu uhalali wa adhabu ya kifo katika muktadha wa dhana za msingi za utu wa binadamu na marufuku ya adhabu au vitendo vya mateso na ukatili, unyama au udhalilishaji."
139. Mtaalam Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso alibaini zaidi kwamba kiwango hiki, ambacho kinaweka kipaumbele kwenye hadhi ya binadamu ndani ya majadiliano ya adhabu, "kilikuwa kinaendelea kuwa kawaida ya sheria ya kitamaduni, ikiwa haijafanya hivyo tayari."²⁷⁷ Aidha, hata kama maendeleo ya kanuni ya kitamaduni kwa kuzingatia adhabu ya kifo ni ukiukaji wa marufuku ya mateso na CIDPT bado haijatambuliwa rasmi, Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso alibainisha kwamba "hali nyingi ambazo adhabu ya kifo inatumika kwa kweli hufanya adhabu iwe sawa na mateso au kitendo cha kikatili, unyama au udhalilishaji."²⁷⁸
140. Tena zaidi, adhabu ya kifo inahusisha vitendo ambavyo kwa muda mrefu vimechukuliwa kuwa mateso. Kwa mfano, mahakama za Umoja wa Mataifa na Marekani zinachukulia vitisho vya kuaminika vya kifo kama aina ya mateso ya kisaikolojia kwa sababu ya kiwewe, maumivu, kuteseka kiakili kunakambatana navyo.²⁷⁹ Na wasomi wamebainisha kwamba,

²⁷⁶Angalia Ripoti ya mpito ya Mwandishi Maalumu kuhusu mateso na adhabu nyingine za kikatili, za kinyama au za kudhalilisha, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, A/67/279, ¶ 72 (Agosti 9, 2012).

²⁷⁷ Id. ¶ 73–76.

²⁷⁸ Id.

²⁷⁹ Angalia Ergün Cakal, Perception, Practice, and Proximity: Qualifying Threats as Psychological Torture in International Law., 31 TORTURE J., ukursa wa 19, 22 (2021); John D. Bessler, Taking

"mashtaka ya makosa ya kifo na hukumu za kifo ni vitisho vya kifo vinavyotolewa na serikali,"²⁸⁰ kwani, baada ya yote, mahakama inayomhukumu mtu adhabu ya kifo inamwambia kihalali kwamba hivi karibuni atauawa. Inaonekana kwamba, ikiwa vitisho vya kifo vinachukuliwa kuwa aina ya mateso, basi adhabu ya kifo inapaswa pia kuchukuliwa hivyo. Vivyo hivyo, nchi nyingi na wasomi wanaainisha hali ya mtu kusubiria kunyongwa ni aina ya mateso ya kisaikolojia.²⁸¹ Mfungwa anayenyongwa anapata hofu sawa na madhara ya kisaikolojia kama mfungwa aliye katika hali ya kusubiri kunyongwa; tofauti pekee ni kwamba mfungwa huyo wa mfano wa pili anaishi. Kwa hivyo, ikiwa hali ya kusubiri kunyongwa ni kitendo cha mateso, basi unyongaji halisi pia ni mateso.²⁸²

141. Kwa sababu hizi zote, tunawasilisha kwa heshima kwamba Mahakama hii inapaswa kuhitimisha kwamba kutoa na kutekeleza hukumu ya kifo ni ukiukaji wa wazi wa marufuku thabiti ya Kifungu cha 5 kuhusu mateso na CIDPT.

iii. Njia zote za Unyongaji ni Zinakiuka Kifungu cha 5

142. Njia zote za kumuua mwanadamu ili kutekeleza adhabu ya kifo zinahusisha CIDPT na mateso, na kwa hivyo hii inaweka sababu ya ziada ambayo kwayo adhabu ya kifo inakiuka Kifungu cha 5.

Psychological Torture Seriously: The Torturous Nature of Credible Death Threats and the Collateral Consequences for Capital Punishment, 11 N.E. U. L. REV., ukurasa wa 1, 7, 12 (2019).

²⁸⁰ John D. Bessler, Taking Psychological Torture Seriously: The Torturous Nature of Credible Death Threats and the Collateral Consequences for Capital Punishment, 11 N.E. U. L. REV., ukurasa wa 1, 10 (2019).

²⁸¹ Id. ukurasa wa 81 (anaelezea jinsi Marekani inachukulia unyongaji wa kutishia kuwa aina ya mateso ya kisaikolojia); Cakal, supra n.279, ukurasa wa 23 (anaelezea jinsi Tume ya Ulaya ya Haki za Binadamu inachukulia unyongaji wa kutishia kuwa aina ya mateso ya kisaikolojia); Linda Piwowarczyk, Seeking Asylum: A Mental Health Perspective, 16 GEO. IMMIG. L.J., ukurasa wa 155, 162 (2001) (anajadili jinsi kuyongwa kwa kutishia kunavyosababisha "madhara makubwa ya kisaikolojia"); Almerindo E. Ojeda, What Is Psychological Torture?, katika THE TRAUMA OF PSYCHOLOGICAL TORTURE: CONCEPTUAL AND NEUROPSYCHOLOGICAL OBSERVATIONS, ukurasa wa 1–3 (akidai kuwa kunyongwa kwa kutishia ni aina ya mateso ya kisaikolojia).

²⁸² John D. Bessler, Taking Psychological Torture Seriously: The Torturous Nature of Credible Death Threats and the Collateral Consequences for Capital Punishment, 11 N.E. U. L. REV., ukurasa wa 1, 79–80 (2019) (marejeleo yameondolewa).

143. Mahakama hii imeona kwamba "njia nyingi zinazotumika kutekeleza adhabu ya kifo zina uwezekano wa kuwa mateso, ukatili, unyama na udhalilishaji kutokana na mateso yatokanayo na adhabu hiyo."²⁸³ Hasa, katika kesi ya Ally Rajabu na wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama ilibaini kuwa kunyongwa kunakiuka marufuku ya Kifungu cha 5 kuhusu mateso na CIDPT, ikibaini kuwa "kumnyonga mtu ni... kudhalilisha" na "bila shaka kunaathiri utu kwa kuzingatia marufuku ya mateso na vitendo vya ukatili, unyama na udhalilishaji."²⁸⁴ Hivi karibuni, katika kesi ya Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama hii ilisisitiza tena kwamba kunyongwa kunakiuka Kifungu cha 5.²⁸⁵

144. Uamuzi wa kimataifa na mamlaka nyingine zimeainisha njia zote za unyongaji zinazotumika sasa (au zinazoweza kupatikana) barani Afrika, kunyonga kwa kamba, kupigwa mawe, kupiga risasi, na kudungwa sindano ya sumu, kuwa kunajumuisha mateso au CIDPT.²⁸⁶ Mwandishi Maalumu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mateso alihitimisha katika ripoti ya mpito ya 2012, ambayo ilizingatia kila moja ya njia hizi za unyongaji, kwamba "hakuna ushahidi dhahiri kwamba njia yoyote ya unyongaji inayotumika leo inatii marufuku ya mateso na ukatili, unyama au

²⁸³Angalia Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 118 (Nov. 28, 2019).

²⁸⁴Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 119–120 (Novemba 28, 2019).

²⁸⁵Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Muhtasari wa Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 151, 199 (Juni 4, 2024) (ikisisitiza kwamba kunyongwa kwa kamba ni njia "ya kudhalilisha kwa asili" ya kunyonga na ikiwaamuru Wajibu Maombi kuchukua hatua zote muhimu za kuondoa "kunyonga kwa kamba" kwenye sheria zao kama njia ya utekelezaji wa hukumu ya kifo); angalia pia Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 1 (Juni 4, 2024) (tamko la Jaji Dumisa Buhle Ntsebeza) (akisema "adhabu ya kifo si tu ni ukiukaji wa wazi wa Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu... kuhusiana na njia ya kunyongwa kwa kamba...lakini pia, yenyewe, inakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba, kwa sababu ni kitendo au adhabu ya kinyama kwa asili."). Angalia pia Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 159 (Septemba 3, 2024) ("... Mahakama inaona kuwa, kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo, kunyongwa kwa kamba bila shaka kunadhalilisha utu kuhusiana na marufuku ya mateso na vitendo vya ukatili, unyama na udhalilishaji.").

²⁸⁶ Angalia *infra* ¶¶ 145–150.

udhalilishaji katika kila kesi. . . . Njia za utekelezaji zitakazotumika sasa zinaweza kusababisha maumivu makali na mateso. Nchi haziwezi kuhakikisha kuwa kuna njia ya unyongaji isiyo na maumivu."²⁸⁷ Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu pia imesema kwamba "bila kujali njia ya unyongaji, uondoaji wa uhai unahusisha maumivu ya kimwili."²⁸⁸ Kila moja ya njia za unyongaji zinazotumika kwa sasa au zinazoweza kupatikana katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo zinaendelea kutoa adhabu ya kifo, kama ilivyoielezwa kwa kina katika Jedwali la 1, hapa chini, zinakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika.

²⁸⁷ Ripoti ya mpito ya Mwandishi Maalumu kuhusu mateso na adhabu nyingine za kikatili, za kinyama au za kudhalilisha, A/67/279, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, ¶ 41 (Agosti 9, 2012).

²⁸⁸ Al-Saadoon na Mufdhi dhidi ya Uingereza, Na. 61498/08, Hukumu, Eur. Ct. H.R., ¶ 115 (Apr. 10, 2010).

Jedwali la 1: Njia za Unyongaji kulingana na Nchi²⁸⁹

Nchi	Njia ya Unyongaji
Algeria	Kupiga Risasi (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka 1992)
Botswana	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa
Burkina Faso	Kikosi cha kufyatua risasi ²⁹⁰ (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka 1988) ²⁹¹
Kameruni	Kupiga Risasi, Kunyonga kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka
Komoro	Kupiga Risasi (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka 1997)

Nchi	Njia ya Unyongaji
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	Kunyonga kwa kamba (kwa raia), kikosi cha kufyatua risasi (kwa jeshi) ²⁹² (unyongaji wa
Misri	Kunyonga kwa kamba (kwa raia), kufyatua risasi (kwa jeshi) ²⁹³
Guinea ya Ikweta	Kupiga Risasi, kunyonga kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka
Eritrea	Kunyonga, kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka 1989)
Eswatini	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka 1992)
Ethiopia	Kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaojulikana mwaka 2007)

²⁸⁹ Isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo, taarifa iliyo katika jedwali lifuatalo imechukuliwa kutoka kwenye ripoti za nchi zilizoandikwa na shirika la World Coalition Against the Death Penalty, kila moja inapatikana katika: <https://worldcoalition.org/resources/the-death-penalty-worldwide/>.

²⁹⁰ Angalia Burkina Faso Coup Attempt Foiled, LOS ANGELES TIMES (Sept. 19, 1989), <https://www.latimes.com/archives/la-xpm-1989-09-19-mn-360-story.html>.

²⁹¹ Burkina Faso imekomesha rasmi adhabu ya kifo kwa uhalifu usio wa kivita. Angalia Burkina Faso has joined the global trend toward abolition of the death penalty in Africa, INTERNATIONAL FEDERATION FOR HUMAN RIGHTS (FIDH), (Juni 6, 2018) <https://worldcoalition.org/2018/06/06/burkina-faso-has-joined-the-global-trend-toward-abolition-of-the-death-penalty-in-africa/>.

²⁹² Angalia Olivier Lungwe Fataki, Towards the abolition of the death penalty in DRC: advances to be confirmed, WORLD COALITION AGAINST THE DEATH PENALTY (Des. 13, 2016), <https://worldcoalition.org/2016/12/13/towards-the-abolition-of-the-death-penalty-in-drc-advances-to-be-confirmed/>.

²⁹³ Angalia Towards the abolition of the death penalty and its alternative sanctions in the Middle East and North Africa: Algeria, Egypt, Jordan, Lebanon, Morocco, Tunisia and Yemen, PENAL REFORM INT'L, ukurasa wa 12 (Machi 2012), <https://cdn.penalreform.org/wp-content/uploads/2013/05/MENA-research-report-on-death-penalty-and-alternative-sanctions-ENGLISH-March-20121.pdf>.

Gambia	Kunyonga kwa kamba, kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Ghana	Kupiga risasi, kunyonga kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Kenya	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Lesotho	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Liberia	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Libya	Kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 2010)
Malawi	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Mali	Kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Mauritania	Kupigwa risasi, kupigwa mawe (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1997)
Moroko	Kupiga Risasi (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1992)
Niger	Kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1976)
Nigeria	Kunyonga kwa kamba, sindano ya sumu, kupiga risasi, kupigwa mawe (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Somalia	Kupiga risasi
Sudan Kusini	Kunyonga kwa kamba
Sudan	Kunyongwa kwa kamba, kupigwa mawe

Nchi	Njia ya Unyongaji
Tanzania	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Tunisia	Kunyonga kwa kamba, kupiga risasi (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Uganda	Kupiga risasi, kunyonga kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Zambia	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)
Zimbabwe	Kunyongwa kwa kamba (unyongaji wa mwisho unaoiulikana mwaka 1994)

1. Kunyonga kwa kamba

145. Kama ilivyojadiliwa hapo juu, Mahakama hii tayari imeona mara kadhaa kwamba kunyongwa kunakiuka marufuku ya Kifungu cha 5 kuhusu mateso na CIDPT.²⁹⁴

²⁹⁴Angalia Ally Rajabu na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 007/2015, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 119–120 (Nov. 28, 2019); Nzigiyimana Zabron dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na. 051/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 151, 199 (Juni 4, 2024); Habyalimana Augustino na Muburu Abdulkarim dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Na.

2. Kupigwa mawe

146. Kupigwa mawe pia ni sawa na mateso au CIDPT chini ya sheria ya kimataifa. Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa imesema kuwa "njia fulani za unyongaji katika hali zote zimepigwa marufuku kwani ni mateso au adhabu ya kikatili, ya kinyama au ya kudhalilisha. . . . Hizi hujumuisha kunyongwa katika vyumba vya gesi, kupigwa mawe, kuchomwa na kuzikwa mtu akiwa hai, kunyongwa hadharani na njia nyingine za kuuawa zenye uchungu na fedheha" (msisitizo umeongezwa).²⁹⁵ Maoni ya Jumla Na. 36 kuhusu Kifungu cha 6 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa ("ICCPR"), ambacho kinashughulikia haki ya kuishi, kinasema kwamba "Nchi ambazo hazijafuta adhabu ya kifo lazima ziheshimu kifungu cha 7 cha [ICCPR], ambacho kinakataza njia fulani za unyongaji. Kushindwa kuheshimu kifungu cha 7 bila shaka kutafanya unyongaji uwe wa kikatili kwa asili na hivyo pia kukiuka kifungu cha 6. Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa tayari imefafanua kwamba kupigwa mawe...[ni] kinyume cha kifungu cha 7" (msisitizo umeongezwa).²⁹⁶ Kwa hivyo imetoa wito kwa Mataifa kurekebisha sheria zao za makosa ya jinai ili kuondoa kupigwa mawe kama njia ya unyongaji.²⁹⁷ Nchi 54 za Afrika zimesaini au kuidhinisha ICCPR na kwa hivyo zimefungwa na vifungu vyake. ²⁹⁸ Mahakama za kimataifa pia zimekubaliana na uainishaji huu wa kupigwa mawe kama njia ya unyongaji ambayo inahusisha CIDPT au mateso. Katika kesi ya Jabari dhidi ya Uturuki, Mahakama ya Ulaya ya Haki za Binadamu iliamua kwamba kuhamishwa kwa mleta maombi kwenda Iran kulivunja marufuku ya CIDPT na mateso, kwa sababu ya hatari kwa mleta maombi kupigwa

015/2016, Hukumu, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 159 (Septemba 3, 2024).

²⁹⁵ Adhabu ya kifo na utekelezaji wa ulinzi unaohakikisha ulinzi wa haki za wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo, A/HRC/42/28, U.N. H.R.C., ¶ 16 (Agosti 28, 2019).

²⁹⁶ Maoni ya Jumla Na. 36 kuhusu Kifungu cha 6: Right to Life, CCPR/C/GC/36, U.N. HUM. RTS. COMM., ¶ 40 (Sept. 3, 2019), <https://www.ohchr.org/en/calls-for-input/general-comment-no-36-article-6-right-life> (msisitizo umeongezwa).

²⁹⁷ Angalia Concluding observations on the fifth periodic report of the Sudan, CCPR/C/SDN/CO/5, U.N. H.R.C., ¶ 30 (Novemba 19, 2018); Concluding observations on the second periodic report of Mauritania, CCPR/C/MRT/CO/2, U.N. H.R.C., ¶ 25 (Agosti 23, 2019).

²⁹⁸ Angalia Ratification Status of the International Covenant on Civil and Political Rights, U.N. TREATY COLLECTION, (ulianza kutumika Machi 23, 1976), <https://treaties.un.org/doc/Publication/MTDSG/Volume%20I/Chapter%20IV/IV-4.en.pdf>.

mawe hadi kufa.²⁹⁹ Kwa hivyo, kupiga mawe ni CIDPT na/au mateso na kunapaswa kupigwa marufuku chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika.

3. *Kupigwa risasi*

147. Nchi kadhaa barani Afrika zimetumia kupigwa risasi kama njia ya kumuua mtu aliyehukumiwa kifo, na angalau nchi moja imefanya hivi mwaka jana.³⁰⁰ Kunyongwa kwa kupigwa risasi au kikosi cha kufyatua risasi kunaweza kuwa na makosa na kuwa tukio linaloweza kuvuta hisia za umma, ³⁰¹ njia zote hizi zinasababisha mateso au CIDPT. Kwa mfano, katika kesi ya Roberto Girón na Pedro Castillo Mendoza dhidi ya Guatemala, Tume ya Haki za Binadamu ya Bara Amerika ("IACHR") ilihitimisha kuwa "kuuawa kupitia silaha za moto kunaweza kusababisha uchungu na mateso ya muda mrefu", kama inavyothibitishwa na ukweli kwamba mmoja wa waliouawa "hakufa wakati wa kufyatuliwa risasi na ilibidi apokee 'pigo la mwisho la kumaliza mateso'" na "unyongaji huo ulitangazwa kwenye televisheni ili kuwafichua wahanga wanaodaiwa kudharauliwa na umma."³⁰² IACHR ilihitimisha pia kwamba "mambo haya yakiwekwa pamoja yanaonyesha kwamba njia ya unyongaji ilisababisha mateso makali ya kimwili na kiakili kwa waathiriwa wanaodaiwa" na

²⁹⁹ Jabari dhidi ya Uturuki, Na. 40035/98, Hukumu, Eur. Ct. H.R., ¶¶ 33-4211 (Oktoba 2000).

³⁰⁰ Angalia, kwa mfano, Naima Said Salah, Somalia's Football Pitch That Doubles as an Execution Ground, BBC (Machi 29, 2024), <https://www.bbc.com/news/world-africa-68675452> (ikisema angalau watu 25 waliuawa kwa kupigwa risasi nchini Somalia mwaka 2023 na kwamba waandishi wa habari wanaalikwa kushuhudia

mauaji na wakazi wa eneo hilo, ikiwa ni pamoja na watoto, hawazuiwi kutazama); Ghana Abolishes the Death Penalty, EQUAL JUSTICE INITIATIVE (Julai 27, 2023), <https://eji.org/news/ghana-abolishes-the-death-penalty/> (akibainisha kuwa Ghana hapo awali ilitumia unyongaji kwa kamba au kufyatua risasi kama njia za unyongaji).

³⁰¹ Hoja hii inaweza kuhusishwa na njia yoyote ya unyongaji uliofanywa hadharani. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa imesema kuwa unyongaji wa hadharani ni

CIDPT. Adhabu ya kifo na utekelezaji wa ulinzi unaohakikisha ulinzi wa haki za wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo, A/HRC/42/28, U.N. HR.C, ¶ 16 (Agosti 28, 2019). <https://daccess-ods.un.org/access.nsf/Get?OpenAgent&DS=A/HRC/42/28&Lang=E>

³⁰² Roberto Girón na Pedro Castillo Mendoza dhidi ya Guatemala, Inter-Am. Comm'n H.R., Ripoti Na. 76/17, Kesi ya 11.686, OEA/Ser.L/V/II.163, doc. 90 ¶¶ 113, 117 (2017). IACHR inatafsiri na kutumia Mkataba wa Marekani wa Haki za Binadamu, ambao unajumuisha marufuku ya mateso au vitendo ay adhabu ya kikatili, ya kinyama, au ya kudhalilisha sawa na Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika. Angala Shirika la Nchi za Amerika, Mkataba wa Amerika wa Haki za Binadamu, O.A.S.T.S. Na. 36, 1144 U.N.T.S. 123, kifungu cha 5, § 2 (Novemba 22, 1969).

kwamba "njia iliyotumika kwa ajili ya utekelezaji wa adhabu ya kifo ilikuwa ya kikatili, ya kinyama na ya kudhalilisha."³⁰³

4. *Sindano ya Sumu*

148. Nigeria ndiyo nchi pekee barani Afrika inayoruhusu kunyongwa kwa kudungwa sindano ya sumu, na bado haijatumia sindano ya sumu katika kunyonga.³⁰⁴ Kwa kiwango ambacho njia hii ya unyongaji inaweza kupatikana katika nchi nyingine Wanachama wa Afrika, inapaswa pia kutambulika kuwa ni ya mateso na/au CIDPT.

149. Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa limesema kuwa matumizi ya dawa za kuua ambazo hazijajaribiwa ni mateso au CIDPT.³⁰⁵ Vivyo hivyo, IACHR ilibainisha katika kesi ya Russell Bucklew dhidi ya Marekani kwamba sindano ya sumu inaweza kuwa mateso au CIDPT kwa sababu "ikiwa itatumika katika unyongaji kwa kutumia itifaki iliyopo ya sindano ya sumu, wakati wa utekelezaji Bw. Bucklew 'atajua anapaliwa na damu yake mwenyewe na akiwa katika maumivu kabla ya pentobarbital kumfanya apoteze fahamu na asihisi maumivu.'"³⁰⁶ Sindano ya sumu pia ingemweka Bucklew katika "hatari fulani ya kuzama kupaliwa na damu yake mwenyewe [na] kutambua hilo, [] kwa kipindi cha hadi dakika nne."³⁰⁷ IACHR ilibaini kuwa "ukali wa maumivu ambayo yangesababishwa chini ya hali kama hizo yanaweza kuwa mateso" na kwamba "katika tukio ambapo Serikali itatambua kuwa kuna hatari kubwa kwamba njia ya fulani

³⁰³ Roberto Girón na Pedro Castillo Mendoza dhidi ya Guatemala, Inter-Am. Comm'n H.R., Ripoti Na. 76/17, Kesi ya 11.686, OEA/Ser.L/V/II.163, doc. 90, ¶¶ 117–118 (2017).

³⁰⁴ Angalia Paulina Lucio Maymon, Nigeria's Debate on Death Penalty: Sign Execution Warrants or Impose a Moratorium?, CORNELL CTR. ON THE DEATH PENALTY WORLDWIDE (Juni 21, 2019) <https://deathpenaltyworldwide.org/nigerias-debate-on-capital-punishment-sign-execution-warrants-or-impose-a-moratorium>.

³⁰⁵ Adhabu ya kifo na utekelezaji wa ulinzi unaohakikisha ulinzi wa haki za wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo, A/HRC/42/28, U.N. HR.C, ¶ 16 (Agosti 28, 2019). <https://daccess-ods.un.org/access.nsf/Get?OpenAgent&DS=A/HRC/42/28&Lang=E>.

³⁰⁶ Russell Bucklew dhidi ya Marekani, Tume ya Amerika ya Haki za Binadamu, Ripoti Na. 71/18, Kesi ya 12.958, OEA/Ser.L/V/II.168, doc. 81, ¶¶ 77–78 (2018).

³⁰⁷ Id. ¶ 78.

ya unyongaji inaweza kusababisha ukiukaji wa wajibu wake wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na kanuni za kisheria za sheria za kimataifa, inapaswa kuacha kuendelea na unyongaji chini ya hali hizo."³⁰⁸

150. Kwa jumla, kila moja ya njia za unyongaji zinazotumiwa sasa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, au zinazoweza kuwepo katika nchi hizo, zinakiuka Kifungu cha 5 cha marufuku ya CIDPT au mateso. Hata hivyo, hata kama kungekuwa na njia fulani ya 'kibinadamu' ya unyongaji ambayo kwa nadharia inaweza kutekelezwa bila kukiuka Kifungu cha 5, matumizi ya adhabu ya kifo kwa uhalisia bado yangekiuka Kifungu cha 5 kwa sababu ya athari zake zingine zisizoepukika, ikiwa ni pamoja na Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfunguwa Anayesubiri Kunyongwa, kama ilivyoelezwa hapo juu.

D. Athari ya jumla ya matatizo yote ya adhabu ya kifo yanaunga mkono uamuzi kwamba adhabu ya kifo haiafikiani na Mkataba wa Afrika na kanuni zingine za msingi za haki za binadamu.

151. Mjadala huo hapo juu unatoa sababu kadhaa ambazo kwazo adhabu ya kifo inakiuka Kifungu cha 4 na Kifungu cha 5 cha Mkataba. Lakini utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo hauhusishi shambulizi moja au mawili ya msingi kuhusu kanuni na ulinzi wa Kifungu cha 4 na 5; unahusisha yote. Kwa hivyo, matatizo haya mengi ya adhabu ya kifo yanapaswa kuzingatiwa kwa ujumla. Athari za jumla zitakapozingatiwa, adhabu ya kifo haiwezi kutolewa au kutekelezwa bila kukiuka Kifungu cha 4 au Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika au kanuni za msingi zilizojumuishwa katika vyombo vingine vya haki za binadamu.³⁰⁹

³⁰⁸ Id. ¶¶ 77–78.

³⁰⁹ Kama ilivyoelezwa hapo awali na Mahakama hii, hata kwa vyombo vya haki za binadamu ambavyo havijaridhiwa na kila Nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika, "Nchi Wanachama wote wa Umoja wa Afrika zimejitolea 'kukuza na kulinda haki za binadamu na watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na vyombo vingine muhimu vya haki za binadamu" na "kwa kujizatiti huku, Nchi Wanachama zimechukua jukumu la kudumisha haki za binadamu kwa kuwaheshimu watu wote walio ndani ya mamlaka yao." Ombi la Maoni ya Ushauri linalotolewa na Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU) kuhusu Kuafikiana kwa Sheria za Uzururaji na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Vyombo vingine vya Haki za Binadamu vinavyotumika barani Afrika, Na. 001/2018, Hukumu, Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶ 35 (Des. 4, 2020).

152. Ukweli kwamba mauaji ya kukusudia ya mwanadamu yanayofanywa na Mwanachama wa Umoja wa Afrika hayawezi kuafikiana na amri ya Kifungu cha 4 kwamba "haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa" au ulinzi wa Kifungu cha 5 kwamba "utu ni kiini cha mwanadamu" na marufuku ya "mateso, adhabu ya kikatili, ya kinyama au ya kudhalilisha" kila mmoja ya haya yanatosha kwa Mahakama hii kuona kwamba adhabu ya kifo inakiuka Mkataba.³¹⁰ Na hata kama migogoro hiyo ya msingi kati ya adhabu ya kifo na kanuni zilizowekwa katika Mkataba wa Afrika na vyombo vingine vya haki za binadamu haikuwepo, matatizo makubwa halisi kuhusu utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo, ikiwa ni pamoja na (1) kuendea kwa matatizo ya mchakato stahiki katika kesi za adhabu ya kifo, (2) utoaji wa adhabu ya kifo kwa ubaguzi na kiholela kwa makundi fulani ya watu, (3) kuteseka kusikoeupika kunakosababishwa na Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa, (4) matatizo mahususi yanayohusiana na kuwahukumu wanawake na watoto adhabu ya kifo na kuwaweka jela wakisubiri kunyongwa, na mateso wanayopitia familia za wale waliohukumiwa kifo, na (5) ukweli kwamba kila njia iliyopo ya unyongaji inajumuisha CIDPT au mateso, pia zinatosha kwa Mahakama hii kuona kwamba adhabu ya kifo inakiuka Mkataba na kanuni za msingi za haki za binadamu.³¹¹

153. Lakini hata kama kila moja kati ya yaliyotajwa hapo juu hayakutosha kwa Mahakama hii kuona kwamba adhabu ya kifo inakiuka Mkataba wa Afrika, athari ya jumla ya masuala haya inatoa sababu ya ziada kwa Mahakama hii kuona kwamba adhabu ya kifo haiwezi kutolewa au kutekelezwa bila kukiuka haki za binadamu za mtu binafsi.

³¹⁰ Angalia supra Kifungu cha 4(A) (adhabu ya kifo kwa asili inakiuka Kifungu cha 4); Kifungu cha 4(C) (ii) (adhabu ya kifo ni ukiukaji kabisa wa kifungu cha 5).

³¹¹ Angalia supra Kifungu cha 4(B)(i) (ukosefu wa mchakato unaostahili katika utoaji wa adhabu ya kifo katika uhalisia); Kifungu cha 4(B)(ii) (utoaji wa kibaguzi wa adhabu ya kifo katika uhalisia); Kifungu cha 4(C)(i) (Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa); Kifungu cha 4(C)(iii) (njia zote za unyongaji zinakiuka Kifungu cha 5).

E. Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu zote zinazoruhusu utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo.

154. Kama ilivyojadiliwa hapo juu, utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo unakiuka Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba na kuendelea kutumia adhabu ya kifo hakupaswi kuruhusiwa tena. Kwa hivyo, tunaomba kwa heshima kwamba Mahakama hii ione kwamba Nchi zote za Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu zozote zinazoruhusu adhabu ya kifo kwa namna yoyote.
155. Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Afrika kinazitaka Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika "kutambua haki, wajibu na uhuru uliowekwa katika Mkataba [wa Afrika] na... kupitisha hatua za kisheria au hatua nyinginezo za kuyatekeleza hayo."³¹² Mahakama hii hapo awali ilipobaini kuwa sheria na/au taratibu fulani za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zinakiuka Mkataba, imetafsiri Kifungu cha 1 kuhitaji kwamba Nchi zote lazima "zirekebishe au zifute [sheria hizo] ili kuzifanya ziafikiane na [Mkataba]."³¹³
156. Kwa hivyo, ikiwa Mahakama hii itaona kwamba sheria na/au taratibu zinazoruhusu utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo zinakiuka Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba, kama inavyopaswa kwa sababu zilizoainishwa hapo juu, Mahakama hii inapaswa pia kuona kwamba Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu hizo.

5. Je, kuna kesi zinazosubiri mbele ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu?

³¹²Kifungu cha 1, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

³¹³Ombi la Maoni ya Ushauri linalotolewa na Chama cha Wanasheria wa Afrika (PALU) kuhusu Kuafikiana kwa Sheria za Uzururaji na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Vyombo vingine vya Haki za Binadamu vinavyotumika barani Afrika, Na. 001/2018, Hukumu, Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu [Afr. Ct. H.P.R.], ¶¶ 153–54 (Desemba 4, 2020) (msisitizo umeongezwa) (ikisisitiza kwamba Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kurekebisha au kufuta sheria zao zote za uzururaji, baada ya kubaini kuwa sheria hizo zinakiuka Mkataba).

157. PALU inawasilisha Ombi hili la Maoni ya Ushauri chini ya Kifungu cha 4 cha Itifaki ya Mahakama na Kanuni ya 82 ya Kanuni za Mahakama.

158. Kifungu cha 4 cha Itifaki ya Mahakama kinaipa uwezo Mahakama ya Afrika kutoa Maoni ya Ushauri:

"kuhusu suala lolote la kisheria linalohusiana na Mkataba au vyombo vingine vyovyote vya haki za binadamu, ikiwa tu mada ya maoni hayo haihusiani na suala linalochunguzwa na Tume."

159. Kwa hivyo PALU kwa heshima inawasilisha kwamba ombi hili la Maoni ya Ushauri ni suala la kisheria linalohusiana na endapo utoaji wa adhabu ya kifo unakiuka vifungu fulani vya Mkataba wa Afrika na vyombo vingine vya haki za binadamu vya Afrika.

160. PALU inaendelea kusema kwamba ombi hili la Maoni ya Ushauri halihusiani na maombi yoyote yanayosubiri mbele ya Tume ya Afrika kulingana na Kanuni ya 82(3) ya Kanuni za Mahakama ya Afrika.

161. Kanuni ya 82(1) ya Kanuni za Mahakama inaeleza kwamba ombi la Maoni ya Ushauri linaweza kuwasilishwa na Shirika la Afrika linalotambuliwa na Umoja wa Afrika. Mahakama hii Tukufu imefasili "shirika" kujumuisha shirika lisilo la kiserikali na imefasili "shirika la Afrika" kurejelea shirika ambalo limesajiliwa katika Nchi ya Afrika, lina muundo katika ngazi za kanda ndogo, kikanda au bara, au linafanya shughuli zake nje ya eneo ambalo limesajiliwa. Kwa hivyo PALU inawasilisha kwa heshima kwamba inakidhi vigezo vyote vilivyowekwa hapo juu kuainishwa kuanishwa kuwa shirika la Afrika.

162. Mahakama hii Tukufu pia imeamua kwamba Umoja wa Afrika kutambua mashirika yasiyo ya kiserikali ni kupitia utoaji wa hadhi ya mwangalizi au kutia saini Mkataba wa Makubaliano kati ya Umoja wa Afrika na mashirika hayo. PALU kwa heshima inawasilisha kwamba kwa sababu ya kutia saini Mkataba wa Makubaliano na Umoja wa Afrika, nakala yake

imeambatishwa hapa kama Kiambatisho B, na baada ya kuonyesha mifano dhahiri hapo kuhusu ushiriki wake na Tume ya Umoja wa Afrika na vyombo na taasisi mbalimbali za Umoja wa Afrika, inatambuliwa rasmi na Umoja wa Afrika, na hivyo kukidhi vigezo vilivyowekwa na Mahakama hii Tukufu.

163. Kwa hivyo, PALU inawasilisha kwa heshima kwamba ni shirika la Afrika linalotambuliwa na Umoja wa Afrika, kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama, na kama ilivyofasiliwa na Mahakama katika busara yake ya kisheria, kuwa imeonyesha kuwa na haki ya kisheria inayohitajika ya kuwasilisha ombi hili la Maoni ya Ushauri.

6. Muhtasari wa Ombi

164. Nchi kadhaa Wanachama wa Umoja wa Afrika zinadumisha sheria zinazoruhusu utoaji wa adhabu ya kifo na zinaendelea kutoa adhabu ya kifo na kutekeleza adhabu ya kifo. Nchi nyingine nyingi za Umoja wa Afrika zimekomesha adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria, zikiweka ukomeshaji huo katika katiba au sheria zao, au zimeondoa ama kusitisha matumizi yake. Mwelekeo huu wa kuondoa adhabu ya kifo barani Afrika unashabihiana na mwenendo kama huo duniani kote na unaonyesha mwafaka wa kimataifa unaokua kwamba utoaji na matumizi ya adhabu ya kifo ni kinyume cha haki za msingi za binadamu.
165. Tunawasilisha kwa heshima kwamba adhabu ya kifo kwa jinsi ilivyo inakiuka ulinzi wa wazi na kamili uliowekwa katika Kifungu cha 4 cha Mkataba wa Afrika, ikiwa ni pamoja na agizo lake kwamba "haki ya binadamu ya kuishi haiwezi kuvunjwa. Kila mwanadamu atakuwa na haki ya kuheshimiwa uhai wake na uadilifu wa utu wake. Hakuna mtu anayeweza kunyimwa haki hii kiholela."
166. Zaidi ya hayo, tunawasilisha kwamba utoaji na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa uhalisia unakiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba, ikiwa ni pamoja na kwa sababu: (i) matatizo ya mchakato stahiki yanayotokana na utoaji wa adhabu ya kifo hufanya matumizi yake yawe ya kiholela; na (ii) adhabu ya kifo hutolewa kwa njia isiyo ya usawa au kiholela, baina ya makundi tofauti ya watu.
167. Hatimaye, tunawasilisha kwamba adhabu ya kifo pia inakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika, ikiwa ni pamoja na kwa sababu: (i) matokeo yasiyoepukika ya kutekeleza adhabu ya kifo, kama vile "Mateso ya Kisaikolojia kwa Mfungwa Anayesubiri Kunyongwa" na athari nyingine za kisaikolojia, matatizo mahususi yanayohusiana na kuwahukumu wanawake na watoto adhabu ya kifo na kuwaweka jela wakisubiri kunyongwa, na maumivu wanayopata familia za wale waliohukumiwa kifo

ni ukatili, adhabu au vitendo visivyo vya kibinadamu au vya kudhalilisha ("CIDPT") au mateso; (ii) uondoaji wa uhai unaofanywa na Serikali kwa wenyewe ni CIDPT au mateso; na (iii) njia za unyongaji zinazotumiwa kwa sasa (au zinazoweza kuwepo) kila moja ni CIDPT au mateso.

168. Kila moja ya yaliyotajwa hapo juu yanatosha kwa Mahakama hii kuona kwamba adhabu ya kifo inakiuka Mkataba. Aidha, athari ya jumla ya kila moja, zikiunganishwa kwa pamoja, inaunga mkono zaidi uamuzi kwamba adhabu ya kifo inakiuka kanuni za msingi za haki za binadamu zilizo katika Mkataba na vyombo vingine vya kimataifa vya haki za binadamu.

169. Kwa hivyo, Mahakama hii inapaswa kuona kwamba kuwepo kwa adhabu ya kifo na namna ya utoaji na utekelezaji wake ni kinyume cha Kifungu cha 4 na Kifungu cha 5 cha Mkataba wa Afrika na kanuni za msingi za sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na kwamba Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika zina wajibu wa kufuta sheria na/au taratibu zozote zinazoruhusu adhabu ya kifo.

Lugha ya mawasiliano inayopendelewa:

Kiarabu

Kiingereza X

Kifaransa

Kireno

Kiswahili

Nyingine (Taja)

Imetiwa saini na kuwekwa tarehe jijini Arusha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 10 Oktoba 2024

Kwa: MWANDISHI/MWAKILISHI

7. Fahirisi ya Viambatisho

A. Orodha ya Mamlaka Zilizotegemewa katika Ombi la Maoni ya Ushauri

- B. Hati ya Makubaliano kati ya Chama cha Wanasheria wa Afrika na Umoja wa Afrika
- C. Jedwali la hali ya sasa ya adhabu ya kifo katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika